**11 APRILI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Nne – Tarehe 11 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita: -

1. Toleo Na. 05 la tarehe 31 Januari, 2025;
2. Toleo Na. 06 la tarehe 07 Februari, 2025;
3. Toleo Na. 07 la tarehe 14 Februari, 2025;
4. Toleo Na. 08 la tarehe 21 Februari, 2025;
5. *Toleo Na. 09 la tarehe 28 Februari, 2025;* **[Toleo hili Liliondolewa Katika Orodha ya Hati Zilizowalishwa Mezani na Spika wa Bunge]**

6. Toleo Na. 10 la tarehe 07 Machi, 2025;
7. Toleo Na. 11 la tarehe 14 Machi, 2025;
8. Toleo Na. 12 la tarehe 21 Machi, 2025;
9. Toleo Na. 13 la tarehe 28 Machi, 2025; na
10. Toleo Na. 14 la tarehe 04 Aprili, 2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu ahsante sana. Hebu angalia pale mbele kwanza, Waheshimiwa Wabunge mvumilie kidogo sekunde chache. Haya ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa wasilisho hilo.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 41

### Ukarabati wa Shule za Msingi – Uyui

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ukarabati wa Shule za Msingi Chakavu za Mtimbola, Mhulidede, Kigwa A, Itobela, Kalola, Igoko, Imalauduki na Ikongolo – Uyui?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ilitumia shilingi milioni 131.1 kwa ajili ya ukarabati na

uboreshaji wa miundombinu kwa Shule za Msingi za Mtimbola, Mhulidede, Kigwa A, Itobela, Kalola, Igoko, Imalauduki na Ikongolo zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Uyui. Aidha, mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali inatarajia kutumia shilingi milioni 80 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu katika Shule za Msingi Kigwa A, Igoko, Itobela, Mhulidede na Imalauduki.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha shule kongwe za msingi kote nchini zikiwemo Shule za Halmashauri ya Uyui kwa awamu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri kabisa kabisa ya Serikali, nina maswali mawili.

Swali la kwanza; hela zilizopelekwa hazikutosheleza, je, Serikali ipo tayari kupanga tena bajeti kwa ajili ya shule hizo hizo kwa sababu walizikarabati pengine vyoo, milango lakini majengo yote ni mabaya sana?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ipo tayari kupokea orodha ya vipaumbele vya shule hizo ili viweze kukarabatiwa na kuokoa majengo ya shule hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Maige, kwamba Serikali, kama ambavyo ilipeleka fedha za ukarabati wa shule hizi kwa awamu ya kwanza iko tayari kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kukarabati shule hizi. Nimhakikishie kwamba tunakarabati kwa awamu. Tuko tayari pia kupokea orodha ya shule nyingine ambazo zinahitaji ukarabati ili Serikali iendelee kutenga bajeti kwa ajili ya kwenda kuziboresha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakarabati Shule ya Msingi Kivava ambayo majengo yake ni chakavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali iliweka utaratibu kwanza wa kutambua na kuainisha shule zote chakavu kote nchini na kutambua Mradi wa *BOOST* ambao unakwenda kukarabati shule zote chakavu za msingi na kwa upande wa sekondari tuna Mradi ya *SEQUIP*. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Vijijini kwamba shule hiyo ya Mpapa aliyoitaja tutaitazama kama imeingia kwenye orodha kwa ajili ya ukarabati na kama haijaingia basi ninamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri awasilishe rasmi Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili itengewe fedha kwa ajili ya ukarabati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba fedha za ukarabati wa shule hizi zipo tayari. Je, ndani ya Jimbo la Temeke, Shule zetu za Yombo Vituka, Azimio na nyinginezo katika kata ni chakavu sana, je, nasi tumo katika idadi hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nirejee jibu langu la msingi kwamba Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati shule chakavu kwa awamu na tayari shule za msingi zimekwishakarabatiwa na shule kongwe za sekondari zimekarabatiwa. Bado tunatambua kwamba kuna shule kongwe ambazo hazijakarabatiwa na zinahitaji ukarabati zikiwemo Shule za Azimio na Shule nyingine ya

Yombo Vituka ambayo Mheshimiwa Dorothy Kilave ameitaja. Ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukarabati shule hizo ili ziwe na ubora unaotakiwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakarabati Shule ya Msingi Gidahababiej Jimbo la Hanang pamoja na shule zingine chakavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, shule chakavu katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang ni miongoni mwa shule ambazo zimeainishwa na baadhi ya shule zimeshakarabatiwa, nafahamu lakini baadhi ya shule bado zinahitaji ukarabati. Kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mbunge, Asia Halamga kwamba tutaendelea kupeleka fedha katika shule hizo ambazo amezitaja na nyingine zote ambazo tutazifanyia tathmini na kuona kwamba zimechakaa na zinahitaji ukarabati ili ziweze kuwa bora na kutoa elimu bora zaidi kwa watoto wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula sasa aulize swali lake. Samahani, Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya kwa niaba ya Mheshimiwa Venant Protas.

Na. 42

**Kuongeza Umri kwa Vijana wa Kiume Wanaopata Mikopo ya Halmashauri**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA K.n.y. MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza umri kwa vijana wa kiume wanaopata mikopo ya halmashauri kufikia miaka 50?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mikopo ya 10% inatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, kifungu cha 37A ya mwaka 2018 na Kanuni za Usimamizi na Utoaji wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2024; ambapo kwa mujibu wa Sheria hii, mikopo ya 10% inatolewa kwa makundi maalumu ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kupata mikopo isiyo na riba. Makundi haya yana fursa ndogo ya kupata mikopo katika taasisi nyingine za fedha kwa kuwa yanakosa dhamana na uwezo mdogo wa kumudu riba. Aidha, umri wa ukomo katika mikopo kwa vijana umeongezwa kutoka miaka 35 hadi 45.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia utoaji wa mikopo hii kwa mujibu wa sheria na kanuni na kufanya maboresho pale itakapohitajika ili kuhakikisha ufanisi na uwiano katika utoaji wa fursa hizi ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa imegundulika kwamba pamoja na kwamba umri uliokuwa umepangwa vijana ni mpaka kufikia miaka 45, lakini bado kuna watu ambao wanaingia umri kufikia miaka 50 hali yao ya kiuchumi inakuwa bado ni mbaya na ni vijana ambao, tuseme ni vijana watu wazima ambao bado wangeweza kusaidiwa ili waweze kufanya shughuli zao vizuri zaidi. Je, kwa nini umri huo usiongezwe ili kuhakikisha kwamba watu wengi wa Tanzania wanaondokana na umaskini na kujikuza kwenye vipato vyao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni kwamba, sasa hivi pia nchi yetu kutokana na jitihada kubwa za uwekezaji wa kiuchumi kwa wananchi wake hali ya maisha ya wananchi *(life span)* imeongezeka kufikia zaidi ya miaka 60. Kwa misingi hiyo kuna watu ambao wanatambulika kama wazee, lakini bado wana

nguvu za kufanya kazi na watu wameachwa kabisa wazee wanaume…

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, wazee wanaume kwa nini nao wasipewe nafasi ya kukopeshwa ili waweze kumudu maisha yao katika hali ya utu uzima walionao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunafahamu kwamba uhitaji wa mikopo ya 10% ni mkubwa zaidi kuliko upatikanaji wa fursa zenyewe; lakini kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo ya 10% ambayo Bunge lako Tukufu liliipitisha, pamoja na kanuni zake za mwaka 2024 mikopo hii inatolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na umri wa ujana ninadhani si miaka 50 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa tunaendelea kutekeleza kwa mujibu wa sheria. Ikibidi na ikionekana ni lazima na inafaa kufanya hivyo basi Serikali itafanya tathimini na kuona uwezekano wa kufanya hivyo. Kwa sasa tutaendelea kutoa mikopo kwa mujibu wa sheria na umri wa kikomo kwa vijana ni miaka 45. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa moja ya kikwazo kinachokwamisha upatikanaji wa mikopo kwa vijana na wanawake waliopo vijijini ni mfumo wa kieletroniki. Je, Serikali inajipanga vipi kuongeza kasi ya kuwaelekeza wanawake na vijana katika Mkoa wa Mtwara ili waweze kuomba mikopo hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, baada ya kuanzisha utaratibu wa kuomba mikopo hii kwa njia za kieletroniki moja ya maboresho ambayo yamefanyika ni kuwahusisha viongozi wa ngazi za serikali za mitaa, serikali za vijiji, kata pamoja na ngazi ya halmashauri. Kuna kamati maalum kabisa katika kila kijiji kwa ajili ya kuratibu na kuelimisha wanufaika wa mikopo ya 10% ili waweze kutumia vizuri mfumo wa kieletroniki.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua kwamba bado kuna changamoto kwa baadhi ya wanufaika kushindwa kuutumia ipasavyo mfumo huu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kutoa elimu na kuhakikisha kwamba katika Mkoa wa Mtwara wananchi wengi wanapata elimu hii, lakini kote nchini ili wote ambao wanahaki ya kunufaika waweze kunufaika bila ya changamoto ya mfumo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa sheria na kanuni zilitungwa na Bunge hili juu ya kutoa mkopo kwa 10%, kwa maana ya nne, nne, mbili (4:4:2) lakini bado mahitaji ni makubwa sana na hasa kama alivyosema muuliza swali la msingi; wazee wamekuwa wengi na wanahitaji kuwezeshwa kiuchumi pia. Je, hatuoni kuna haja sasa Bunge lijalo tuweze kutunga na kubadilisha hii sheria na kuhakikisha na watu wengine wananufaika na mfuko huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine ili tukaifanyie tathmini na kuona uwezekano huo na baada ya hapo Serikali itafanya maamuzi kuona uwezekano wa kuboresha katika eneo hilo. Kwa sasa tutaendelea na utaratibu wa kutoa 10% kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Ujenzi wa Ofisi za Halmashauri ya Wilaya Magu**

**MHE. MARY F. MASANJA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Magu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Jengo la Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Magu linakadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 8.9 mpaka kukamilika, ambapo katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025, Serikali imetoa shilingi bilioni 7.9 na ujenzi umefikia 87%. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ukamilishaji na shilingi milioni 300 kwa ajili ya ununuzi wa samani.

Mheshimiwa Spika, huduma zimeanza kutolewa katika sakafu ya chini na ghorofa ya kwanza kuanzia Februari mwaka huu 2025 na ujenzi unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Juni, 2026. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mary Masanja, swali la nyongeza.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali jengo hili lifikie kwa asilimia 7.9 na tunashukuru kwa sababu tayari sasa hivi wafanyakazi wamekwishahamia katika jengo hilo. Ombi langu tu ni kwamba fedha hizi ambazo tayari wamekwishaidhinisha zipelekwe haraka ili ziweze kumalizia jengo hilo na wananchi, kwa maana ya wafanyakazi, wanaofanya kazi katika jengo hilo

waweze kulitumia ili huduma iweze kutolewa kwa ufanisi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani hilo lilikuwa ni ombi, hivyo mwambie Mheshimiwa Mbunge kuwa umelipokea.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Serikali ya vitendo na vitendo vinaonekana na ndiyo maana tumekwishapeleka bilioni 7.9 na tumeishatenga fedha. Nimhakikishie tu kwamba tutahakikisha fedha hiyo inakwenda na jengo lile linakamilika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Na. 44

**Kumalizia Ujenzi Vituo vya Afya Busokelo**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaunga mkono juhudi za wananchi kwa kumalizia ujenzi wa Vituo cha Afya vya Lupigi, Lufilyo, Kisegese, Lusafi na Kambasegele – Busokelo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Busekelo imepokea shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vinne vya Ntaba,

Mpata, Kifunda na Isange ambapo ujenzi umekamilika na vinatoa huduma.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Lufilyo kinahitaji shilingi milioni 120, Kisegese shilingi milioni 120, Lusasi shilingi milioni 82 na Kambasegela shilingi milioni 120 ili kukamilika. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vituo hivi vya afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze sana Serikali kwa namna ambavyo wanapeleka huduma ya afya ya msingi katika maeneo ya karibu kabisa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nina swali moja la nyongeza. Ipo ahadi ya Serikali ya kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kimkakati. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo kwa ajili ya kusaidia vituo hivyo kujengwa kwa wakati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Ni kweli kwamba Serikali imeshajenga vituo vya afya katika kata takribani 367 za kimkakati kote nchini kwa thamani ya shilingi bilioni 107 katika kipindi cha miaka minne hii ya Serikali ya Awamu ya Sita. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge zoezi hili la ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati ni endelevu na tumekwishaainisha kata za kimkakati kote nchini, tutaendelea kutenga fedha kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani ya halmashauri, Serikali Kuu pia *World Bank* tunaendelea na utaratibu wa kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa hivi vituo vya afya vya kimkakati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe maswali mafupi, nenda moja kwa moja kwenye swali. Shukrani zenu

kwangu nimeshazipokea maana maombi ni mengi na muda wetu ni mchache.

Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini, Kata za Maretadu, Haydarer na Geterer wamejenga vituo vya afya vilivyo katika hatua mbalimbali. Je, lini unapeleka fedha ili kuunga mkono jitihada hizo za wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi..

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge vituo vyote ambavyo vimeanza kujengwa kwa nguvu za wananchi vitaingizwa kwenye bajeti kwa ajili ya ukamilishwaji. Kwa hivyo, tutatoa kipaumbele katika vituo hivyo katika Wilaya ya Mbulu Vijijini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Ilemba, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini yenye wakazi zaidi ya 27,000 haina kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninafahamu kwamba, kata hiyo iliwasilishwa kwenye kata za kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kwa kila Jimbo na mchakato wa kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa hivyo vituo vya afya unaendelea. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hiyo mara itakapopatikana tutapeleka kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hicho kituo cha afya. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Kirua Vunjo Mashariki yenye wakazi wengi, wamechangisha fedha zaidi ya shilingi milioni 30 wakanunua kiwanja ili Serikali iwawezeshe kujenga kituo cha afya. Je, Serikali imejipangaje kwenye jambo hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, niwapongeze Wananchi wa Kata ya Kirua Vunjo Mashariki kwa kuanza michango na kutenga eneo la ujenzi, lakini nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, kuanza kutenga fedha kwenye mapato ya ndani. Pia, kuleta andiko la maombi kwa maana ya mawasilisho ya kata hiyo ya kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa hicho kituo cha afya, ili Serikali iweze kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata ya Ibumu hawana kituo cha afya na wanatembea umbali mrefu sana. Vilevile, Kata jirani ya Image hawana kituo cha afya wote wanaenda Kata ya Ilula ambayo ni umbali mrefu sana na barabara yao ni mbovu. Je, ni lini Serikali itawawekea kituo cha afya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali inatambua uhitaji wa vituo vya afya kwenye kata ambazo zipo mbali zaidi na zina idadi kubwa ya wananchi, lakini safari ni hatua tunakwenda kwa awamu. Nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati tutaendelea kutenga bajeti katika miaka ya fedha inayofuata kwa ajili ya kujenga vituo vya afya katika kata hizo ikiwa zitakuwa zinakidhi vigezo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni sera ya Serikali kwamba wananchi wakijitolea wakakamilisha maboma kuna wajibu wa Serikali sasa kukamilisha ili huduma iweze kupatikana. Kata ya Msikisi, Mkwapa, Chikukwe pamoja na Nangoo wameshakamilisha maboma ya vituo vya afya. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, maboma yote ya zahanati ambayo yamefikia hatua ya *lintel*, Serikali ilishaandaa orodha yake na kila mwaka wa fedha si chini ya shilingi bilioni 15 zimekuwa zikipelekwa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma hayo, ikiwemo katika Jimbo la Ndanda. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mwambe kwamba, maboma hayo yatapelekewa fedha kwa awamu. Vilevile, nisisitize kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Masasi kuanza kutenga fedha kwa mapato ya ndani, kuchangia nguvu za wananchi wakati Serikali Kuu pia ikitafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza. Samahani, Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara ya Waziri Mkuu Jimboni Mwibara mwaka jana aliahidi kwamba, kutajengwa Kituo cha Afya Buramba. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahadi za Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa ni kipaumbele namba moja kwenye mipango yetu ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, ahadi hiyo itatekelezwa. Tumeingiza orodha zote za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwenye mpango kwa ajili ya kuanza utekelezaji mapema iwezekanavyo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wahehsimiwa Wabunge, badala ya kumtaja Mheshimiwa Charles Kajege nilimtaja Mheshimiwa Ally Kassinge. Kwa hivyo, Mheshimiwa Ally Kassinge ninaomba radhi kwa kuchanganya, nilikuwa nimetazama vibaya sehemu aliyokaa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

Na. 45

**Uhitaji wa Umeme kwenye Shule na Taasisi Lindi**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha kupeleka umeme kwenye shule na taasisi zote zikiwepo za dini katika Mkoa wa Lindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini imeendelea kuunganisha umeme katika taasisi nchini ikiwemo taasisi zilizopo katika Mkoa wa Lindi. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2025, jumla ya taasisi 1,272 zimeunganishiwa umeme katika Mkoa wa Lindi zikijumuisha zahanati 259; vituo vya afya 42; hospitali tisa (9); shule za msingi 554; shule za sekondari 151; na taasisi za dini

257 (Misikiti 142 na Makanisa 115). Aidha, kupitia miradi inayoendelea kutekelezwa na kusimamiwa na *REA*, taasisi 27 zinatarajiwa kupatiwa umeme. Vilevile, Serikali itaendelea kuzipatia umeme taasisi, ikizingatiwa kuwa kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha kuwa taasisi zote nchini zinafikiwa na huduma ya umeme. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niipongeze Serikali kwa jitihada ambazo imefanya kuhakikisha kwamba vijiji vyote sasa vinapata umeme kupitia Mradi wa *REA III Round II.* Hongereni sana Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; mzunguko wa kwanza wa utekelezaji wa mradi huu ulihusisha ujenzi wa kilometa moja ambazo ni nguzo 20 kwa kila kijiji, lakini wakandarasi wale walisainishwa mkataba kuhakikisha kwamba wanapeleka kilometa mbili kwa kila kijiji. Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba zile kilometa mbili ambazo waliongezewa wakandarasi hawa zitakamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pia Jimbo la Newala Vijijini zipo taasisi ambazo nazo hazijafikiwa na huduma hii ya nishati ya umeme. Je, ni lini napo umeme utafikiwa ili waweze kunufaika na huduma hii? Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kilometa mbili katika Vijiji vya Jimbo la Newala Vijijini, mkandarasi alichelewa lakini yupo *site*. Tutaendelea kuhakikisha kwamba anaongeza jitihada na kasi ili kilometa hizi mbili zilizobakia na zenyewe ziweze kukamilika na wananchi wengi waendelee kupata huduma hii ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na taasisi tunapotekeleza miradi hii zinafikiwa na huwa ndiyo kipaumbele chetu. Kwa hiyo, kadri ambavyo tunavyoendelea kutekeleza miradi hii tutahakikisha vilevile tunaendelea kufikia taasisi nyingi katika hili Jimbo la Newala Vijijini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama nimewaona, nirejee tena, moja kwa moja kwenye swali. Ukishaanza na maelezo unatuchukulia muda bila sababu na tunaotaka kuuliza maswali tupo wengi.

Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, Makanisa na Misikiti ya Mbogwe hayajapata umeme. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipelekea taasisi hizi umeme? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunayo miradi ya vitongoji ambayo inaendelea katika Jimbo la Mbogwe. Vilevile, tunao mradi mkubwa ambao sasa hivi tumeutangaza na wenyewe utakuja. Tutahakikisha katika utekelezaji wa miradi hii taasisi hizi zinaendelea kufikiwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekamilisha kupeleka umeme vijijini kwenye Jimbo la Tanganyika. Je, Serikali ina mpango gani na mkakati upi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vikubwa vya Ifinsi, Kabatini na Silonge?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, tunayo miradi ambayo inaendelea ukiwemo vitongoji 15 vya Mbunge. Vilevile, katika mradi mkubwa ambao unakuja vitongoji hivi ambavyo

Mheshimiwa Mbunge amevitaja tutaenda kuangalia ili na vyenyewe viweze kufikiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujua ni lini Serikali itawalipisha umeme wa *REA,* wananchi wa eneo la Nyamwaga, Sirari na Nyamongo badala ya kulipishwa bei ya mjini shilingi 320,000 ambayo wananchi wameshindwa kufunga umeme na wanahitaji sana kwa ajili ya maendeleo yao? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, miradi ya kupeleka umeme vijijini ni miradi ambayo inatekelezwa kwa utaratibu, kwa maana ya kupeleka vijijini kwa shilingi 27,000. Kwa maeneo ambayo yapo nje ya wigo huo tunayo miradi mingine ambayo inapeleka umeme ikiwemo miradi ya pembezoni mwa mji ikiwemo *peri urban*. Tutaenda kuangalia kwa miradi ambayo inakuja ya *peri urban,* ili wananchi wao pia waweze kunufaika na miradi hiyo na kuunganishwa kwa bei nafuu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itapeleka umeme wa gridi kwenye mitambo ya kuondoa *fluoride* kwenye maji ambayo imesimikwa Kijiji cha Ngwasenga, Kata ya Leguruki? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nipokee suala hili la Mheshimiwa Mbunge na tutalitazama kwa sababu eneo hilo silifahamu. Tutalitazama halafu baada ya hapo tutampatia majibu sahihi Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, katika Vijiji vya Jimbo la Singida Mashariki vyote 50 vimeshapata umeme. Je, sasa ni lini vitongoji ambavyo vimesalia vitapata umeme vikiwepo vile vitongoji 15 vya Mbunge? Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Ipo mikoa mitatu ambayo ilikuwa bado haijapata mkandarasi (Singida, Mbeya na Tanga). Kwa sasa wakandarasi wameshapatikana na tupo katika hatua za mwisho ili kuwapatia mikataba na kazi iweze kuanza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hivi karibuni mkandarasi atasaini mikataba na ataingia *site*. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kigoma zipo shule za sekondari na msingi pamoja na taasisi za dini zilipeleka maombi ili ziweze kupatiwa umeme, lakini mpaka sasa shule hizo hazijapatiwa umeme. Je, ni lini Serikali itatekeleza maombi hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni kipaumbele cha Serikali pale ambapo tunapeleka umeme kwenye vijiji ama vitongoji, kipaumbele huwa ni taasisi za kijamii, kidini na kiuchumi. Niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge tunapoendelea kutekeleza miradi hii ya kupeleka umeme kwenye vitongoji kwa Mkoa wa Kigoma, tutaendelea kuzingatia kupeleka umeme kwenye taasisi hizi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

Na. 46

**Hitaji la Umeme Vijiji 42 vya Kishapu**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA K.n.y. MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, lini vijiji 42 vilivyobaki vya Wilaya ya Kishapu vitapatiwa umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kishapu lina jumla ya vijiji 117 ambapo hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2025 vijiji vyote 117 sawa na 100% vilikuwa vimekwishaunganishwa na huduma ya umeme kupitia miradi mbalimbali iliyotekelezwa na Serikali. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kuunganisha umeme katika vitongoji vya Wilaya hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna Wilaya kama Kahama na Shinyanga zina kata ambazo zipo vijijini na zinaunganishiwa kwa kigezo cha kwamba zipo mjini; nini kauli ya Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, maeneo ya kiutawala yapo *governed* kulingana na *GN* za Serikali, maeneo ya vijijini, miji na miji midogo. Maeneo yale ambayo yanapata vigezo vya vijijini huunganishiwa umeme kwa shilingi 27,000. Nje ya hapo maeneo hayo yanaunganishiwa umeme kwa shilingi 320,960.

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo yale ambayo wananchi wanapata taabu kuunganisha kwa kuwa uchumi wao ni wa chini,

tunayo mikakati ikiwemo kuweka miradi mbalimbali ya *peri urban* ya pembezoni mwa miji ili wananchi hawa waweze kuunganisha umeme kwa bei rahisi. Kwa maeneo hayo pia tutayazingatia kupeleka miradi hii na wananchi waweze kuunganisha umeme kwa shilingi 27,000 kulingana na miradi ya pembezoni mwa miji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa Maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

Na. 47

**Serikali Kuanzisha Madarasa ya Elimu kwa Mlipakodi**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Madarasa ya Elimu kwa Mlipa Kodi kupitia vikundi vya wanawake wajasiriamali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* imekuwa ikitoa elimu ya kodi kwa njia mbalimbali kwa makundi yote ya walipakodi pamoja na vikundi vya wanawake wajasiriamali. Kwa muktadha huo, *TRA* imekuwa ikielimisha wanawake wajasiriamali kupitia vikundi vyao mbalimbali ikiwemo chemba ya wafanyabiashara wanawake *(Tanzania Women Chamber of Commerce (TWCC))* na makundi mengine ya wajasiriamali wanawake.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha uendelevu wa *TRA* kuwafikia wajasiriamali wanawake, *TRA* itaendelea kushirikiana kikamilifu na Wizara husika kuimarisha mawasiliano na mtandao wa wanawake wajasiriamali, ili kupitia taasisi au jumuiya zao tuweze kukidhi mahitaji ya elimu ya kodi na shughuli zao za kiuchumi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina swali moja la nyongeza. Elimu ya mlipakodi itakuwa imechangia vipi kuboresha usajili wa biashara ndogondogo za wanawake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, elimu ya mlipakodi imeongeza idadi kubwa ya wanawake wajasiriamali ambao wamesajiliwa katika kanzidata ya *TRA* na wanalipa kodi kwa hiari bila shuruti. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 48

**Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Rukwa**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Mkoani Rukwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Matumizi ya Ardhi *(Masterplan)* unaotoa mwongozo wa uboreshaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa tayari umeshakamilika. Kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa Jengo la Damu Salama ambalo limefikia 55% na tayari limeshaombewa fedha kiasi cha shilingi milioni 500 katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Hata hivyo, kwanza ninashukuru kwa kutenga fedha za ujenzi wa wodi za wanawake. Swali la kwanza; kuna uwanja ambao ulitengwa kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Rufaa ambapo ni muda mrefu tumeongelea hapa Bungeni, lakini bado ujenzi haujaanza kwenye ule uwanja ambao upo Kijiji cha Milanzi. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni lini Serikali itatuletea Madaktari Bingwa wa Mifupa katika Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Rukwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu wakati wote amekuwa akija kwa Mheshimiwa Waziri kufuatilia masuala ya msingi yanayohusu afya ya watu wa Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge; kama alivyosema na nimwombe pia tumekuwa tukishirikiana wote katika kutatua pamoja masuala mbalimbali, kwa sababu anajua hospitali ya wilaya ilipo na hospitali ya sasa ilipo, ili tuweze ku-*strategize* vizuri ili kugawa hizi huduma vizuri, ningeomba tukae kwa pamoja tumweleze tunachokifikiria na hii *masterplan* inapanga nini. Kwa pamoja kwa kushirikiana na Wabunge wa Mkoa wa Rukwa, ili tuamue vizuri kwa kuzingatia hii *Masterplan* ambayo tayari tumekuja nayo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu suala la Madaktari wa Mifupa ni suala la msingi sana. Kila kibali kitakapotoka na kwa sababu ameshasema hapa, tutafuatilia hali ilivyo kwenye mkoa wao. Tunajua kuna Madaktari wa Mifupa lakini hawatoshi, tutaangalia na sehemu nyingine. Kama kibali hakijaleta madaktari wao tuone ni wapi wamejaa ili waweze kuhamishiwa kwenye Mkoa wako wa Rukwa na kuhakikisha hilo *gap* limezibwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pale kwenye Hosptilai yetu ya Kwangwa ni lini Serikali itamalizia usimikaji wa *X-rays* ili kuondoa adha ambayo wananchi wanaipata ya kuhamisha wagonjwa na kupeleka katika hospitali ndogo kwa ajili ya kipimo hicho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mbunge tukitoka hapa kwa sababu kama vile anavyojua Rais wetu kwenye eneo hilo la vifaa ameshaweka mkakati mzuri ambao ni wa uhakika, tukae chini halafu tuone kuna shida gani kule na tuwasiliane na *MSD* ili tuje na *plan* ya pamoja kuhakikisha hilo tatizo linatatuliwa mapema zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Arusha ni mkoa ambao umekuwa ukipokea wageni wengi kwa ajili ya mikutano na hata sasa kuna maandalizi ya Mashindano ya *AFCON*. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inaboresha huduma za afya kwa kipindi hiki ambacho tunakuwa na mikutano hiyo na matarajio ya mashindano yanayokuja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimtoe tu wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwenye hilo ambalo amesema. Tayari Serikali imeunda Kamati ya kuhakikisha hayo anayofikiria yamezingatiwa kwa maeneo yote ambayo michezo hiyo itachezwa. Pia, ninampa tu taarifa Mbunge kwamba, Hospitali yake ya *Mount Meru* juzi imechukua nishani, ni mojawapo ya hospitali zinazofanya vizuri sana na akienda sasa hivi ataona uboreshaji unaofanywa kwenye hospitali yao.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu imetengwa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuja na jengo zuri la kisasa ambalo pia litalenga kwenye eneo hili la Tibautalii, kuhakikisha hilo suala ambalo Mheshimiwa Mbunge analisema linaweza kutekelezeka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mkoa wa Simiyu haina wodi za kulaza wagonjwa. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa Wodi za kulaza wagonjwa Hopsitali ya Mkoa wa Simiyu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu, nimetoka na Kamati ya Bunge kwenye Hospitali ya Mkoa wa Simiyu juzi. Ninamhakikishia Mbunge, kwa idadi ya wagonjwa wanaopatikana sasa hivi kwenye Hospitali ya Mkoa wa Simiyu, hata wodi zilizopo hawajai. Ila, ni kweli kwamba, kwa maana ili

hospitali ya mkoa ikamilike ina *wing* mbalimbali zinazotakiwa ziwe zimejengwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, kuna baadhi ya *wing* ambazo zinatakiwa zijengwe hazijajengwa. Ninamhakikishia suala hili liko kwenye *plan* ya mwaka huu. Hizo *wing* zitajengwa, lakini nimtoe wasiwasi, kwa majengo yaliyopo mpaka sasa na vitanda vilivyopo, vitanda ni vingi kuliko wagonjwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Mustafa Mwinyikondo Rajab, Mbunge wa Dimani, sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Fidia kwa Wananchi wa Kisakasaka – Zanzibar**

**MHE. MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB** aliuliza:-

Je, lini JWTZ litafanya uhakiki na kuwalipa fidia wananchi 13 waliobaki katika eneo la Kambi ya Jeshi Kisakasaka Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Taxi, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Mustafa Mwinyikondo Rajab, Mbunge wa Dimani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhakiki wa wananchi waliobaki katika eneo la Kambi ya Jeshi Kisakasaka – Zanzibar ulifanyika tarehe 13 Februari, 2025. Katika uhakiki huo ilibainika kuwa wananchi 11 walistahili kufanyiwa uthamini, na uthamini umekwishafanyika.

Kitabu cha uthamini kimewasilishwa Kamisheni ya Ardhi Zanzibar ili kuweza kuendelea na taratibu zinazofuata, ikiwa ni pamoja na kuidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kitabu hicho kuidhinishwa, Wizara itakiwasilisha Wizara ya Fedha kwa ajili ya maombi ya fedha ili wananchi hao wanaostahili kulipwa fidia waweze kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mustafa Mwinyikondo Rajab, swali la nyongeza.

**MHE. MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi 11 wanaodai fidia, tumeridhika na majibu ya Serikali kwa hatua tuliyofikia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa Olomitu na Moshono waliochukuliwa eneo lao na Jeshi Kikosi Na. 977 ambao wamepimiwa eneo tangu tarehe 31Januari, 2023? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo aliyoyataja ya Moshono na Mlangarine na yenyewe tayari yamekwishafanyiwa uthamini na vitabu vimekwishawasilishwa Hazina kwa ajili ya kulipwa fidia iliyobainishwa na Wizara itaendelea kufuatilia na Serikali italipa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, uongozi wa Wizara ya Ulinzi ulifika Ilalila na kuongea na wananchi katika eneo ambalo walikuwa wanalihitaji kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Je, ni lini sasa Serikali itawalipa wananchi wale fidia wapatao 50?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwapigania wananchi wao katika maeneo husika. Ni kweli tulikwishakwenda na kufanya mazungumzo. Kwa hiyo, tunakamilisha taratibu. Tukishamaliza kukamilisha taratibu uthamini utafanyika na tutaendelea na taratibu zinazofuata, ikiwa ni pamoja na kuyatwaa maeneo tutakayoona tunayahitaji na kuwalipa fidia katika maeneo ambao tutakuwa tumeyachukua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swali lake. Hakuna Mbunge amesimama kuuliza kwa niaba yake?

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Malima ninaomba swali lake lipate majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Nani huyo anaongea? Aah, Mheshimiwa Mkundi ni swali Na. 50. *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Malima ninaomba swali lake Namba 50 lipate majibu ya Serikali.

Na. 50

**Ujenzi wa Daraja la Godegode**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Godegode, ikizingatiwa kuwa Mkandarasi ameshapatikana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Kasekenya Msongwe, majibu

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** aljibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha taratibu za manunuzi ya mkandarasi wa ujenzi wa Daraja la Godegode. Kwa sasa Serikali iko katika hatua za kukamilisha taratibu za kusaini mkataba wa ujenzi. Mara baada ya mkataba kusainiwa kazi za ujenzi zitaanza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Daraja la Rugezi – Kisorya Jimboni Ukerewe ni kiunganishi muhimu sana cha Visiwa vya Ukerewe na Wilaya ya Bunda na ni eneo litakalokuwa muhimu sana kuimarisha uchumi wa Wananchi wa Ukerewe. Ni lini sasa Serikali itajenga daraja hili? Ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Daraja la Rugenzi – Kisorya ni daraja muhimu ambalo linaunganisha Bunda na Wilaya ya Ukerewe na ni kati ya madaraja ambayo ni makubwa kuvuka Ziwa Victoria. Serikali imeshakamilisha usanifu.

Mheshimiwa Spika, wakati tunajiandaa kutafuta fedha za kujenga, tulichofanya ni kuimarisha kivuko na tunajenga kivuko kikubwa kati ya Rugezi na Kisorya, lakini pia tunajenga barabara ya lami ndani ya Ukerewe wakati tunafanya maandalizi ya kuanza kujenga daraja ambalo tayari tumeshakamilisha usanifu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Daraja la Mzinga litaanza kujengwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Daraja la Mzinga ni daraja moja kwa sasa. Tumeshafanya usanifu ambao utakuwa ni *Dual Carriage Way*, yaani itakuwa ni madaraja mawili ambapo tunategemea kuanza kulijenga muda si mrefu kupitia fedha ya *World Bank CRW*. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ni lini ujenzi wa Barabara ya Iringa – Msembe au *Ruaha National Park* utaanza pamoja na madaraja yake? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Msembe pamoja na madaraja ambayo yapo ni barabara ambayo tayari tumeshasaini mkataba na tayari tumeshapata fedha kutoka *World Bank*, ambapo tumeshasaini mkataba. Kwa hiyo, madaraja yaliyopo katika hiyo barabara yatajengwa ikiwa ni

sehemu ya Mradi wa Barabara hiyo, kilometa 103 kutoka Iringa hadi Msembe. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Daraja la Bujonde na Ilondo litaanza kujengwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, daraja analosema ameliuliza mara kadhaa na tayari tumeshafanya usanifu. Kwa hiyo, tunategemea baada ya kutangazwa hilo daraja litaanza kujengwa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Sanzate – Nata imekuwa kero kwa muda mrefu sana. Sasa, ninaomba kujua, Serikali imeitelekeza hiyo barabara au itaendelea nayo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara haijatelekezwa, lakini ni Barabara ambayo tayari mkandarasi ameshaanza, na tunategemea kulipa hati zake za malipo na aweze kuendelea kukamilisha hiyo kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omary Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARY M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, Daraja la Kibirashi linaunganisha Wilaya ya Handeni na Kilindi, lakini limekatika takribani miezi sita sasa. Je, ni lini huduma hiyo itarejeshwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tulishapata makadirio ya Mkoa wa Tanga na kibali kimeshatolewa daraja hilo litangazwe kuanza kujengwa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Hassan Mtenga.

Na. 51

**Uhamasishaji wa Utalii wa Ndani**

**MHE. HASSAN S. MTENGA K.n.y. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhamasisha Watanzania kutembelea hifadhi zetu na kuongeza mapato ya utalii badala ya kutegemea watalii toka nje ya nchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha na kukuza utalii wa ndani, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wadau wa utalii imeendelea kuandaa na kushiriki kampeni na maonesho na matukio mbalimbali ikiwemo 'Twenzetu Kileleni' na "Funga Mwaka Kijanja, Talii".

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara imeshiriki maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), Maonesho ya Wakulima Nanenane, Maonesho ya *Karibu Kili Fair*, Maonesho ya Karibu Kusini, *Serengeti Marathon*, *Kili Marathon*, *Ruaha Marathon, Simiyu Cultural and Tourism Festival, Nyangumi Festival, Kizimkazi Festival, Valentine*

*Gateway na TANAPA,* Shangwe la Sikukuu na *TANAPA*, *Selous Marathon, Kilombero Festival*, na *Mafia Festival*, ambayo yamechangia ongezeko la watalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imeendelea kujenga huduma za malazi za gharama nafuu katika maeneo yenye vivutio vya utalii nchini ili kuendelea kuhamasisha utalii wa ndani. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* limejenga huduma ya malazi katika hifadhi mbalimbali za Taifa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kupitia Mradi wa *REGROW* Serikali ilijenga huduma za malazi zenye jumla ya vitanda 409 katika Hifadhi za Mikumi ambapo tulijenga 116 na Nyerere 120 kwa lengo la kuvutia utalii wa ndani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya maboresho makubwa ya miundombinu ya utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere. Kupitia Mradi wa *REGROW*, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa uwanja wa ndege mkubwa, lango la kisasa la kuingilia Hifadhi ya Mtemerwa. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani awamu ya pili kurekebisha madaraja na mazingira ambayo yapo kwenye mradi huu ujao awamu ya pili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mradi wa *REGROW* una dhamira ya kuhuisha utalii Ukanda wa Kusini, ikiwemo Hifadhi ya Mwalimu Nyerere. Je, Wizara ina mpango gani wa kutangaza Hifadhi ya Mwalimu Nyerere duniani kwa ujumla? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na dhamira yake ya kufungua utalii kwenye mikoa ya kusini na katika hili eneo la madaraja Serikali inaweka kwenye mipango yake kuhakikisha madaraja muhimu yote yanayounganisha au kufungua maeneo haya yanafanyiwa kazi. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge atuunge mkono wakati tutakapowasilisha bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kutangaza Hifadhi ya Mwalimu Nyerere Kimataifa, Wizara kupitia *TTB* na taasisi zetu za utalii inafanya kazi kubwa ya kutangaza utalii wa nchi yetu. Kama mnavyofahamu, Mheshimiwa Rais amekuwa kinara katika utangazaji wa utalii wa nchi yetu. Vilevile, kupitia taasisi zetu na kampuni za utalii tumekuwa tukishiriki katika maonesho mbalimbali ya Kimataifa na hata Kitaifa, kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano *'Tunalo Site'* ambalo ni tamasha kubwa sana la kuvutia uwekezaji na ushiriki kwenye Sekta ya Utalii hapa nchini. Vilevile, mwezi Machi kampuni zetu zaidi ya 100 zilishiriki maonesho ya Kimataifa kule Berlin katika *ITB Berlin* ambapo jumla ya kampuni 5,800 kutoka duniani zilishiriki maonesho yale. Vilevile, mwezi huo huo Machi takribani kampuni 100 za Kitanzania zilienda kufanya *Roadshow* katika Nchi za Ulaya, katika Majiji ya *Colon*, *Antwerp, Amsterdam*, na *Manchester na London* kule Uingereza. Kwa hiyo, kazi inafanyika na matokeo yanaridhisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali inakwenda kujenga geti la Hifadhi ya Mkomazi katika Wilaya ya Mkinga ili kuboresha mazingira mazuri zaidi ya utalii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuiboresha Hifadhi ya Mkomazi, tulikuwa tuna kazi ya kujenga geti kule Mwanga, tutahamia upande wa Lushoto

na hatimaye tutaelekea Mkinga ambapo Mheshimiwa Mbunge ameuliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Kuboresha Usikivu wa *TBC* – Itigi**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaboresha usikivu wa redio ya *TBC* katika Mji wa Itigi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)*, ipo katika hatua za awali za ujenzi wa kituo cha kurushia matangazo ya redio masafa ya *FM* katika Mji wa Itigi. Eneo ambalo mitambo itajengwa ni katika Kijiji cha Mitundu ambapo hatua za awali za umiliki wa eneo zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, Kituo hiki kinajengwa kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Usikivu wa *TBC* unaosimamiwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)*. Kupitia mradi huu, wilaya 15 zitanufaika kutoka maeneo mbalimbali nchini hasa zile za mipakani, zisizo na usikivu au usikivu wa redio ni hafifu na kwa Mkoa wa Singida, Wilaya ya Iramba pia itanufaika na mradi huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zangu lakini na Bunge hili linaonesha ni karibu swali hili linaweza kuwa ni la nane au la 10. Je, ni lini wanaenda kuanza ujenzi wa mnara huu ili wananchi wa Itigi sasa wasikie redio yao ya Taifa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, hatua ambayo mradi huu upo sasa hivi ni kurasimisha eneo ambalo lilitolewa na Serikali ya Kijiji cha Mitundu bila gharama yoyote na vikao mbalimbali vimekuwa vikiendelea ambavyo vinawashirikisha wajumbe wa Serikali ya Kijiji ili kurasimisha eneo hili. Mradi huu unakwenda kuanzwa kujengwa rasmi mwezi Mei, 2025, yaani mwezi ujao. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Fatma Toufiq.

Na. 53

**Huduma Stahiki kwa Wafungwa Wajawazito**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ K.n.y. MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kutoa huduma stahiki kwa wafungwa wajawazito?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Magereza, inaendelea kutoa huduma stahiki kwa wafungwa na mahabusu

wajawazito walioko magerezani kwa kufuata miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya, kwa wataalam wa Vituo vya Afya vya Magereza. Huduma hizo ni pamoja na kupima afya zao kuthibitisha ujauzito huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubainika ana ujauzito hupelekwa kliniki na kufunguliwa kadi, kupatiwa chanjo, elimu ya lishe na kupima vipimo vyote muhimu vya awali, ikiwemo upimaji wa VVU ambao hufanyika kwa akinamama wajawazito. Wanaobainika kuwa na maambukizi huwekwa katika mpango wa huduma za kuzuia maambukizi ya VVU, kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto *(Prevention from Mother to Child HIV Transmission)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali haioni sababu yakuwa na *cell* maalum kwa ajili ya wanawake wanaonyonyesha na wale wajawazito? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, wale wanawake wafungwa ambao ni wajawazito Serikali ina mpango wowote wa lishe bora ili kusudi waweze kuimarisha afya zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Fatma Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Fatma Toufiq, kwa maswali yake mazuri na kwa kufuatilia haki za akinamama wajawazito wanapokuwa magerezani pamoja na watoto wao. Tunao utaratibu maalum wa kuwahudumia akinamama wajawazito wanapokuwa gerezani na kupitia utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai, kwanza tumelegeza masharti ya wakina mama pamoja na wafungwa

wote wanapokuwa magerezani tumelegeza masharti ya dhamana ili kupunguza msongamano wa wafungwa gerezani wale ambao wanakuwa na sifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa akinamama wajawazito suala la lishe ni suala la lazima na Serikali inaendelea kufanya kila aina ya jitihada kuhakikisha lishe bora wanapata akinamama wajawazito wanapokuwa magerezani. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Malembeka, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninataka kujua ni zipi haki za mtoto anayezaliwa gerezani kwa kosa la mama yake. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, watoto wanaozaliwa magerezani wana haki sawa na watoto wengine ikiwemo kuhakikisha wanapata huduma za afya muhimu kama watoto wengine. Pia, inapofikia miaka miwili Serikali inaweka utaratibu wa ndugu wa mama ambaye yupo gerezani kuweza kuchukua mtoto huyu na kumhudumia nje ya gereza ikiwemo kushirikiana na taasisi ambazo zinatoa huduma kwa watoto, kuchukua watoto hawa na kuwalea katika mazingira mazuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, katika hili eneo la lishe bora kwa ajili ya wafungwa na mahabusu, kwa upande wa wale ambao wafungwa na mahabusu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI sheria imeweka wazi aina gani ya chakula wanatakiwa kupata ikiwemo hadi gramu. Je, Serikali haioni ipo haja ya kufanya hivyo pia kwa akinamama ambao ni wajawazito

ili ieleweke bayana mama mjamzito anatakiwa apate lishe ya aina gani ikiwemo na zile gramu ili kuondoa wengine kupata na wengine kutopata? Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tumechukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tutaufanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 54

**Miradi ya Umwagiliaji kuwa na Tija kwa Wananchi wa Kalenga**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha miradi ya umwagiliaji iliyopo Jimbo la Kalenga inaleta tija kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha miradi ya umwagiliaji iliyopo katika Jimbo la Kalenga inaleta tija kwa wakulima, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeanza kufanya maboresho ya skimu hizo. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imefanya usanifu kwa ajili ya kukarabati skimu hizo na kuanza taratibu za manunuzi.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa taratibu za kumpata Mkandarasi wa Skimu ya umwagiliaji ya Mngalali zimekamilika na mkandarasi atakabidhiwa eneo la mradi tarehe 17 Aprili, 2025. Pamoja na kufanya ukarabati huo, Serikali kupitia Maafisa Ugani wa Halmashauri ya Wilaya itaendelea kutoa elimu kuhusu kanuni bora za kilimo cha umwagiliaji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuuliza maswali mawili ninaomba kwanza niishukuru Serikali kwa kuweza kutoa tozo ambazo zilikuwa zinatozwa kwenye uchimbaji wa mabwawa na kwenye vinyungu ambavyo ilikuwa ni changamoto kubwa kwa wananchi wetu wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza bajeti katika uchimbaji wa mabwawa katika Jimbo hili la Kalenga ili wananchi waweze kunufaika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa tuna wawekezaji wengi katika Jimbo letu ambao wana kilimo cha umwagiliaji wa kisasa; je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi wanapata elimu hiyo na ikaweza kuwasaidia na wao katika ukulima wa kisasa wapate tija? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba, moja; Serikali imekubali kuongeza fedha katika Wizara ya Kilimo na ndiyo maana katika hata bajeti tutakayosoma utaona tumejitahidi kuongeza baadhi ya maeneo kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Kalenga na Tanzania nzima kwa ujumla wanafikiwa na hiki kilimo cha kisasa cha umwagiliaji. Kwa hiyo hilo tuwaondoe shaka wananchi kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amelitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hiyo elimu ndiyo wajibu wetu sisi kama Serikali na tumekuwa tukisisitiza kila wakati ili tuwe na kilimo

bora na chenye tija kwa wananchi wetu. Kwa hiyo tutaongeza kasi ili tuweze kuwafikia zaidi wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Sabu, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Mradi wa umwagiliaji Kasoli - Wilaya ya Bariadi utakamilika na kuanza kufanya kazi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji tunatekeleza Mradi wa Kasoli uliopo Wilaya ya Bariadi ambao ulianza mwaka 2023, Januari na tunatarajia kukamilika kwake itakuwa mwaka huu 2025 mwezi Agosti ndipo utakapokamilika na kuanza kufanya kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mpango wa Serikali ulikuwa ni kuongeza skimu za umwagiliaji saba ndani ya Wilaya ya Ileje. Ninataka kujua utekelezaji wake umefikia wapi mpaka sasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, mpango uliopo ni kwamba tumeshazifanyia *feasibility study* na sasa hivi tupo katika hatua ya kutangaza *tender* ili tupate wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, Kwanza nitoe shukrani zangu kwa ajili ya Skimu ya Ruaha Mbuyuni kwamba Wizara imeikumbuka na ipo kwenye ukarabati naomba tu *speed* iongezeke. Swali langu la nyongeza ni kwamba, ni lini Skimu ya

Mgambalenga ambayo imesimama kwa muda mrefu itaanza tena ujenzi na mkandarasi yule kupewa fedha ili aweze kutekeleza jukumu lake? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba kwenye Skimu ya Mgambalenga ni miongoni mwa skimu ambazo tumeziombea fedha Wizara ya Fedha na imetuahidi kutupatia fedha mwezi huu Aprili na mwezi Mei tutahakikisha kwamba tunawakabidhi wakandarasi fedha walizoomba ili waweze kuendelea. Kwa hiyo ipo miongoni mwa hizo skimu ambazo tumeziombea fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa Wilaya ya Makete, Kata ya Kitulo ndio tuliiorodhesha kama wanastahili kupata mradi wa umwagiliaji. Ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi wa Kitulo kupata mradi wa umwagiliaji kwa sababu kumekuwa na ukimya kwa muda mrefu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Makete chini ya Mbunge wao Mheshimiwa Festo Sanga, tuwathibitishie tu kwamba skimu hiyo ipo katika mpango wa Serikali, watapata huo mradi na itawasaidia wananchi wake. Kwa hiyo, hiyo ndio kauli ya Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Je, mchakato wa ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Makeresho imefikia hatua gani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, Skimu ya Makeresho tulitangaza awali katika mfumo na tukakosa wakandarasi wenye sifa. Sasa hivi tumetangaza upya ili tupate wakandarasi wenye sifa na skimu hiyo itasaidia wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini pamoja na Hai. Kwa hiyo, tupo katika hatua hiyo.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaleta matangazo kwenu kulikuwa na jambo hapa. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu akiweka mezani Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali, kuna gazeti mojawapo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili, nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili. Atakuwa ametoka nje? *Okay,* yupo pale, sawa. Sasa Mheshimiwa *Chief Whip* asikie. Aah! Naona mnasikiliza wote kwa pamoja, haya ahsante.

Hili Tangazo la Serikali Na.146 la tarehe 28 Februari, 2025. Tangazo hili, kuna Mbunge wa Kiteto, lakini pia Mbunge nadhani wa Chemba walishapata kuleta; sio kuleta hoja lakini kuna hoja iliibuliwa humu ndani kuhusu eneo lenye mgogoro. Sasa hili Tangazo linahusu Pori la Akiba la Mkungunero.

Sasa kwa sababu hatuna hakika na haya yaliyotajwa, maelezo ya mpaka wa eneo, haya yamo ama hayamo kwenye lile eneo lenye mgogoro ili hili Tangazo lisije kuwa limewekwa hapa mbele halafu ikatokea kwamba yale maeneo waliyokuwa wameyalalamikia Wabunge hapa ndani na Serikali mkapewa maelekezo kwamba mkakae nao muangalie namna bora ikishindikana jambo lirudi hapa ili Bunge litume Kamati kule isije ikawa ni sehemu.

Kwa sababu maamuzi yalitoka kwenye Bunge lile la Januari, Februari kuwapa Serikali kazi hiyo. Kama hilo jambo limeshafanyika leo mtatupa taarifa na kama halijafanyika bado tangazo hili kuwekwa hapa ndani itakuwa mmelikosea Bunge. *(Makofi)*

Vinginevyo tunaweza kulitoa ili ninyi mkatazame mipaka iliyotajwa, hawa Wabunge walichokuwa wamekieleza kimo ama hilo eneo halipo kabisa ili tuwape nafasi ya hili tangazo kulileta tena ili leo tuwe tumeliondoa kwenye orodha ili mkaliangalie, halafu kama halipo mnalileta sisi tunalipokea hapa tunapeleka kwenye Kamati yetu ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Kwa ngazi hii majibu hayo yapo Mheshimiwa au hayapo tuwape muda mkalitazame. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kweli tangazo limetolewa na tunazo *copy* kama utaratibu ulivyo, ila sina uhakika kama hawa waliotoa hoja wameliona na wamethibitisha hizi *coordinates* na mgawanyo wa hili pori ulivyo.

Sasa sisi limeshachapishwa, tumelileta leo. Kwa hiyo labda tungewapa fursa wao walisome kwanza halafu wakuletee hoja, baadaye uamuzi ufanyike. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, hili Tangazo Na. 146 kwenye hii orodha yetu ya shughuli za leo linatokea namba tano. Kwa hiyo katika haya matoleo yaliyowekwa hapa yapo 10, sasa yatakuwa tisa. Hili namba tano tutaliondoa ili Waheshimiwa Wabunge wale waliokuwa wameleta hoja yao hapa tujue kama hili tangazo linaondoa ule mkanganyiko uliokuwepo au haliondoi?

Kama haliondoi na lipo nje kabisa ya lile eneo walilokuwa wanalalamikia Wabunge basi tangazo hili litawekwa tena kwenye orodha yetu na litakuwa limeshawekwa mbele ya Bunge na tutapeleka kama matangazo mengine tunavyopeleka kwenye Kamati yetu ya Sheria Ndogo. Kama haikuwa hivyo, basi Serikali itatazama namna ya kulifanyia kazi hili kwa sababu hatutataka tangazo lianze kutazamwa kabla hoja ya Waheshimiwa Wabunge haijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa maelezo uliyotoa kwa maana ya kutangaza tangazo ni haki yenu ninyi kutangaza na ni kisheria kabisa isipokuwa sisi lazima tujiridhishe kama hoja za Waheshimiwa Wabunge walizozileta kwa niaba ya wananchi zimefanyiwa kazi au hapana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, matoleo tisa yamepokelewa hapa na kwa utaratibu wetu ule wa kawaida tutaendelea nayo.

Baada ya kusema hayo sasa nilete matangazo kwenu. Tangazo la kwanza Waheshimiwa Wabunge; Mheshimiwa Naibu Waziri keti kidogo, ahsante sana.

Waheshimiwa wabunge, kuna mmoja naye anatembea kule nyuma sijajua yeye, hebu simama ulipo bwana unayetembea huko nyuma.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Tunao wageni tisa wa Bunge na hii ni Kamati ya Bunge ya Uchumi wa Taifa, Biashara na Masuala ya Kazi kutoka Bunge la Zambia. Wapo Mheshimiwa Sibeso Sefulo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati; Mheshimiwa Joel Chibuye, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Davison Mungandu, Mjumbe wa Kamati.  Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Kabwe Chewe, Mjumbe wa Kamati; Mheshimiwa Wesley Kolala, Mjumbe wa Kamati; Mheshimiwa Simon Banda, Mjumbe wa Kamati; Mheshimiwa Walusa Mulaliki, Mjumbe wa Kamati; Mheshimiwa Derick Chilundika, Mjumbe wa Kamati; na Ndugu Moses Chumba, Katibu wa Kamati. Ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, lakini pia nitumie fursa hii kuwapa pole sana wamepoteza Katibu wao wa Bunge, amefariki siku chache zilizopita akiwa kwenye mkutano Uzbekistan. Poleni sana ndugu zetu wa Zambia na tunawatakia Mwenyezi Mungu awajalie

mnapoendelea na shughuli za kumpumzisha huyu ndugu yetu na Mwenyezi Mungu ampe pumziko analostahili.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, hawa ni ndugu zake kutoka Ruvuma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Hindu Lugome ambaye ni Mkurugenzi *Rana Decor.* Karibu sana Ndugu Tawaqul Hassan. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu Mheshimiwa Naibu Spika, ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Jesca David Kishoa, ambao ni wanafunzi wa Shahada ya Uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, ambao ni ndugu zake kutoka Kasulu Mkoa wa Kigoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, ambaye ni mtoto wake Ndugu Keflen Songe kutoka Dodoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, ambaye ni mjukuu wake Ndugu Nabil Ramia. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ambao ni Viongozi wa Mbogwe *Jogging Club* kutoka Mkoani Geita. Karibuni sana. Mheshimiwa Maganga, tunaamini hawa wamekuja mahsusi kwa ajili ya kushiriki Bunge *Marathon* kesho. Karibuni sana wageni kutoka Geita. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, Wageni saba ambao ni wanachama wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi wa Chuo cha Teknolojia Dar Es Salaam *(DIT)* kutoka Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 80 na walimu sita kutoka Shule ya Msingi, Waheshimiwa mnaozungumza nimesimama bado. Sijajua kama mnataka kutajwa majina na Bunge linaelekea mwisho sijui. Miaka mitano mko humu ndani msizungumze nikiwa nimesimama. Mheshimiwa Mwinjuma na Mheshimiwa Hamad Chande, nimesimama.

Wanafunzi 80 na Walimu sita kutoka Shule ya Msingi *Precious* ya Wilaya ya Arumeru Mkoani Arusha wakiongozwa na Mkurugenzi wa Shule ya *Precious* nchini Tanzania, Ndugu Mchungaji Sarah Gwau. *(Makofi)*

Wanafunzi 74 na Walimu 10 wa Shule ya Msingi Shalom ya Jijini Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 83 wa Chuo Kikuu St. Joseph kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao. Ninayo matangazo mawili yote yanatoka kwa Katibu wa Bunge.

Kwanza, Waheshimiwa Wabunge wote mnakumbushwa kwamba kesho siku ya Jumamosi tarehe 12 Aprili, 2025 kutafanyika Bunge *Marathon* kwa awamu ya pili. *Marathon* hii itahusisha mbio za kilomita tano, kilomita 10 na kilomita 21 na washindi watapewa zawadi mbalimbali zikiwemo fedha taslimu.

Waheshimiwa Wabunge, *Marathon* hii kama ambavyo tulikubaliana ni kwa ajili ya kujenga Shule Maalum ya Sekondari ya Bunge ya Wavulana kwa Kidato cha Tano na cha Sita na kauli mbiu ya *Marathon* hii ni "Shiriki Michezo kwa Maendeleo ya Taifa Letu". Mgeni rasmi katika mbio hizi tunamtarajia kuwa

Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, taarifa niliyopewa ni kwamba kwa kesho Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakuwa akikimbia kilomita 21. Kwa hiyo, wale ambao tumejifua tutaungana naye wengine tutakutana kwenye mbio za kilomita tano. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, washiriki wote wanapaswa kuwasili Uwanja wa Jamhuri Saa 11.30 Alfajiri kwa ajili ya kuanza mazoezi ya viungo kabla ya kuanza *Marathon*. Waheshimiwa Wabunge wote mnasisitizwa kwamba kuhudhuria *Marathon* hii ni lazima. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, nalo linahusu kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere inawaalika kwenye Maadhimisho ya Kumbukizi ya Miaka 103 ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere. Maadhimisho haya yatafanyika siku ya Jumapili tarehe 13 Aprili, 2025 kuanzia saa 2.00 asubuhi katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma. Kauli mbiu ni "Chagua Viongozi Bora kwa Ustawi wa Jamii na Maendeleo Endelevu ya Taifa Letu".

Waheshimiwa Wabunge, maadhimisho haya ni mwendelezo wa utekekezaji wa mpango wa miaka 10 wa kuenzi na kusherekea urithi wa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ambao ulizinduliwa Kitaifa mwaka 2022 Butiama Mkoani Mara. Madhumuni makubwa ya maadhimisho haya ni mawili; moja ni kuwashirikisha Watanzania, Wizara na Taasisi. Upande wangu wa kushoto Mheshimiwa Asia na Mheshimiwa Hawa, bado nimesimama.

Madhumuni makubwa ni mawili:-

Moja, kushirikisha Watanzania, Wizara na Taasisi wakiwemo watoto na vijana wa Taifa letu katika kumuenzi Baba wa Taifa kwa kazi nzuri aliyolifanyia Taifa letu la Tanzania;

Pili, kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi uliotukuka kwa kuongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake na huyu si mwingine ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mgeni rasmi katika maadhimisho haya anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa Wabunge wote hii itakuwa ni siku ya Jumapili mnaalikwa kushiriki maadhimisho haya muhimu kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo Mwenyekiti anaingia kwa ajili ya kunipokea. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEORNAD- KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu. Tutaanza na Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo. Tunaanza na Mheshimiwa John Poul Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia bajeti hii ya kipekee. Hii ni bajeti ya mwisho ya mwaka katika bajeti 15 za Dira ya Taifa ya 2025 upekee unaanzia hapo, lakini ni bajeti ya tano ya mwisho katika mpango wa tatu wa miaka mitano, mpango

wenye dhima ya ujenzi wa uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri hii ni bajeti ya mwisho kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020 mpaka 2025. Kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu nitachangia katika kupitia mawanda hayo. Naunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, bajeti ya Mheshimiwa Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa lakini bajeti ya mlezi wa Mkoa wa Kagera. Kwa hiyo, kwa sababu hizo tatu sina jinsi yaani kabisa kwa vigezo naunga mkono bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojenga uchumi shindani na viwanda, hapa tulipofikia taarifa alizotoa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wale wataalam wa riadha tumefikia kwenye mahali panaitwa *spring body,* yaani kama unajua riadha hapa ndiyo pa kuchupa kwenda kwenye hali ya juu unayoitegemea. Wale wengine wasiojua sayansi hii wakiangalia malengo yetu ya *Vision 2025* wanaweza kuhoji kwa nini hiki hakijafanyika? Hapana! Tulikuwa tunajenga *spring body*. Ili ujenge viwanda, ujenge uchumi shindani unapaswa kuwa na miundombinu wezeshi, lakini na miundombinu saidizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumefanikiwa kupata umeme, tunao umeme wa kutosha kwa sasa. Tunao umeme wa kutosha kuweza kuendesha viwanda vyetu na shughuli zetu. Kabla sijasahau, kuanzia viwandani mpaka vijijini unaweza kupata umeme wa uhakika, ndiyo maana sasa maisha ya vijijini yanavutia na ni rahisi na inapendeza kuishi vijijini. *The village life is loveable and livable*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *spring body* ninayotaka kuizungumzia tumefanikiwa kutengeneza miundombinu. Miundombinu ya barabara, miundombinu ya reli, miundombinu ya usafiri wa anga. Kwa kuwa na nyenzo hizo ina maana tunakwenda sasa kuwa na *production* katika upande wowote wa nje ya nchi ambao ni *cost effective.* Ni kwa misingi hiyo, ninaunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza miundombinu ya barabara nichukue fursa hii kuunga mkono au kuishukuru Serikali kwa ujenzi wa madaraja manne makubwa Mkoani Kagera ambayo ni Daraja la Kamishango, Daraja la Kalebe, Daraja la Kietema na Daraja la Kanyabasa. Niishukuru Serikali na nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia, kwa kutoa pesa za kujenga uwanja mpya wa ndege Kagera ambao kimsingi siyo wa Tanzania tu na nchi jirani zitautegemea uwanja huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Uganda ya Kusini ukijenga uwanja wa ndege pale ulipowekwa Kyabajwa ni karibu sana na kwenda sehemu za Mbarara. Kwa hiyo, tutakuwa tunaweza kutengeneza pesa za kigeni za kuhudumia majirani zetu tukiwa pale. Ninaomba tunapokwenda kujenga uwanja huu wa ndege kuna mambo mawili ya kushirikiana. Moja, watu wa *TANROADS* watusaidie kutengeneza Daraja la Kasinda, lakini Wizara ya Kilimo unapotengeneza ule Mradi wa Kimataifa wa Umwagiliaji wa Bonde la Mto Ngono lazima wachoraji wa mfumo ule, ile *design* ya *irrigation scheme* lazima ioanishe Daraja la Kasinda na ile *irrigation scheme* ya kimataifa ambayo itaweza kutengeneza chakula cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau hii ni Wizara ya Kazi, ni Wizara ya Ajira, nichukue fursa hii kufanya ubaguzi niwachague wafanyakazi wachache niwapongeze. Tumefanya mambo mazuri tumefanya vitu vizuri, lakini ni muhimu kuwapongeza wafanyakazi. Niwapongeze wafanyakazi wa Shirika la *TANESCO* Mkoa wa Kagera, kuanzia kwa *RM,* kwenda *DM* na kwenda Mratibu wa *REA* Mkoani Kagera wamefanya kazi nzuri, lakini wanao uwezo mkubwa wa kuitika kuwaeleza watu kitu gani walichofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewachagua hao kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tunapofurahia majengo mazuri, tunapofurahia wanafunzi kufanya vizuri, tunapofurahia matibabu tuwakumbuke wale wafanyakazi, 'unapokula pilau usisahau kasufuria kajikoni kale kanako kaanga, keusi ndani na nje'. Wafanyakazi wa Watanzania wanafanya kazi nzuri, shimeni na Mama atawaona tarehe Mosi mwezi Mei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu viwanda, viwanda nioanishe na suala la ajira na kazi, tunapolenga huu utaratibu wa kutoa mikopo kwa vijana 4:4:2 lakini na watu wengine kutafutiwa mikopo ya bei nafuu. Katika viwanda kuna Mfuko unaitwa *NEDF (National Entrepreneurial Development Fund)*. Huu Mfuko ni tofauti na Mifuko mingine. Huu Mfuko haupewi pesa mpaka ufundishwe na ukihitimu ndiyo unakwenda na kimsingi ukifuatilia mfumo wake unakuwa na *incubator,* ina maana kuna maeneo maalum wananchi wanapelekwa wanafundishwa mtapewa vifaa *shared equipment* mpaka uelewe, ukishaelewa sasa ndiyo una-*graduate* kwenda kujitegemea kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuishauri Serikali na Ofisi ya Waziri Mkuu, kapitieni ile *NEDF* kusudi wale watakaopewa pesa ziwe za benki ziwe za vyanzo vya ndani waweze kwenda ku-*graduate* kwa ile dhamira yetu kwa lengo la Mheshimiwa Rais kwamba watoke kwenye hatua hii waende kwenye hatua kubwa iliyo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipozungumza miundombinu wezeshi upande wa nishati nichukue fursa hii kuomba Wizara ya Nishati kwamba ile miradi ya kupeleka umeme visiwani ambayo mikataba imeshasainiwa, ninaomba chonde chonde watu wa Muleba ndiyo wenye maji mengi ya Ziwa ya Victoria, Wakandarasi wanapokwenda wahakikishe mimi na Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, tunawasindikiza. Sisi tuna bendi yetu ya muziki iwapeleke ikaweke mwanga, ikaweke nishati katika Visiwa vya Goziba, katika Visiwa vya Mazinga, katika Visiwa vya Bumbile, Kyabona, Makibwa kusudi watu waone mwanga tuweze kuokoa ile *post-harvest loss* tunayoipata inayotokana na dagaa wetu kutokuwa na umeme mzuri wa kuweza kukausha mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, namwona Mheshimiwa Waziri wa Afya, aje aniletee salamu za mjomba nilimwona amepiga picha na mjomba, lakini kazi aliyonayo visiwa vya kwetu waliomba *speed boat (ambulance speed boat)* iweze

kuwasaidia wananchi wanaoishi kwenye *square kilometer* 7,000 kusudi waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga zahanati tunashukuru, wanaona *ambulance* za nchi kavu wanatamani *ambulance* ya kwenye maji, mahusiano yangu mimi na yeye wanayajua, kazi niliyomfanyia kwao watu wakagalagala na yeye alipize aje anifanyie kwetu, atuletee *ambulance* inayokwenda kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la uchukuzi, Wizara ya Uchukuzi tunawashukuru sana. Mwenzio anapopewa wewe shukuru akishapewa yeye umebaki wewe, tunashukuru kwa meli kubwa ya MV Mwanza inakuja, tunashukuru kwa Bandari za Kemondo na Bukoba. Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, jana aliomba Kyamukwikwi, akaomba Magarini, nami ninaomba juu ya hiyo watuletee meli itakayoweza kuhudumu kwenye visiwa vile na kwenye bandari ile. Nimwombe Mwenyezi Mungu kila aliyeweka mkono wake katika kuiangusha ile Meli yangu ya Clarias, Mwenyezi Mungu amjibu duniani asimjibu mbinguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli yangu ya Clarias ilishamaliza *survey* kwamba ianze huduma wakaja watu wenye nia mbaya, samahani katika kwaresima lakini naomba Mwenyezi Mungu awajibu sasa tunahitaji Serikali watupatie meli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kivuko cha kuunganisha Tanzania na Uganda ninaomba kivuko cha kutoka Rubafu kwenda Uganda ujombani kurudi haraka ili kusudi tuunganishe Afrika Mashariki iliyo kubwa. Wizara hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Idara zake zote karatasi yenu waliyoileta imeakisi picha kubwa ya mambo tuliyofanya. Kimsingi kwetu Kagera kwenu Kagera, Mwenyekiti ni mtu wa Kagera huyu, nataka niwaeleze mwelewe mambo yote wanayozungumza sisi tuna uhakika wa kura. Kura zetu ni 1,560,000 *plus*, ni kura za kuheshimisha, lakini nisikudanganye ni kura za shukrani na anayeshukuru anaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa John Poul Mwijage. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mwenzetu Mheshimiwa Kiswaga, ametuambia kwamba neno la busara la leo ni hili, *always say less than necessary, I hope* nitaweza ku-*live within that wisdom.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kusema kwamba ukitaka kumfahamu kiongozi mzuri uangalie namna ambavyo anajali safu anayoichagua kwenda nayo. Ninaamini kwamba wote tutampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumchagua Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambao wanatekeleza yale ambayo kila Mtanzania anafurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hiyo tu, kama tunavyofahamu safu ya Mheshimiwa Rais ni pamoja na Mawaziri wote na wale watendaji kwenye taasisi na Wizara kwa hiyo, tunampongeza sana. Ninaamini kwamba, amechagua viongozi wazuri, wanatuletea matokeo; tumeyaona na tumeyasikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mambo makubwa yametekelezwa ndani ya kipindi cha miaka hii minne na ni mambo ambayo naamini wenzetu, majirani zetu, wanapoona wanaona wivu sana kwamba, hii nchi inapiga hatua kwa kasi kubwa. Sio tu kasi kubwa, kasi ambayo inajali maendeleo endelevu, kasi ambayo inakuwa kubwa, lakini pia, tunaangalia kwamba, lazima tulinde mazingira yetu, tunajali nishati safi, ili kulinda mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea pia kujali vijana wetu watakapopata ajira na zaidi ya yote demokrasia. Ninaamini demokrasia imeendelea kushamiri na zile *4Rs* za Mheshimiwa Rais zinaonesha matokeo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Taifa letu, tumepewa picha nzuri ambayo ni mahali pazuri pa kuanzia. Tunavyoenda kuomba kura tumepewa picha ya jumla, lakini

niseme kwamba, kule kwetu Vunjo mambo yamekaa sawa; maji tumepata, umeme tumepata, vituo vya afya tumepata na zahanati tumepata. Tumepata shule, ingawa bado kuna shule za kukarabati na tumekuwa tunasisitiza hapa shule za msingi kwenye Jimbo la Vunjo ni kongwe na zinahitaji ukarabati, lakini tunashukuru tumepata shule mpya za kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru pia barabara zimeboreshwa kwa kiasi kikubwa, isipokuwa niseme kwamba, baada ya hizi mvua zilizonyesha, unajua barabara zile zilitengenezwa zaidi na kokoto na hata sio zote, zimepata uharibifu mkubwa ambao tunaamini Serikali itaenda kuuboresha kwa haraka, lakini kuna viporo vya barabara. Kwa mfano, ile barabara ninayoizungumzia kila wakati ya Pufu – Mandaka – Kilema, ile Barabara ya Uchira – Kisomaki – Kolarie na Barabara ya Chekereni – Kahe – Mabogini, ni barabara za kimkakati kwa upande wa Mkoa na kwa Jimbo, bado zinangojea kupewa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza na wahusika wakaniambia kwamba, sasa tukifanya kila kitu bila kuacha kiporo watakuchagua tena, kweli? Si utakuwa umemaliza kila jambo? Kwa hiyo, wameniambia kwamba, chukua hivi viporo, vitamaliziwa, ili na wewe upate kura. Sasa wasiponipa kura ina maana kwamba, hivi viporo vitaendelea kubebwa na watu ambao, pengine hawataweza kuvifikisha mahali ambapo tumevifikisha mpaka sasa hivi kwa sababu, bado kazi zinaendelea kwenye hizi barabara chache ninazotamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Vunjo ninaamini tutampa kura zote Mheshimiwa Rais wetu, timu yake na mwenza wake, Mheshimiwa Nchimbi na ninawahikikishia kwamba kwa 100% atapata hizo kura. Sasa nikirudi, lakini kabla sijarudi kwenye mada hasa, niseme hivi; kwa hili lililosemwa la kwamba, kuna kazi ambazo tumebakiza za kumalizia nataka niwaonye wale vijana wanaojipitishapitisha kule sasa hivi, wasije wakaingia kwenye lile daftari la CCM la hukumu, halafu wakashindwa kugombea. Watulizane, mambo yanaenda vizuri na ninaamini watajua kile ambacho tumefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye mada na nitazungumza mambo mawili tu. Nitazungumzia *issue* ya umuhimu wa kudhibiti uhamiaji holela unaokuja kwa kivuli au mwamvuli wa uwekezaji kutoka nchi mbalimbali; hapa mtu anaingia, anasema anakuja kuwekeza, kumbe anakuja kuchukua ajira na shughuli zile ambazo zingefanywa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili, nitazungumzia kuhusu mifuko ya uwezeshaji. Ipo mifuko na mipango 74 kwenye Wizara hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mifuko hiyo ni mingi sana, lakini nitaizungumzia kidogo na nitoe ushauri wangu ambao nafikiri unaweza ukasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme hivi, siku za karibuni tumeona kuna raia kutoka nchi tunazozifahamu ambao wameingia mjini na kuanza kufanya shughuli za uzalishaji na biashara ambazo kwa *scale* yake, kwa uhitaji wa mitaji yake, kusema kweli, sio shughuli za kufanywa na wageni ni za kufanywa na Watanzania na hakuna sababu ya kwamba, biashara ya mke wangu mimi ikauawe na mtu ambaye ametoka nje. Tumewekeza kwa nia ya kwamba, Watanzania wazawa na wale ambao ni wazalendo waweze kuingia kwenye biashara watengeneze fedha na fedha hiyo ibaki hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli hizi za uchuuzi ambazo zinafanywa na watu wa nje na wanakuja kwa kasi kubwa, ambao bahati mbaya au nzuri wao wanajiunga na mnyororo wa uzalishaji kwenye nchi zao, wanajua bei zile zilivyo kwa hiyo, wanazileta zile. Ninaamini kwamba, kuna ukiukwaji wa kutokulipa kodi kwingi kwenye hizi bidhaa ambazo zinazoingia na zinaenda kwenye mnyororo ule ule wa wale watu wenyewe kwa hiyo, inakuwa ni vigumu sana hata kwa *TRA* kuweza kudhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hivi, zile mamlaka ambazo zinahusika, *TIC,* Wizara ya Mambo ya Ndani na Uhamiaji, watafute namna ya kuweza kudhibiti masuala haya kwa sababu, mpaka kule kwenye vijiji watu wanafanya kamari. Mtu kutoka nje anakuja kufanya kamari! *It is not acceptable* kusema kweli na mimi naona watu watumie uzalendo tu, hata kama ni sheria, lakini

kama uzalendo ukizingatiwa ninaamini suala la hawa watu wanaofanya biashara na shughuli ambazo zitafanywa na watu wetu litaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye suala zima la hii mifuko na program za kuwezesha ambazo ziko chini ya *NEEC,* ile *National Economic Empowerment Council.* Ninafikiri hivi, kwanza kuna kutokuelewana, sintomfahamu nyingi, hii mifuko haifahamiki; kitu tunachozungumza hapa kila wakati tukikutana, haya mambo ya uwezeshaji tunazungumzia ya Halmashauri, ile ya kumi ambayo inatoka 4:4:2, nyingine yote hatujawahi kuizungumza kwa sababu, watu hawaifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu anayeuza hii Mifuko, wa kusema ukienda mfuko huu utapata hiki, ukienda *SIDO* utapata hiki; hakuna kwa sababu, imekaa mahali ambapo sio sehemu yake, naamini. Ninaamini kwamba, ni lazima tuunde mamlaka itakayosimamia suala zima la uwezeshaji, ili waweze kupata jukumu ambalo kuna sera na sheria ambayo inaongoza. *Of course,* sera zipo kwenye masuala yote haya, lakini ni vizuri ikajulikana wazi na ikawa *transparent* kwamba, ipo mifuko hii ambayo inaweza ikasaidia katika kuwezesha wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru Mheshimiwa Mwijage alipokuwa anazungumza ametaja hii ya *NEDF (National Economic Development Fund)* ambapo mimi ninajua kwamba, Mifuko hii sasa imechanganyika, hakuna vipeperushi na ukweli ni mtu aliye kule kijijini hawezi kabisa ku-*access* hii Mifuko kama tunavyoifahamu. Kwa sababu hiyo, ninaamini hata kama ingeundwa ikawekwa kwenye chombo ambacho kitashughulika na mikopo pamoja na udhamini wa mikopo kutoka kwenye benki, itakuwa imeongeza sana wigo na uwezo wa fedha hizi ambazo zimelala huko na hazitumiki kama ipaswavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana naomba tathmini ifanyike ijulikane kila Mfuko umemkopesha nani na watu watashangaa wakiona matokeo yake, halafu tuunde mfumo ambao utamwezesha kijana hata akiwa *university*, akimaliza pale anaweza akaingia kwenye mfumo akaomba mkopo mwenyewe,

sio lazima aende kwenye vikundi, vikundi vinaharibu mikopo. Kwa hiyo, ninaomba kuwe na mfumo ambao ni kama *M-pawa* tu, mtu anaomba, data zake zipo kwenye *system*, kwenye *NIDA* zipo na simu yake ipo, anaomba, akikidhi vigezo vya mkopo ule anaambiwa nenda mahali fulani kachukue. Ninaamini hicho kitafanyika kama tutaunda shirika au chombo ambacho kitasimamia mifuko hii na hizi *program* za kuwezesha, ambazo ninaishukuru Serikali kwamba imeziweka, lakini zikae mahali pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme ninashukuru. Ninataka kumpongeza tena Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi ambayo amefanya na ninaamini kwamba, huku twendako ni kuzuri zaidi na ndiyo sababu, ninaamini kwamba, Watanzania wote watatuunga mkono Wana-CCM kwa kumpa kura zote ufikapo Mwezi *October*. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei. Nilimtaja Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo, Ijumaa, kusimama mahali hapa kuongea masuala yetu ya watu wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya nchini. Tunaona anazunguka kila eneo, kila sehemu, kwenda kuhakikisha mambo yanakwenda sawa. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali sikivu, chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Watu waliongea mambo mengi kuhusu uchaguzi na

mpaka leo wanaongea kuhusu *reform* za uchaguzi; *reforms* zipo na zinaendelea kufanywa. Hivi tunavyoongea kila wakati wasimamizi wa uchaguzi ni Wakurugenzi wa Halmashauri, lakini Serikali hii sikivu sasa hivi imetangaza nafasi za wasimamizi wa uchaguzi nchi nzima; watapimwa, watachujwa, wale watakaoonekana wanatosha ndiyo watakaosimamia uchaguzi na siyo wakurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali hii ni sikivu, inasikia, ina *reform* za uchaguzi na tunakwenda kufanya uchaguzi Mwaka 2025 kwa sababu, tuna *reform* zote na tunafanya vizuri. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kujali demokrasia, kwa kuisimamia na kwa kuifanya kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kuhusu kilimo. Sisi watu wa Tabora ni wakulima wakubwa wa zao la tumbaku. Hapa niipongeze sana Serikali, kupitia Wizara ya Kilimo, kwa kazi kubwa waliyoifanya. Tunaishukuru sana Serikali wakulima wetu wa tumbaku, mwaka jana nilisimama hapa kudai ruzuku ya mbolea, sasahivi wana ruzuku ya mbolea, tuna wanunuzi wa kutosha na pembejeo zimefika kwa wakati. Tunaishukuru sana Wizara ya Kilimo kwa kazi hii kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi sasa hivi wanatujengea mabani ya kisasa; mabani ya zamani yalikuwa yanadondoka, yanaharibika, lakini Serikali ipo kazini kujenga mabani ya kisasa. Hili jambo ni kubwa sana, tunaipongeza Serikali na tunasema sisi watu wa Tabora tunasubiri muda ufike tumpe kura nyingi za heshima Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mema changamoto hazikosi. Sisi watu wa Tabora ni wakulima wakubwa wa tumbaku, tunalima tumbaku kwa karibu 70% ya nchi hii, lakini hatuna kiwanda ndani ya mkoa wetu wa Tabora. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kaka yangu Mheshimiwa Bashe, anatoka Tabora, haya ni malalamiko makubwa sana. Tunajua anakutana na watu mbalimbali na anaongea na wawekezaji mbalimbali, tunaomba atuhakikishie tunapata Kiwanda cha Tumbaku Tabora, vijana wetu wapate ajira, mama zetu wapate

ajira, kwa sababu, tumbaku tunalima sisi na pia, tutaongeza bei ya tumbaku. Angalau umepambana sasa tumbaku ni dola tatu na kuendelea, lakini tukichakata Tabora bei itapanda kwa sababu, hatutaisafirisha kwa gharama kuipeleka Morogoro. Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri ajitahidi tupate kiwanda cha kuchakata tumbaku katika Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tabora tulikuwa na Kiwanda cha Nyuzi, kinatokana na pamba, kiwanda hiki kimekufa. Bado tunajua Mheshimiwa Waziri alikuja Tabora akakitembelea, sijui mikataba imefanya nini, lakini ninajua Serikali hawashindwi. Tunaomba Kiwanda hicho cha Nyuzi kifufuliwe, ili watoto wa Tabora, wananchi wa Tabora waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora hakuna kiwanda, inasababisha watu wengi wanakuwa *jobless* na hatimaye tunaambiwa Tabora hakuna maendeleo, lakini hatuna viwanda vya kutosha. Tunaomba sana, tunalima pamba katika Wilaya yetu ya Igunga, Wilaya ya Nzega kidogo tunalima pamba, sasa hivi tumeanza kulima pamba kwenye Wilaya ya Kaliuwa, tunaomba tupate kiwanda chetu cha nyuzi ili tupate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kuhusu mabwawa kwenye Wizara hiyo ya Kilimo. Tunaishukuru Wizara ya Kilimo kwa kutujengea bwawa katika Kata ya Tumbi, lakini kuna upembuzi yakinifu Magoweko. Tumepeleka maombi yetu, kwa ajili ya kupata mabwawa Itetemia, Isukamaela, Nyakato Kata ya Mesha, Manoleo Kata ya Itondanda na Kalumwa Kata ya Uyui. Tunaiomba sana Serikali ituwekee mabwawa ili tuweze kulima kwa tija, tuweze kulima muda wote na hatimaye ndoto ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu ya Watanzania kulisha Afrika basi, iende ikatimie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee tena kidogo kuhusu elimu. Kule Tabora kuna shule nyingi kongwe, ule ni mji wa zamani, shule nyingi ni kongwe. Tunaomba Serikali itupe pesa za ukarabati; kuna shule ya Mwenge, hii shule ni maarufu sana, lakini imekuwa kongwe kabisa. Kuna shule ambazo wamesoma viongozi karibia wote wa nchi hii, mpaka Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere

amesoma Tabora *Boys*, shule hii bado ina mambo ya ukarabati haijakamilika. Tuliomba pesa, tukapata shilingi milioni 900, kwa ajili ya *boys* na *girls*, lakini mpaka sasa shule hizi bado hazijamilisha pesa, kwa ajili ya ukarabati. *Town school*, tuliomba pesa ya ukarabati tukapata, lakini bado hatujajenga uzio na pia, shule ya Uhusu. Tunaiomba sana Serikali itupatie fedha za ukarabati wa shule hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya, Tabora Manispaa kuna kata 29, lakini pamoja na *population* kubwa sana ya watu wa Tabora unaweza ukashangaa kuna vituo vinne tu vya afya ndani ya kata 29, hiki kitu hakikubaliki kabisa. Tuna kata ya Uyui ambayo sasa tunaenda kujenga *Station* ya *SGR* ambayo itakuwa katikati ya Uyui na Ifucha. Ninaiomba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu watujengee kituo cha afya kwenye Kata ya Uyui, ni kata kubwa ambayo ipo jirani na kata za pale jirani na ina wananchi wengi; kituo hicho cha afya kitatusaidia sana pale kwenye Kata ya Uyui ambayo inaenda kujengwa *Station* kubwa ya *SGR* na pia, kutakuwa na bandari kavu pale na mwekezaji ameshaonekana kwa hiyo, tunaomba tupate kituo cha afya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, kule maeneo ya mjini katikati, uswahilini kule kwetu, nilipozaliwa mimi, hakuna kituo cha afya. Kuna Kata ya Chemchem, Mwinyi, Gongoni, Tambukareli, Mbugani, na kadhalika ambazo zote hizo karibu kata nane ambazo zina *population* kubwa hazina vituo vya afya. Ile Kata ya Chemchem ndiyo niliyozaliwa mimi, ina watu wengi sana, lakini pia, alipotoka Mheshimiwa Hawa na yeye pia, kwao Gongoni pale, kote hatuna kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali, nilikuja hapa nikatoa maoni, basi ile *town clinic* ambayo ni zahanati ya miaka yote, ipo mjini, watuongezee ghorofa, ili iweze kupata hadhi ya kituo cha afya. Leo hii ni zahanati inayozalisha kwa mwezi watoto 200 kwa hiyo, mnaweza mkaona tuna uhaba upi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Usule eneo ni kubwa sana. Tungeweza kupata kituo cha afya, lakini kwenye kata hizi ambazo nimezitaja pia, ni lazima tupate kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuhusu bodaboda; imekuwa ni ajira ya vijana wetu, wanafanya kazi, wanajipatia riziki, lakini vijana hawa wengi wanakuwa wameajiriwa na kuambiwa wapeleke fedha kwa waajiri wao na wao kubaki na fedha kidogo sana ambayo haikidhi mahitaji yao. Mimi binafsi nilijitolea kwenda benki kuwasaidia vijana hawa wapate mkopo, angalao halmashauri zinajitahidi sana, lakini vijana hawa ni wengi, pesa peke yake ya halmashauri haiwezekani. Benki nikakutana na jibu wanasema wanataka hati ya nyumba ndiyo wampe mtu pikipiki. Hii inakubalika kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, aingilie kati suala hili, vijana hawa wakopeshwe bodaboda. Waache kadi za bodaboda kwenye benki kama dhamana, wapewe bodaboda warejeshe hizo fedha kila siku. Unaambiwa tunataka tuone mzunguko wake wa akaunti, jamani, dereva wa bodaboda anapata wapi mzunguko wa akaunti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tupo *serious* kabisa tunataka kusaidia hawa vijana wetu waweze kujiajiri wao wenyewe tuhakikishe tunawasaidia kweli kweli, wakopeshwe, benki ibaki na dhamana ya kadi. Kama mtu mkubwa kama mimi au mtu mzima mfanyabiashara anakopeshwa Scania, anaacha dhamana ya kadi ya gari benki, unashindwaje kumkopesha bodaboda akaacha kadi yake ya bodaboda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku ni kuwabagua na ninaomba Serikali, kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakae waliangalie hili suala bodaboda wakopeshwe pikipiki na waache kadi zao benki kama dhamana na pia, unaweza ukaongezea ukamwambia leta mdhamini mmoja au wawili kama litatokea tatizo lolote, lakini sio kumwambia alete hati ya nyumba. Hao ni vijana wadogo, wamepata wapi hizo hati za nyumba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana, naiomba Serikali yangu sikivu ya Chama Cha Mapinduzi tuliangalie suala hili la bodaboda kupitia kwenye mabenki yetu kwa sababu, halmashauri peke yake hazitaweza kukidhi. Vijana hawa ni wengi na hizi ni ajira zao, zinawasaidia wao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana n ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii muhimu sana ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo amefanya kazi nzuri sana ya kuratibu kazi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya kazi nzuri na hotuba yake imetupa muhtasari mzuri wa mambo yaliyofanyika na kutufungulia jinsi ambavyo tutakwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu; hivi karibuni amefanya ziara kwenye jimbo langu, amezindua miradi kadhaa na kuweka mwongozo katika mambo mengine vizuri sana. Nimpe tu taarifa pia kwamba, hivi tunavyozungumza maagizo aliyoyaacha kwa upande wa Wizara ya Afya wataalam wameshakwenda na tayari wameanza utekelezaji; nimepigiwa simu na wahusika kule. Leo hii tunavyozungumza, Mheshimiwa Jerry Silaa yuko jimboni kwangu kwa ajili ya kushughulikia suala la mawasiliano kama alivyoagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, ninamshukuru na pia ninawashukuru wataalam na Waheshimiwa Mawaziri wengine ambao wameendelea kutekeleza maagizo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM iliaminiwa na kuchaguliwa kwa mujibu wa Ilani ambayo tuliiuza mwaka 2020. Anayesimamia na kuratibu utelekezaji wa Ilani hiyo ni Mheshimiwa Waziri Mkuu; na tumeiona taarifa yake ya jinsi ambavyo ofisi yake imeratibu utekelezaji wa ilani kwa viwango vya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kiongozi mkuu wa utekelezaji huu ni Mheshimiwa Rais; Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa anaratibu tu. Kwa hiyo, kwa kweli pongezi nyingi sana zimwendee Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ametuongoza vizuri tukaweza kutekeleza ilani kwa viwango vikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunapoelekea kwenye uchaguzi huu, mengi yatakayoletwa ni kelele, mbwembwe nyingi, vitisho na namna za kutaka kuvuruga uchaguzi kwa sababu hakuna lingine la kusema kwa kuwa yale tuliyowaahidi wananchi yametekelezwa. Nilipata kusema kwamba, upembuzi wa wataalam juu ya vyama vilivyoleta uhuru katika nchi zao ulisema kwamba, Chama Cha Mapinduzi kinaendelea kuwa madarakani kwa sababu ya utekelezaji wa yale ambayo kimekuwa kikiwaahidi wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukichukua tu Jimbo langu la Mwanga kama *sample,* kwenye Sekta ya Afya tumepata hospitali mpya ya wilaya, imeshajengwa na inafanya kazi, vituo vya afya vipya vitatu na kuna kingine kinakuja katika vilivyoahidiwa ambavyo tumeelezwa kuanzia wiki ijayo. Hicho kitakuwa ni cha nne katika vipya ukiacha vile vya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye suala la elimu upande wa sekondari kila kata ina shule na tuna shule mpya tatu na bado kuna nyingine inakuja. Nichukue fursa hii kuwaambia kabisa wananchi wa Mwanga kwamba iko shule mpya ya sekondari inakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya kidato cha tano. Tulikuwa na shule zenye kidato cha tano na zile ambazo hazina. Ndani ya muda huu wa Serikali ya Awamu ya Sita

tumepata miundombinu ya kidato cha tano katika shule tano zingine. Kwa hiyo, tunaendelea kupata jinsi ya kuwatoa vijana wetu wanaomaliza kidato cha nne kwenda kwenye elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata Chuo cha *VETA* na tumeweza kupandisha hadhi chuo cha ustawi wa jamii kuwa chuo kikuu. Sasa hivi tunaenda kudahili wanafunzi wa mwaka wa tatu. Hayo yote ni kwenye eneo moja tu linaloitwa Mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa Sekta ya Maji, kipekee sana tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa ajili ya juhudi za kipekee ambazo aliweka kumalizia Mradi wa Maji mkubwa sana wa Same – Mwanga – Korogwe; mradi wa takribani bilioni 400 kwa awamu ya kwanza ambao umekamilika kazi ya usambazaji inaendelea vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko pia miradi mbalimbali ya *RUWASA* ambayo inaendelea kuwapatia maji wananchi ambayo iko kwenye hatua mbalimbali; ina changamoto ndogondogo lakini zote hizo tumeshawasiliana na wahusika zinatatuliwa na maji yataendelea kutoka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa Sekta ya Barabara. Hali kadharika, tumejenga barabara ya kipekee kabisa inaitwa *CD Msuya Bypass* ambayo ilikuwa na madaraja 21, lakini tumeshajenga madaraja 18 na sasa wanaendelea na awamu ya kwanza ya kuweka lami. Huu ni utekelezaji ambao ni wa kipekee sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme moja tu hapa linaloangukia Wizara ya Ujenzi. Barabara ya Mwanga – Kikweni – Vuchama, kile kipande cha mwisho cha kilometa kama saba mkandarasi yuko *site* lakini amesimama. Ninaomba Wizara ya Ujenzi walitazame hili ili kile kipande kimaliziwe ili ile kazi iweze kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa Sekta ya Utalii, miaka yote tumekuwa na Hifadhi ya Mkomazi lakini tulikuwa tunaitazama kama vile haiko kwetu. Kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyoeleza hapa, mwezi uliopita Mheshimiwa Waziri Mkuu

alikuja akatuzindulia geti langu jipya na la kisasa kabisa. Kwa hiyo, sasa Mwanga tutaendelea kunufaika na utalii na matunda ya *Royal Tour* yataendelea kufurika katika Wilaya yetu ya Mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu ya huduma za jamii lakini pia upande wa uchumi kilimo, mkandarasi ameingia site kwenye Skimu ya Umwagiliaji ya Kigonigoni inayogharimu shilingi bilioni 16.873. Skimu ya Kivulini imepata tena shilingi bilioni nne kwa ajili ya kuendelea kuimalizia ili ifanye kazi kwa 100% na Skimu ya Kambi ya Swala inaendelea vizuri kwenye uboreshaji wa mifereji pamoja na barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mawili yaliyobakia ambayo yako kwenye hatua za utekelezaji, lakini bado hayajafikia hatua kubwa sana ni suala la stendi ya kisasa ambalo ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais alipokuja juzi amelitolea maelekezo na ninaamini linaenda sasa kwenye utekelezaji, kwa sababu kazi za awali zote zilishaanza, bajeti imetengwa na uwanja umeshaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la magugumaji katika Ziwa Jipe ambalo ni moja ya vyanzo vikubwa sana vya Mradi huu wa Maji wa Same – Mwango – Korogwe uliozinduliwa na Mheshimiwa Rais. Ninafahamu kwamba bajeti ya kuanzia ilikwishatengwa. Kwa hiyo, basi Wizara husika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira wahimize basi kupeleka fedha ili ile kazi iweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yote yametupa mwitikio mkubwa sana wa sekta binafsi katika Jimbo la Mwanga. Ninazungumzia Mwanga kama *sample* kwa sababu ninajua hata katika majimbo mengine ni hivyo hivyo. Sekta binafsi imefanywa mwitikio mkubwa sana.  Ndiyo maana Profesa wa kwanza wa *Oncology,* Profesa Twalib Ngoma aliyekuwa Mkurugenzi wa kwanza wa *Ocean Road Cancer Institute* amefungua hospitali kibingwa pale Mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa ninawambia watu kwamba, Mwanga itafurika watu kutoka ndani na nje ya nchi kwa sababu kama watu walienda kunywa Kikombe cha Babu itakuwa hapa sasa ambapo pamefunguliwa hospitali ya kibingwa. Kwa hiyo, huo ni mwitikio wa kipekee kabisa wa sekta binafsi ambao huwa haupo kama Serikali haifanyi vizuri. Serikali ikifanya vizuri ikajenga *confidence* na imani, basi sekta binafsi huwa inafurika na ndiyo maana tumepata haspitali hiyo kubwa na hoteli kubwa kubwa katika Jimbo la Mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la utawala bora ambalo mara nyingi watu wanaliangalia kwa wembamba sana. Utawala bora ni mfumo unaohakikisha kwamba taasisi zote za umma zinaendesha shughuli zake kwa namna ambayo ni jumuishi na namna ya uwazi zikizingatia utawala wa sheria na haki za binadamu. Sasa kazi ya Serikali katika hili ni kuweka mifumo ya kuwezesha hayo kutendeka na siyo kushika fimbo kuchapa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tangu tupate uhuru nchi yetu imekuwa ikijenga mifumo ya utawala bora kwa kasi kubwa sana na imeendelea kufanya hivyo tangu uhuru. Katika hili ni lazima tulishukuru Bunge kwamba limekuwa likitunga sheria za kuwezesha hiyo mifumo. Pia, Mahakama zetu zimekuwa zikirekebisha sheria kwa kutoa maamuzi kwenye zile sheria ambazo zinakiuka Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda wengine hawafamu kwamba juzi juzi tu hapa ilikuwa ukitaka kuishtaki Serikali Mahakamani lazima umwombe ruhusa Mheshimiwa Waziri wa Sheria, lakini Mahakama ilipangua hilo ikafuta. Sasa hivi una uwezo wa kutoa *notice* ya siku 90 na ukashtaki ukapata haki zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi watu wanaangalia kuishtaki Serikali kwenye zile kesi za kiharakati harakati, lakini ziko nyingi za watu waliofutiwa hati zao za ardhi na watu walionyimwa haki mbalimbali, wanashtaki na wanashinda Mahakamani, wanapata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilichokuwa kinakosekana ni ule uthubutu tu na utashi wa baadhi ya watendaji wetu kutoa haki hizo ambazo pengine zinaonekana ni dhidi ya Serikali au namna gani. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita ametufungulia hilo kupitia *4R*. Ametuonesha utashi wake kwamba, anachotaka ni haki kwa sababu ni kiongozi anayejiamini na anayeamini katika haki. Kwa hiyo, kwa kuzingatia zile 4R sasa watendaji wote wanapewa nguvu sasa ya kuweza kutenda haki kwa sababu ndio utashi wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuko kwenye harakati za hili suala la *Dr.* Samia Suluhu Hassan *Legal Aid Campaign*. Hii sasa ndiyo ishara ya dhati kwamba Mheshimiwa Rais anajiamini yeye na pia anataka haki. Kiongozi ambaye hajiamini hawezi kuhimiza watu wajue haki zao na kuzikimbilia. Kwa sababu watu wanapojua haki zao inakupunguzia nguvu wewe kiongozi kutaka kuwaburuza maana yake ndiyo viongozi wengi wanavyopenda. Viongozi wengi katika historia wamefeli kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala zima la *4R,* suala la Tume ya Haki Jinai na suala la *Legal Aid* limeonesha wazi kabisa kwamba Serikali yetu inakwenda vizuri katika eneo hili. Dunia imeona na sisi tumeona na ndiyo maana Mheshimiwa Rais amepata tuzo nyingi za kimataifa ambazo bila kujipambanua katika maeneo hayo hizo huwezi kupata hata ungefanya mambo mangapi hapa kwenye dunia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengine ambayo ni vyema tukayataja. Ninasema, kwa lugha yetu ya Kipare ni mambo ambayo ni *iconic*. Kwa mfano, suala la vita dhidi ya madawa ya kulevya limefanyika vizuri sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele imelia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limefanyika vizuri sana lazima tuwapongeze. Pia, suala la kuruhusu waangalizi *(observers)* kwenye kuandaa daftari au uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura, hili halijafanyika kwenye nchi nyingi. Kwa hiyo, hili ni la kipekee kabisa. Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imeruhusu waangalizi wa kimataifa waje kuangalia wakati wa uboreshaji wa daftari la kudumu la mpiga kura. Hili ni jambo kubwa sana ambalo ni vizuri dunia ikajua kwamba linafanyika; ila sasa ni lazima tutofautishe *role* ya *observers* na *monitors. Observers* wanafanya kazi yao vizuri na hakuna mahali ambapo wamefungiwa au wamefichwa wasione hayo yanayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia zote. Kazi iendeee. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo. Nilimtaja Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa; Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba na Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo wajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika bajeti hii ya tano na ya mwisho tunayokwenda kuidhinisha Bunge hili la 12 ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninaomba pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba yake iliyotumia masaa mawili aliyoiwasilisha kwa ufasaha kabisa. Ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili; Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Lukuvu na Naibu Mawaziri wote wawili wa Wizara hii dada yangu na kaka yangu pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi pia kuishukuru sana sana Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waheshimiwa Mawaziri wote. Kusema ukweli wamenipa ushirikiano mkubwa wa kutekeleza majukumu yangu ya uwakilishi wa wananchi katika Bunge hili la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashuku sana pia Waheshimiwa Wabunge wote ndani ya Bunge, wamenipa ushirikiano mkubwa sana. Vilevile, Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ninayoiongoza, wamenipa ushirikiano mkubwa katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninawashukuru sana pia Madiwani wa Wilaya ya Namtumbo kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuibua miradi, kuisimamia na kunipa ushirikiano wakati wote wa kazi ya uwakilishi wa wananchi wa Namtumbo. Wamefanya kazi kubwa sana. Safari haikuwa nyepesi, lakini Madiwani wa Namtumbo wamesimamia kikamilifu miradi yote iliyoletwa na Serikali na tumepata mafanikio makubwa. Hongereni sana Waheshimiwa Madiwani wa Namtumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi, Sura ya tatu, ukurasa wa 124, kipengele cha huduma za jamii, Ibara ya 7 ilieleza sera ya msingi ya CCM kuhusu huduma za jamii ni "kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na fursa ya kupata huduma bora za jamii na za kutosha bila vikwazo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi Namtumbo Ilani imetafsiriwa kwa vitendo ndiyo maana nimeanza kuishukuru sana Serikali. Katika elimu Serikali ilitupatia zaidi ya shilingi 12,526,000,000 katika kipindi hiki ili kutekeleza miradi ya elimu. Tumejenga shule mpya tano za sekondari na nne wanafunzi wako madarasani hapa tunavyozungumza. Pia, tunaendelea na ujenzi wa shule moja ya sekondari, Hanga Sekondari. Vilevile tumejenga shule tatu mpya za msingi na tumejenga madarasa 207, vyoo vya wanafunzi na tumeboresha mazingira ya maliwato kwa wanafunzi na walimu. Tumejenga maabara katika shule zetu za sekondari kwa ajili ya kufundishia watoto wasomo ya sayansi. Hii ni kazi kubwa sana ambayo imefanywa na Serikali yetu katika wilaya yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sekta ya Afya tulipatiwa zaidi ya shilingi 6,753,000,000 katika kipindi hiki ambapo zimetuwezesha kujenga zahanati 15, vituo vya afya viwili,

tumeboresha vyoo na mifumo ya maji, ujenzi wa baadhi ya nyumba za waganga, majengo mapya katika hospitali yetu ya wilaya, lakini pia tumejenga jengo la mama ngojea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jengo la mama ngojea ni jengo ambalo kwa sisi, jiografia ya Wilaya yetu ya Namtumbo imekaa kushoto kushoto. Kuna watu wanatoka kilometa 254, kuna watu wanatoka kilometa 200, kuna watu wanatoka kilometa 120 na kata nyingine wanatoka kilometa 80. Kwa hiyo, kwa akinamama wanaopata *complications* za uzazi, wanapopata rufaa ya kuja kwenye hospitali ya halmashauri ya wilaya wanakuwa hawana maeneo ya kuishi. Hivyo basi tuliiomba Serikali itujengee jengo la mama ngojea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikubali ikatujengea jengo hilo. Tunaishukuru sana Serikali. Akinamama hao wanaotoka katika maeneo mbalimbali wanafikia katika jengo hilo na wasaidizi wao. Wanamwona daktari na kurudi katika jengo hilo. Kwa hiyo, imepunguza sana vifo vya akinamama na watoto. Hili ni jambo kubwa sana katika wilaya yetu na nchi yetu. Tunaishukuru sana Serikali kwa kutupa fedha za kujenga jengo hili la mama ngojea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza pia kujenga *mortuary*, majengo mengine na kadhalika. Hii kama nilivyosema ni kazi kazi kubwa sana ya kuhudumia wananchi wa hali ya kawaida katika nchi yetu, kule vijijini na katika Wilaya yetu ya Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la maji; ninaishukuru Serikali, tulitengewa jumla ya shilingi 17,583,000,000 katika kipindi hiki na miradi tisa ya maji yenye thamani ya shilingi 6,364,000,000 imekamilika na wananchi vijijini wanakunywa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utanuzi wa maji katika Kijiji cha Mwangaza kwenda Mtakuja, wananchi wanakunywa maji. Ukarabati wa Mtandao wa Maji Njomlole, wanakunywa maji, Ligunga, Lusewa, Maji Litola, Kumbala, Mradi wa Maji Likuyu, Masugulu na Likusanguse, kote huko wanakunywa maji. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwenye eneo hili la maji. Tuna maji mengi sana katika Mradi wa Litola – Kumbala – Litola. Ni maji ya mtiririko, yanakuja kwa nguvu ya *gravity*. Vilevile tuna kata ya jirani ambayo iko kilometa tano tu barabarani, inaitwa Kata ya Namabengo, ina shule kubwa ya sekondari lakini kuna uhaba wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuishauri Serikali kama itawezekana kutujengea tenki lingine la maji na kuweka mtandao wa maji ili yaweze kufika pale Namabengo, itatusaidia sana kupata maji. Kwa sababu maji ni mengi sana yanayokuja katika mradi huu na yakifungwa mipira huwa inapasuka. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali ifikirie kutuletea mradi wa kutujengea tenki la maji na kupeleka mabomba kuyasogeza kilometa tano ili yaweze kufika pale Namabengo ili kuweza pia kuhudumia shule ya sekondari yenye Watoto wengi sana wa kidato cha kwanza mpaka cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi pia ya shilingi 9,286,000,000 inayoendelea kujengwa Luhimbalilo, Naikesi, Mhangazi, Mgombasi, Msisima, Mnalawi na Mchomoro, hii bado inaendelea. Pia, tuna miradi mipya ya matokeo ya haraka ya maji *(quick win)*. Miradi hii bado haijaanza, lakini ipo katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuishauri Serikali, basi tungeweza kupata fedha hizo katika kipindi hiki kabla bajeti haijaisha. Katika maeneo hayo ni Limamu, Ligera, Muungano, Hanga, Misufini, Lumecha, Kitanda, Mtonya, Uboreshaji wa maji Kitulika, Sasawala, Magazini, Migelegele, Lwinga, Namtumbo, Minazini, Libango, Mageuzi, Mliyayoyo, Mdwema, Nambecha na Utwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa ajili ya programu ya visima vitano, tumeweza kufanikiwa. Katika kila jimbo tumepata na sisi tumechimba katika vijiji vitano; Kiwayuyu, Mteramwahi, Mtakanini, Kilimasela, Matepwende na lisimonji pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la barabara, katika kipindi hiki tunaishukuru sana Serikali kupitia *TARURA* tumeweza kutekeleza miradi ya barabara na vivuko kwenda vijijini na mashambani, ambapo Serikali ilitupatia zaidi ya shilingi 12,640,000,000 na tumeifanyia kazi ya kufungua barabara mpya, kukarabati barabara za zamani zinazokwenda vijiji kwa vijiji, tunaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la kilimo niliiomba Serikali iweze kutuletea miradi ya kuweka maghala, tunaishukuru sana Wizara ya Kilimo chini ya uongozi wa Mheshimiwa Bashe, waliweza kutuletea maghala nane ambayo yamejengwa katika maeneo ya: Mhangazi, Kitanda; Lumecha, Kata ya Msindo; Mtwara Pachani; Mtakuja; Lingusanguse; Matependwe; na Ligunga, tunawashukuru sana, sana Serikali. Maghala haya yametusaidia sana na yatatusaidia sana kuokoa upotevu wa mazao ya chakula kwa sababu ya kukosa uhifadhi sahihi, lakini pia itasaidia katika katika masoko ya stakabadhi ghalani na kuongeza kipato kwa wakulima wetu, hivyo tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ushauri kwamba unajua katika safari yoyote ya mafanikio pia kuna changamoto. Changamoto ya kwanza ni kwamba tunashukuru walituletea vituo vya kununulia mazao ya mahindi lakini vituo ni vichache. Kwa hiyo, tunaamini kabisa ujenzi wa maghala haya pia yatatumika katika ununuzi wa chakula cha mahindi na mazao mengine kupitia *NFRA*. Tunaiomba sana Serikali itumie maghala yale mapya makubwa mazuri kabisa. Pia yatatumika katika biashara stakabadhi ghalani, kwa hiyo, ninaomba sana pia yaweze kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunawashukuru sana..., kengele ya mwisho?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Rashid, ahsante sana.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, Mheshimiwa Shamsia Mtamba Azizi, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ajiandae.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hii bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Baba yetu mzuri Kassim Majaliwa Majaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali yangu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia, Rais wetu, lakini pia na timu yake nzima ukijumlisha na Waziri wetu Mkuu ambaye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali, kiukweli wao na timu yao wamefanya kazi nzuri, wamesema asiyekuwa na macho haambiwi tazama. Kwa hiyo, mimi niwaombe Watanzania kwa sababu wote tuna macho tuweze kuona na tuwe mashahidi wa kuelezea kazi nzuri ambayo imefanywa na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweze pia kutoa pongezi za kipekee kwa Chama changu Cha Mapinduzi. Chama ambacho kimejitabainisha kuwa ni Chama sahihi kuiongoza Nchi ya Tanzania. Wametekeleza Ilani kwa vitendo kama walivyoahidi wameweza kufanya. Pia, niwatakie kheri wagombea wote wa Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi, kwamba uchaguzi ni mpango ambao upo lakini Mungu ameshaandaa viongozi ambao wataenda kutumika kwa miaka mitano. Kwa hiyo, niwatakie Wabunge wenzangu wote kila la kheri kuelekea

uchaguzi na kiukweli tunaamini kwa kazi nzuri walizozifanya Mungu atawasaidia waweze kurejea Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani niipongeze Serikali kwa upande wa nishati ya gesi kwa zoezi la ugawaji wa mitungi ambalo limekwishapita. Tumeona Mheshimiwa Dkt. Samia na timu yake ambavyo wameweka ruzuku ya kutosha kwenye mitungi ya gesi. Wananchi wetu walio wengi wamepata mitungi ya gesi japokuwa kwa zoezi lilivyofanyika imeonekana uhitaji ni mkubwa. Tunakumbuka kabisa hii mitungi ya gesi inayotolewa kwa shilingi 20,000/= ilikuwa inauzwa karibia shilingi 75,000/=. Kwa hiyo, kitendo cha kuondoa shilingi 55,000/= hii inaonesha kwamba Serikali iko makini kuhakikisha wanawake wote wanakomboka na matumizi ya nishati zisizo safi na salama. Kwa hiyo, niwapongeze Wizara ya Nishati, lakini ninampongeza Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Rais kwa maamuzi magumu, kugawa mitungi halikuwa zoezi jepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu pia Serikali hii kwenye kilimo imetoa ruzuku ya kutosha kwenye mbegu na kwenye pembejeo. Kwa hiyo, hii itoshe pia kusema kwamba wananchi wetu ambao ni wakulima pia nao wanaendelea kunufaika na msaada ambao Mheshimiwa Rais na timu yake wameweza kuutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia nina maombi matatu ambayo ningetamani Serikali yangu iendelee kuyafanyia kazi. Kwanza, niiombe Serikali yangu kwa upande wa *NFRA*, changamoto iliyojitokeza kwa mwaka wa fedha uliopita ambapo wananchi hawakuweza kupata fedha kwa wakati tuwaombe kuelekea mwaka huu watakaponunua, kuelekea uchaguzi wetu, tafadhali wawalipe wananchi kwa wakati. Tulikuwa tunapokea simu nyingi ilikuwa ni tabu, sasa ilikuwa inatupa shida kama wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo, wananchi ili waweze kuwa na kipato endelevu waongeze ufanisi inatakiwa wawe wanalipwa fedha zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi maalum kwa Mfuko wa Pembejeo wapewe fedha kwa ajili ya uratibu ili waweze kuwafikia

wananchi na kuwaeleza habari njema ya mikopo ya pembejeo ambayo ipo. Hawa watu wanakuwa na fedha za utoaji wa mikopo lakini za uendeshaji unakuta hazipo. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuona ipo haja ya kutoa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa huo Mfuko wa Pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kama ombi maalum kwa Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi, kwamba mgawanyo wa walimu katika shule za Serikali uzingatie uwiano wa *gender*. Kwa maana ya kwamba sehemu yenye watoto wa kike wengi, pia kuwe na uwiano wa walimu wa kike unaoridhisha. Nimefanya ziara katika maeneo mengi unakuta walimu wa kike ni wachache sana. Basi kama Taifa walimu wa kike ni wachache basi ufanyike mpango maalum wa kufanya ajira za walimu wa kike tu ili kuleta uwiano wa walimu wa kike kwenye shule zetu. Kwa sababu tunasema ukimwelimisha mwanamke umeelimisha Taifa, haiwezekani tukawa na watoto mashuleni wanaolelewa na watoto wa kiume, sidhani kama hawa watoto watakuwa ni akinamama wazuri watakapokuwa wamepata nafasi ya kulea Taifa na watakapokuwa wamepata nafasi ya kupata watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujielekeza kwenye mchango ambao leo nilikuwa nimedhamiria kuuchangia kwa maslahi ya Serikali yangu. Serikali kupitia sekta mbalimbali imekuwa na zoezi la utoaji wa mikopo, kuna mikopo inayotolewa na Mfuko wa Pembejeo ambapo wananchi, wakulima na wajasiriamali mbalimbali wanapata mikopo huko. Vilevile, kuna mikopo kwa upande wa Wizara ya Mifugo na uvuvi, lakini kuna mikopo ambayo inatolewa kwa upande wa Wizara ya Nishati kupitia *REA*, kuna mikopo inayotolewa kupitia Maendeleo ya Jamii kupitia Programu ya Machinga na Wanawake, lakini kuna mikopo inayotolewa katika Wizara ya Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu, lakini pia tunafahamu kuna mikopo inayotolewa halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuongee ukweli dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia ni njema sana kuhakikisha wananchi

wake wanatoka hatua moja kwenda nyingine, kwa maana ya kwamba kuwainua kipato. Tunafahamu kabisa tuna wananchi wengi ambao kipato chao kiko chini na ndiyo maana hata Programu ya *TASAF* bado inaendelea kuwasaidia hawa maskini; lakini hatuioni ile dhamira ya wazi ya kwamba watu waliopewa dhamana kwenye haya maeneo ya kutoa hii mikopo kuwafikia wananchi wetu. Katika ziara ambazo zote nimefanya kwenye mkoa wangu ukiwauliza hata Watendaji wa Serikali unakuta hawana habari kuhusu hii mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa kuwa fedha zipo na fedha ni nyingi, Serikali ione haja ya kuwafikia wananchi na kuwaelimisha kwa habari ya hii mikopo. Ukiwauliza hata Wabunge humu ndani kuna watu hawajui hata kama kuna mikopo ipo *REA*, kuna watu unakuta hawafahamu kwamba kuna mikopo ambayo inatolewa huko ambayo sisi kama Wabunge wenye wananchi tulitakiwa tuijue na twende kutoa elimu kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo mikopo yote hii ya Serikali basi iundwe tume maalum ya kusaidia kutoa mikopo kwa wananchi. Kwa sababu kama kila Wizara itakuwa inajiratibu hata gharama za uendeshaji wa namna ya kuwafikia wananchi itakuwa kubwa, lakini tukiwa na tume maalum ambayo inaratibu mikopo yote ya Serikali kwa ngazi tofauti ninadhani hata utoaji wa elimu kwa jamii utakuwa mwepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali yangu ya CCM kwa namna ambavyo imekuwa ikiendelea kutekeleza zoezi la ukuzaji ujuzi kwa vijana. Tumefanya ziara nyingi katika Kamati yetu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, tumefikia vituo vingi ambavyo vijana wapo wanapatiwa elimu. Tulikutana na changamoto ambazo zipo; mojawapo ni kwamba vijana wanasajiliwa, lakini unakuta muda wa mafunzo ni mchache kuliko muda halisi wa mafunzo unaopatiwa, yaani Serikali imejiwekea muda mchache kuliko muda maalum wa mafunzo ambao unatakiwa watoto waweze kuhitimu. Niiombe Serikali yangu inapokuwa inatoa haya mafunzo basi izingatie utaratibu ambao upo wa utoaji wa hizo elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niiombe Serikali yangu kwamba kiwango cha pesa kinachotolewa bado ni kidogo sana, kwa sababu kama lengo lilikuwa ni kuwajengea ujuzi vijana 136,200 kwa mwaka, inakuwaje tunawajengea watoto 12,000 tu? Inakuwaje wakati Fungu tayari tulishakuwa tumelitenga kwamba kwenye *Skills Development Levy* tutakuwa tunatoa 1/3 ya mapato yale, lakini mapato yako juu kiwango cha pesa kinachotolewa ni kidogo hizi fedha nyingine ambazo tulizitenga kwenye hiyo 1/3 zinapelekwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali yangu sikivu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kweli ione haja kuwakomboa vijana wetu. Niseme kama kweli vijana watajengewa uwezo, kama kweli vijana watatafutwa popote walipo wakajengewe uwezo, ninaamini Taifa letu la Tanzania litasonga mbele. Maisha ya vijana ni magumu, maisha ya vijana huko mtaani yanasikitisha, vijana wamepoteza *confidence*, kitu ambacho kama Taifa tukiwatambua tukawawezesha, tukawaweka wakawa ni vijana wa kutumainiwa na kutegemewa, Taifa letu litasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuongelea upande wa Mji wangu wa Tunduma. Baada ya kumaliza haya ya vijana nitataka kuongelea kwa upande wangu wa Tunduma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia sentensi yako.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Tunduma iangaliwe kwa jicho la tofauti, ni fursa kwa Taifa, ni fursa kwa kipato cha Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mheshimiwa Sylvia

Francis Sigula, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, wajiandae.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia Hotuba hii ya Waziri Mkuu. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nzuri na leo hii nikaweza kusimama katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze na nimshukuru Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu ya kuhakikisha tunapata maendeleo mijini na vijijini. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya tumeona amekuwa akimsaidia Mheshimiwa Rais katika maeneo mbalimbali, kwa kweli ninampongeza sana kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nikupongeze kwa kazi nzuri ambayo unaifanya na tunaona namna unavyoendesha Bunge letu vizuri, Mwenyezi Mungu akujalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitaanza kuchangia kwenye mambo ya barabara, Barabara ya Kibiti – Lindi – Somanga. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ulega kwa hatua kubwa aliyoichukua baada ya changamoto hii kutokea. Tulimwona, alikwenda pale na akatoa maelekezo na sasa hivi tunaona magari yameanza kupita. Kwa hiyo, hii ilikuwa ni suluhisho la muda mfupi, tunahitaji suluhisho la muda mrefu katika Barabara ya Kibiti – Somanga – Lindi, bado barabara hii imekuwa na changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara hii ya Kibiti – Somanga – Lindi kuanzia Mbagala mpaka unafika Lindi barabara ni mbovu, barabara ina mashimo mengi. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iangalie barabara hii kwa macho mawili, barabara hii ni barabara ambayo ina umuhimu mkubwa sana kwetu sisi watu wa kusini. Barabara hii ina changamoto nyingi, ina mashimo mengi maeneo

mengi hayapitiki. Kwa hiyo, niiombe Serikali iiangalie barabara hii kwa macho mawili, barabara hii haikutengenezwa vizuri, barabara hii ilitengenezwa kwa kiwango cha *low standard*. Kwa hiyo, niiombe Serikali iingize barabara hii kwenye mpango Barabara hii ya Kibiti – Lindi ili iweze kupitika vizuri na sisi Wananchi wa Mtwara – Somanga – Kibiti – Ikwiriri – Lindi tuweze kuitumia barabara hii vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mtwara kwa miaka mingi tumekosa usafiri wa njia ya bahari (usafiri wa meli) kwa miaka mingi sana. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali sisi Mtwara tuna bandari nzuri na bandari yetu imefanyiwa maboresho mazuri, tunaomba tuletewe meli kwa ajili ya abiria itaweza kutusaidia sana. Barabara inavyopata changamoto tukiwa na usafiri wa bahari (usafiri wa meli) tutaweza kutumia vizuri na changamoto hii itaweza kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila bajeti ambayo tunakaa huwa ninazungumzia sana barabara ya ulinzi na barabara ya uchumi, barabara hizi ni barabara muhimu sana. Tuna Barabara ya uchumi ambayo inaanzia Ziwani – Madimba – Msimbati ninaiomba sana Serikali, kule imeweka uwekezaji mkubwa sana, kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa sana wa Barabara hii ya Madimba – Msimbati ijengwe kwa kiwango cha lami. Kila siku hapa tunaambiwa maneno kwamba barabara hii imeingizwa kwenye mpango ninaiomba sana Serikali barabara hii kweli iingizwe kwenye mpango na ijengwe kwa kiwango cha lami kutokana na umuhimu wake. Kule kuna mitambo ya gesi Madimba ndipo inapochakatwa gesi, kwa hiyo tuna kila sababu ya kupata barabara nzuri, ambayo inapitika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la fidia. Hapo nyuma tulikuwa na mradi mkubwa wa maji wa Mto Ruvuma, Mayembe Chini. Takribani vijiji 25 vilitarajia kunufaika na mradi huu wa maji. Mpaka sasa uthamini ulishafanyika katika hivyo vijiji kwa ajili ya mradi huo wa maji, lakini mpaka sasa hivi vijiji hivyo hawaelewi chochote na hawajui chochote ambacho kinaendelea. Vijiji hivyo ni kama vifuatavyo: Mayembe Chini; Kitaya; Kihamba; Kivava; Maulunga; Kihimika; Magomeni Nyasi;

Tangazo; Itembe; Madimba; Namindondi; Mtendachi; Ziwani; Mtawanya; na Mangamba. Tangu mwaka 2025 vijiji hivi vilifanyiwa uthamini, wananchi wanashindwa kuendeleza maeneo yao kwa ajili ya fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo hatuelewi huo mradi kama upo au umekufa na kama haupo basi hawa wananchi warejeshewe maeneo yao ili waweze kuyaendeleza maeneo yao. Kwa sababu kwa muda mrefu sana takribani miaka 13 sijui 14 wananchi hawa hawaelewi kinachoendelea kuhusiana na mradi huu. Kama fidia watalipwa, walipwe na kama huo mradi haupo basi hawa wananchi warejeshewe maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *TARURA*, *TARURA* iongezewe pesa ili ziweze kutanua na kufungua mitandao ya barabara zetu. Barabara zetu za vijijini ni mbovu mno, na hazipitiki, lakini *TARURA* wanajitahidi kutaka kufanya kazi kuhakikisha wanafungua mtandao wa barabara lakini wanakwama kwa ajili ya pesa. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iweke fedha za kutosha kwa ajili ya kufungua mtandao wa barabara za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Taarifa inatoka wapi?

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Felista Njau.

**MWENYEKITI:** Haya Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nimpe taarifa mchangiaji anayeongea Mheshimiwa Shamsia, suala la *TARURA* limekuwa kwikwi na kimsingi mtandao wa *TARURA* nchini wa bajeti ya *TARURA* ipo

lakini haifiki kwenye majimbo na mikoa ya kimkakati hasa Jimbo la Moshi Vjijijini kuna shida kubwa mameneja wapo vizuri, wanafanya vizuri sana, lakini hawana pesa kwenye mifuko yao. Kwa hiyo, tutawaumiza bure tuwape pesa watu wa *TARURA* wafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarudia kila siku ni kilio, ni kilio

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** …Mtwara, ni sawa na Moshi. Naomba *TARURA* wapate pesa.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka, Mheshimiwa Shamsia unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nimeipokea taarifa kwa mikono miwili. Kwa kweli changamoto ndiyo hiyo kwa mfano katika jimbo langu kumekuwa na changamoto kubwa sana na barabara kwa mfano Kata ya Kitele kuna sehemu imekatika kabisa barabara kila siku nawapigia simu *TARURA* waende wakarekebishe sehemu ile sasa hivi wanashindwa kunipokelea simu kwa sababu hawana pesa za kutosha za kuhakikisha wanakwenda kutengeneza zile barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara ya Mikindani – Kitope – Naumbu nayo imekatika hamna mawasiliano kabisa ninawasumbua kila siku *TARURA* kuwaambia waende wakarekebishe maeneo yale lakini nao wanashindwa kwa sababu hawana pesa za kutosha za kwenda kuhakikisha wanarekebisha barabara zetu. Kwa hiyo, niiombe Serikali iweke fedha nyingi za kutosha katika Mfuko wa *TARURA* ili waweze kufungua mtandao wa barabara zetu za vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije niongelee kwenye suala la watumishi, katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini kumekuwa na shida kubwa sana ya watumishi kada ya afya pamoja na elimu.

Kwa hiyo, niiombe sana Serikali iangalie Jimbo la Mtwara Vijijini waniletee walimu wa kutosha pamoja na wauguzi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, ahsante sana. nilimtaja Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hotuba hii ya bajeti ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wote ambao kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana katika kipindi hiki cha miaka minne na nusu ambayo tunaimaliza sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianza na Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ambayo ilielezea mambo mbalimbali kwa wananchi wakati wa uchaguzi wa mwaka 2020 na wananchi waliikubali ilani ile kwa maana ndiyo ulikuwa mkataba kati ya chama, kupitia Serikali yake na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kabisa kukipongeza Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuandaa ilani na hatimaye kusimamia utekelezaji wake. Niendelee kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wetu tena wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhakikisha wamesikiliza vilio vya wananchi na hoja mbalimbali ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiziwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jimbo langu nishukuru sana Serikali yangu chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Katika kipindi hiki cha miaka minne na nusu, suala la elimu msingi, tumepata shule mpya za msingi nane, lakini katika suala la shule za sekondari, tumepata shule mpya za sekondari saba ukiachana

na ongezeko la madarasa katika shule zote zilizokuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu pamoja na wingi wa watu sasa hivi tumeshuhudia tunayo Shule ya *English Medium* ya Serikali tunaendelea kuipongeza sana Serikali yetu. Tulipotoka hatukuwahi kuwa na shule ya kidato cha tano na cha sita katika Jimbo langu la Mbagala sasa hivi tunazo shule mbili za kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, tunawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, kwa maana mambo haya yote tuliyazungumza kama Waheshimiwa Wabunge. Hivyo tulitoa hoja kwa Waheshimiwa Mawaziri na wao Waheshimiwa Mawaziri, wametusikiliza na hatimaye Mheshimiwa Rais wetu ametupa fedha za kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la afya, katika jimbo langu kwa sasa hakuna kata ambayo haina zahanati au kituo cha afya. Kazi nzuri sana imefanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia watendaji wake kuanzia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wote ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi katika Jimbo langu la Mbagala sasa hivi tunavyo vituo vipya vya afya vitano, vituo ambavyo vimejengwa katika kipindi hiki cha awamu ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hata hivyo, tumejenga hospitali ya wilaya nyote mnafahamu *population* ya pale Mbagala ilivyokuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu ametupa zaidi ya bilioni 10, tunajenga hospitali ya wilaya ya ghorofa sita lakini pia tuwashukuru sana watu wa Wizara ya Afya wametupa eneo pale eneo la Muhimbili iliyokuwepo Kata ya Chamazi na tumeingia makubaliano kati ya Muhimbili na Manispaa ya Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga hospitali ya pili ya wilaya lakini pia tunajenga ghorofa moja kwa ajili ya madaktari bingwa wa Muhimbili. Sasa hivi wananchi wa jimbo langu la Mbagala ile adha ya kwenda mbali kufuata *referral* ya kwenda Mloganzila tunaenda kuondokana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Barabara, tunaishukuru sana Serikali tunazo barabara za aina mbili; barabara zile za *TANROADS* na barabara za *TARURA*. Katika jimbo langu barabara za *TANROADS* ambazo zilikuwa zina shida na nimeziombea sana katika Bunge letu hili ni Barabara ile ya Kokoto - Kongowe kwenda Mwandege. Habari njema Mheshimiwa Rais wetu amelipa fidia zaidi ya shilingi bilioni 16.8 kwa wananchi wote ambao wanapisha ujenzi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mikataba miwili imeshasaini; mmoja mkataba wa ujenzi wa daraja kubwa lile la pale Mzinga, lakini mkataba wa ujenzi wa barabara ya njia sita, nne za magari, mbili za mwendokasi; tunatarajia mwendokasi sasa utakwenda hadi Vikindu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya pili ni ile Barabara ya Mbande – Msongola, katika kipindi chote cha Bunge nilikuwa naisemea sana barabara hii tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kutupa fedha. Pia tuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhakikisha barabara hiyo sasa inaendelea na ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la *TARURA*. Tuendelee kushukuru miradi ya *DMDP* imesainiwa katika awamu tofauti tofauti na wakandarasi wanatakiwa waje *site*. Hapa ndiyo nataka nianze kutoa maombi yangu kwa Serikali na naamini kwa sababu Serikali yetu hii ni Serikali ambayo inafanya vitu kwa vitendo na hawajawahi kuniangusha pale ambapo nimeomba jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba sana wakandarasi wote waliopewa kazi ya kujenga Miradi ya Uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam *DMDP* tunawaomba sana Serikali wawasimamie

kwa sababu wameshasainiwa mikataba na taarifa tulizokuwa nazo *advance payment* walishapewa. Kwa hiyo, waingie *site* waanze ujenzi ili wananchi wa Jimbo la Mbagala sasa na wa Dar es Salaam kwa ujumla waone namna gani Serikali yao inavyowajali katika kutekeleza miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo barabara mbalimbali za *TARURA* ambazo kwa kweli bado hazijawa vizuri tunaiomba sana Serikali kwa kipindi hiki kilichobaki na kipindi kijacho tuwekeze nguvu zetu sana katika kuboresha barabara za ndani Barabara za Kata ya Chamazi, Kata ya Charambe, Kata ya Mianzini, Kata ya Kilungule, Kata ya Mbagala, Kata ya Kiburugwa, Kata ya Mbagala Kuu, Kata ya kijichi, Kata ya Kibondemaji na Kata ya Tuangoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua *population* ya Mbagala ni kubwa sana barabara hizi za TARURA zikifanyiwa utaratibu wa kutengenezwa basi wananchi wetu wataendelea sana sana kufurahi na hatimaye tunatarajia kupata kura nyingi za kishindo katika uchaguzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo la umeme katika Jimbo la Mbagala na hapa ndiyo naomba nizungumze sana. Tunafahamu *TANESCO* wanafanya maboresho ya umeme katika Jimbo la Mbagala, wanabadilisha nguzo kutoka nguzo za miti kuleta nguzo za zege, lakini tatizo lililokuwepo mabadilisho yao ya nguzo yanatumia zaidi ya saa 18 mpaka 20 kwa siku sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe Serikali tubadilishe utaratibu wafanye kubadilisha hizi nguzo kuanzia saa 12 asubuhi mpaka saa 11 jioni, ili wananchi ikifika saa 12 waweze kupata umeme ambao utasaidia usalama mkubwa katika Jimbo la Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbagala lina watu wengi na kama lina watu wengi linahitaji lipate umeme muda wa usiku ili wananchi wao waendelee kudumisha usalama. Tunaiomba Serikali hali ya sasa ya Mbagala ni ngumu sana katika suala zima

la umeme. Tunaomba waangalie upya suala hili ili umeme uweze kupatikana muda wa jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie suala la maji, Jimbo la Mbagala linategemea maji kutoka Mto Kizinga lakini kwa sasa tunategemea maji kutoka katika visima mbalimbali vikiwepo vile visima vya Kisarawe II, tuiombe sana Serikali na hasa Mheshimiwa Waziri wa Maji katika bajeti ya mwaka huu waweke fedha nyingi kwa ajili ya kusambaza maji katika Jimbo la Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visima vile vya Kisarawe II tayari vina maji ya kutosha na wanufaika wakubwa wa visima vile ni katika Jimbo la Kigamboni na Jimbo la Mbagala katika Kata ya Chamazi Kata ya Charambe, Kata ya kijichi, na Kata ya Tuangoma. Tuwaombe sana Serikali iweke nguvu na iweke fedha za kutosha kuhakikisha suala hili la maji linapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kabisa wananchi wa Jimbo langu la Mbagala wanaiamini Serikali yao na wanakuja kwa kishindo kuhakikisha ile rekodi tuliyoiweka mwaka 2020 ya kupata kura nyingi kwa wagombea wa CCM tunaenda kuirudia mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo ahsante sana. nilimtaja, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mheshimiwa Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara wajiandae.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuweka mchango wangu katika Wizara hii muhimu, Wizara ambayo imewasilisha ripoti yake hapa chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu na ni Wizara ambayo inatugusa sisi vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mungu, namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema nami leo

nimesimama mbele ya Bunge letu hili Tukufu nami kuweka mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wasilisho lake zuri kwenye hotuba hii aliyoiwasilisha mbele yetu. Pia ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa sisi vijana Mheshimiwa Ridhiwani pamoja na wasaidizi wake wote na timu nzima wa Wizara hii ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitajielekeza katika ajenda kubwa ya sisi vijana ya changamoto ya ajira. Hapa ninaomba sana kwa dhati ya moyo nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwaka 2020 wakati tunainadi Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, tulipita kwa vijana wa nchi hii kuwaambia kwamba tutatengeneza ajira 8,000,000 kwa vijana wa Taifa letu. Leo kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaona jambo hili limefanyika kwa vitendo na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amelisimamia na leo tumetimiza ajira 8,000,000 kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu, sisi vijana tunampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu tunaiona dhamira yake ya dhati ya kupambana na changamoto hii ya ajira kwa vijana. Pamoja ya kuwa ameshatengeneza ajira milioni nane kupitia kwenye ilani, lakini bado tunaona dhamira yake inaenda kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mambo mengi ambayo yanaonesha kabisa ni dhamira ya dhati ya kupambana na changamoto ya ajira kwa vijana. Mheshimiwa Rais huyu amejenga nchi hii Vyuo vya VETA, karibu halmashauri zote zina vyuo vya *VETA* yote hii ni mapambano ya changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amerejesha mikopo ya 10% ya halmashauri ambayo kwa muda mrefu ilikuwa imesitishwa yote hii ni mapambano ya changamoto ya ajira kwa vijana, lakini tunaona program

mbalimbali zinaendelea kuna Samia *Scholarship* yote hii ni mapambano na kutoa fursa kwa vijana ili waweze kujikwamua na changamoto ya ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niliomba sana wasaidizi wa Mheshimiwa Rais waibebe ajenda hii kama ambavyo Mheshimiwa Rais anaibeba. Chini ya Serikali kuna Mifuko ambayo inatoa mikopo moja kwa moja kwa walengwa Mifuko zaidi ya 22 si hiyo tu chini ya Serikali, kuna Mifuko inayotoa ruzuku, Mifuko inayotoa ruzuku ambayo ipo chini ya Serikali ni Mifuko 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu chini ya Serikali kuna programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi zipo programu zaidi ya tisa sisi vijana wa Taifa hili tunaona bado vijana hatuna taarifa sahihi kuhusu Mifuko hii. Leo ukienda Rukwa kijana wa Nkasi ukimuuliza ni mikopo mingapi ambayo unaweza ukaipata kwenye Serikali atakwambia ni mikopo ya halmashauri tu, lakini tuna taasisi nyingi chini ya Serikali ambazo zinatoa mikopo, lakini vijana bado hatuna taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunatamani sana kuona Serikali inaweka mkakati ambao utatoa taarifa kwa vijana wa nchi hii kuifahamu Mifuko hii na iwanufaishe moja kwa moja. Ili kijana aweze kupata huduma kwenye Mifuko hii ambayo ipo chini ya Serikali, itamlazimu aje Dodoma. Najiuliza kijana kutoka Wampembe, kijana wa kutoka Kalambo, Kijana wa kutoka Laela anafikaje Dodoma, anapataje *access* ya kufikia Mifuko hii ya uwezeshaji wa vijana ambayo ipo chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali hii Mifuko ni kwa ajili yetu sisi vijana, lakini Mifuko bado haijafika chini kwa walengwa wenyewe ambao ndiyo dhamira ya Mheshimiwa Rais. Sasa kwa sababu vijana wana uelewa mkubwa na mikopo ya halmashauri, tulikuwa tunaomba Mifuko hii ishuke au iwe *connected* na mikopo ile ya 10% ya halmashauri. Vijana watakapoomba pale kwenye halmashauri zao, kama halmashauri wataona wao hawana uwezo wa kuwapa ile mikopo kwa sababu vijana ni wengi, basi moja kwa moja wao wapeleke

maombi yao kwenye Mifuko hii ambayo inawawezesha vijana kiuchumi hiyo itatusaidia vijana wengi kuifikia Mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu natamani sana kuona Serikali inaweka mkakati maalum, kuona Serikali inaweka utaratibu maalumu ambao utatuambia ni kwa kiasi gani kijana mkulima wa kijijini, kijana mvuvi aliyepo Kasanga kule anapata faida na Mifuko hii ambayo ipo chini ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mifuko hii ipo mbali na sisi vijana hatuna taarifa nayo na ndiyo maana vijana wengi tunaona kwamba Mifuko hii ipo kwa ajili ya watu wa mijini, lakini dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha vijana wote awe wa kijijini, awe wa mjini anapata fursa sawa kama Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wawakilishi vijana tumekuwa tukipita kwa vijana kupokea maoni yao kuhusu mikopo ya 10% ambayo inatolewa na halmashauri. Kwanza tunaishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, mikopo baadhi ya halmashauri wametoa na mikopo mingine utaratibu unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, changamoto bado ipo. Vijana wanatamani sana kuona mikopo hii inatolewa kwa mtu mmoja, mmoja. Bado sharti la kikundi limekuwa ni jambo ambalo linawafanya vijana wengi wakose fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukisema hapa na nimewahi kuuliza swali hapa, tukaambiwa kwamba wanakopa kwa kikundi, lakini pesa anapewa mtu mmoja, mmoja. Bado sharti la kikundi lipo pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba sana Serikali, tuna vijana wengi wabunifu na tumeona kwa kuanzishwa hizi *VETA*, vijana wengi wameenda na wamepata ujuzi. Changamoto kubwa ya vijana kwa sasa ni mitaji. Sasa naiomba Serikali kuona namna nzuri ya kuwakopesha vijana mmoja, mmoja na kuacha sharti la kikundi kama sharti la lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii mikopo ambayo inatolewa, bado ni midogo. Naungana na maoni ya Kamati. Maoni ya Kamati yanasema, Serikali iendelee kutoa fedha kwenye hii mifuko. Ukiangalia huu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, mwaka wa fedha 2024/2025 mpaka kufikia mwezi Machi, ilikuwa imetengwa zaidi ya shilingi milioni 600, lakini mpaka kufikia mwezi Machi, hakuna hata shilingi moja ambayo imeenda huko. Sasa kwa hali hii hao vijana wanaenda kunufaika vipi? Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ione uzito wa jambo hili la vijana na itoe fedha ili vijana waweze kunufaika na mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitamani sana kuliongelea kwenye Wizara hii, ni vijana. Vijana wa nchi hii ni wapambanaji sana na sisi ni mashahidi. Ukichukua sensa ya watu na makazi, vijana ni asilimia kubwa ya wananchi wa Taifa letu hili. Pia, vijana tumepata mafunzo, tuna elimu nzuri, tuna ujuzi, lakini changamoto yetu imekuwa suala la uwezeshaji wa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tunafanya hizi programu kwa pamoja, hizi programu ziwe na *package* nzima. Kama tunampeleka mtu *VETA* akapate mafunzo, akapate ujuzi, tusipomwezesha vifaa, ile elimu inakuwa haijaleta tija. Kwa hiyo, naomba sana hii programu iwe na muunganiko wa *package* nzima. Huko huko *VETA* tuwatambue, tuwapatie vifaa baada ya mafunzo kwa sababu kuna mifuko inayowawezesha, inawapa mikopo, waunganishwe moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ni muhimu sana kwa Taifa letu, tunafurahi sana kuona mipaka imefunguka, nchi imefunguka na vijana wanatamani sana kufanya biashara. Kuna suala la vijana au raia wa kigeni kufanya biashara kuliko raia wa Tanzania, tena biashara ambazo ni ndogo ndogo ambazo zingeweza kufanywa na vijana wetu wa kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili naomba sana liangaliwe kwa kina, ni jambo ambalo lipo na ni jambo ambalo vijana wetu wanakatishwa tamaa. Leo unaenda Kariakoo, unakuta raia wa

kigeni anauza mpaka vitana vya buku buku ambavyo sisi wazawa tungeweza kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana jambo hili lichukuliwe kwa uzito wake, vijana wa Kitanzania tupo timamu, tuko tayari na tunaweza. Tunaomba tu uwezeshwaji wa kifedha tuweze kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula. Nilimtaja Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, wajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, naungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu kwa ujumla na hususan katika Jimbo langu la Musoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, sasa tuko mwisho kwa maana ya awamu hii, ndiyo miaka yetu mitano sasa tunaelekea kumaliza. Hata hivyo, mimi binafsi kama Mbunge ninayetoka Musoma Mjini, niseme moja tu kwamba naipongeza sana au ninaishukuru Serikali kwa namna ilivyoweza kunipa fedha za kutosha na kwa namna hata kwenye zile ahadi tulizoahidi. Kusema kweli kwa Musoma Mjini tumefanya zaidi ya pale tulipotarajia kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza sana Mama Samia, na wapigakura wangu wa Musoma Mjini kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote cha Ubunge wangu wa awamu hii katika kipindi chote cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa ufupi kwamba kati ya yale mambo tuliyoyaahidi, yaani mimi pale kwangu karibu yote yameisha. Maana leo unapozungumza, mfano habari ya elimu; kulikuwa na tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa, uhaba wa shule, lakini leo kila mtoto wangu anayefaulu anakwenda sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tumekuwa na *secondary in excess* kwa sababu hata katika kipindi cha mwaka 2024 na mwaka huu 2025 peke yake nimepata sekondari zaidi ya mbili, nimepata shule za msingi zaidi ya mbili ambazo zote Mheshimiwa Rais amenipatia fedha zaidi ya shilingi milioni 500 kila shule, na shule zimejengwa, sasa watoto wanaendelea kusoma. Hiyo ni mbali na zile shule zilizokuwepo. Kwa hiyo, kwa upande huo siyo shule ya msingi, siyo sekondari, naomba niseme tu, tuko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto ndogo tu ambazo na sisi tunaendelea kuzimaliza. Moja, ni pamoja na ile changamoto ya watoto wetu kukaa chini. Hata hivyo, niseme tu kwamba leo mimi hapa nilipo pamoja na wadau wangu wa maendeleo, tumejitolea, tunatengeneza madawati zaidi ya 3,500. Tunahitaji watoto wote wakae juu ya madawati na mengine yabaki ya *reserve* kwa ajili ya watoto wengine watakaokuja ili waendelee kusoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ungeenda kwenye afya, na kwenyewe tumefanya vizuri, kwa maana kuna hospitali yetu ya rufaa inaendelea vizuri. Pia, ile hospitali yetu ambayo Mama alitupatia Manispaa, inaendelea vizuri na vituo vya afya ametupatia fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo changamoto ipo ndogo, na hata nimemwuliza hapa Waziri wa Afya na majibu nimepata kwamba ile *X-Ray* yetu ambayo ilikuwa haijakamilika, wakati wowote ndani ya wiki mbili itaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, kwenye upande huo, naendelea kumshukuru sana Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyoendelea kutoa fedha kwa ajili ya maendeleo ya Jimbo langu la Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumza habari ya maji, mimi niseme nini kwa sababu maji kwangu ni 100%, yaani hakuna mtaa usiokuwa na maji. Maeneo yote yana maji, na ni maji ya kutosha. Kwa hiyo, kwenye huo upande sasa hivi tunachoendelea nacho ni kusogeza tu maji, yaani kila mwananchi asiende zaidi ya mita 200 kwenye upatikanaji wa maji. Kwa hiyo, kwenye huo upande nako wala mimi sina lawama kabisa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, ukizungumza habari ya umeme, nadhani katika hili Bunge lote ni Jimbo langu pekee ambalo tuko mjini, lakini tumepata umeme wa gharama nafuu ya shilingi 27,000 katika ile mitaa yote ya pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna alivyosikiliza kilio changu akaweza kunipatia umeme wa bei nafuu pamoja na kwamba mimi ni mtu wa mjini. Hivi tunavyoongea, wakandarasi wanaendelea kusambaza huo umeme wa gharama nafuu. Kwa hiyo, naendelea sana kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, hata ungegusa barabara. Ziko zile barabara za *TARURA,* mvua ilipokuja imetusumbua kidogo, lakini sasa hivi tunaendelea na matengenezo, fedha tunazo japokuwa hazitoshi, lakini walau maisha yanaendelea. Mbali na hiyo, tumepata fedha, tunajenga kwa kiwango cha lami na hivi tunasubiri mkandarasi aingie *site* kuanzia pale *Musoma Bus* kwenda kwenye ile Hospitali yetu kubwa ya Kwangwa. Pia, hata ile Barabara yetu ya Shabani na yenyewe mkandarasi anaingia pamoja na ile Barabara ya Mkendo, huko kote tunachapa lami. Kwa hiyo, naendelea kumpongeza na kumshukuru sana Mama yetu Samia kwa namna alivyoendelea kuleta fedha katika Jimbo langu la Musoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tulikuwa na stendi mbovu. Leo yeyote yule akienda pale ataangalia ataona sasa stendi imeanza kubomolewa, mkandarasi amepatikana, tunajenga stendi kwa zaidi ya shilingi bilioni 14 ili watu wetu

waendelee kufanya biashara zao au wasafiri kwa raha wakifika pale kwenye stendi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, hata kwenye lile soko letu la Nyasho kwa zile fedha tulizopata, soko limebomolewa, linajengwa soko la kisasa ili wajasiriamali wetu na wananchi wetu waendelee na maisha yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusema kwamba, leo ninapokuja mbele yenu, kikubwa ninachoendelea, ni kushukuru, maana kwa haya mambo makubwa yaliyofanyika, tuna kila sababu ya kushukuru, na tuna kila sababu ya kujivuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye habari ya uvuvi, leo ninaishukuru Serikali, wameweza kutupatia vizimba vya kutosha, wajasiriamali wetu wamepewa mikopo, kwa hiyo, wanaendelea na maisha yao. Tuna vizimba zaidi ya 14, lakini hata leo tu nilikuwa nazungumza na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, anasema wakati wowote atatupatia vizimba vingine. Hapo pote ni kwamba wananchi wetu waendelee kujenga uchumi wao na maisha yao yaendelee vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilidhani kwamba niseme hayo kama baadhi tu ya shukrani katika mambo mengi makubwa ambayo tumeendelea kuyapata katika Jimbo letu la Musoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mafanikio, zipo changamoto chache zinanisumbua na katika zile changamoto chache zilizopo ni kwamba kuna kile kilichokuwa Kiwanda cha *Mutex,* bado watumishi wake bado wanadai mafao yao baada ya kuwa Serikali imekibinafsisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba siku zote Serikali huwa inatupa *comfort* kwamba inatafuta fedha kwa ajili ya kuwashika mkono, basi naomba ijitahidi katika bajeti hii waweze kulipwa mafao yao na waweze kuendelea na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni la kuikumbusha Serikali tu, ni ile mikopo ya huduma za pensheni kwa watumishi. Nakumbuka mwaka jana 2024 tulipitisha, sasa watumishi wengi kule wananiuliza, hiyo mikopo inaanza kutoka lini ili waweze kupunguza ile mikopo ya riba kubwa (mikopo ya kausha damu)? Kwa hiyo, hilo nalo naikumbusha tu Serikali yangu iweze kuliangalia ili huo msukumo uwepo na maisha yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo ni la mwisho na kwa kweli kule kwetu linatusumbua, baada ya haya mafanikio yote kuwa yamepatikana, huduma za kijamii zote zimepatikana, lakini watu wangu wa Jimbo la Musoma mifukoni mwao, hali siyo nzuri. Hali siyo nzuri kwa sababu viwanda vingi vimekufa na hili tatizo la viwanda kwa kusema ukweli ni tatizo la nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali sasa ina haja ya kulifikiria upya, maana viwanda vingi vilijengwa na Serikali wakati ule ilipokuwa inajishughulisha na biashara. Sasa tulipoingia kwenye ubinafsishaji, Serikali ikaachana na vile viwanda, tukavibinafsisha kwa watu binafsi. Kwa hiyo, vimeendelea kufa kimoja baada ya kingine. Sasa nadhani ni wakati mwafaka Serikali iliangalie tena, itakuja na *modal* gani namna ya kufufua viwanda ili watu wetu waendelee kupata ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli tatizo la ajira bado ni kubwa sana na bahati nzuri katika nchi yetu tuna nguvu kubwa sana ya vijana. Wale vijana Serikali inajitahidi, inawasomesha, wanamaliza elimu ya msingi, sekondari, inawapeleka mpaka vyuo wakishamaliza ajira zinazopatikana Serikalini ni chache sana na zile zinazopatikana kwa watu binafsi, ni chache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani tuna kila aina ya sababu ya kuangalia *modal* mpya ya namna ambavyo tunaweza tukawaajiri vijana wengi katika kilimo, biashara na tukawaajiri vijana wengi katika ujasiriamali. Ndiyo maana leo ukiangalia wapo hata wageni wengi wanaingia, wanachukua ajira za vijana wetu na hao vijana unawakuta saa sita mchana wapo kwenye *pool* kwa sababu hawana kazi za kufanya kwa sababu hawana mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunadhani kwamba katika hii bajeti inayokuja na huko tunakoenda katika kipindi kingine cha miaka mitano, hebu Serikali yetu ijikite zaidi katika kuona namna ya kuboresha ajira za vijana ili maisha yao yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana, naunga mkono hoja na ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo. Nilimtaja Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu wajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Baada ya bajeti hii, nitakuwa nimetimiza miaka 10 nikiwa nahudumu katika Bunge hili kama mwakilishi wa wananchi katika mikoa miwili tofauti na majimbo mawili tofauti. Kwa hiyo, nina uzoefu wa kutosha, na kwa kweli nikitaka kuzungumza miaka mitano ya utumishi wangu Tarime Vijijini na miaka minne ya Mama Samia, nahitaji masaa mawili. Sasa wamenipa dakika 10 tu, nitaeleza kwa muhtasari tu baadhi ya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Tarime Vijijini mwaka 2021 mpaka sasa hivi tunapozungumza tumejenga madarasa ya shule ya msingi 376 sawa na shilingi bilioni 7.256. Tumejenga shule mpya 13 za Mama Samia, Getena na Kewanja zimejengwa kwa thamani ya zaidi ya shilingi milioni 500 na watoto wanasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madarasa ya sekondari 322 sawa na shilingi bilioni 6.57, kwa upande wa shule mpya, Tarime Vijijini tumejenga shule za sekondari 19. Pia, Shule ya Bukira, Nyastaricho, Mtana na Nyandage zimejengwa na Mama Samia bila mchango wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ninapozungumza, tumetengeneza madawati ya shule ya msingi 6,765 pamoja na viti na meza 5,869. Tumekubaliana kwamba kwa kuwa mpango uliopo ni kunirudisha uchaguzi ujao, basi mwaka 2025/2026 shida ya madawati, viti na meza Tarime Vijijini itakuwa ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ninapozungumza hapa, tumejenga vituo vya afya vitano, sawa na shilingi bilioni 3.66. Maji yameenda kwenye kata 24 isipokuwa kata mbili (Pemba na Mbugi) kuna shida ya vyanzo vya maji. Tunaendelea kufanya kazi ya kutafuta vyanzo vya maji, vikipatikana, wananchi wangu wapenzi wa maeneo hayo watapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango wa maji kutoka Ziwa Victoria ambao utaenda Sirari, uende mpaka Mriba, Nyansicha. Pia, utaenda Mogabiri - Nyamwaga – Komaswa - Nkerege – Nyamongo na tunatarajia kwenda mpaka Karakatonga katika Kata ya Kwihancha kupata maji safi na salama ya kunywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* tumefanya kazi nzuri sana, mvua zimenyesha sana katika Jimbo la Tarime Vijijini lakini maeneo mengi yanapitika. Tumepata madaraja makubwa Magoma, Kebweye kwa zaidi ya shilingi milioni 510, lakini sasa nimeambiwa mkandarasi ameshapatikana kujenga Matongo iunganishe Kibasuka ili watu wa Nyamango kama wanakuja Musoma siyo lazima wapite Nyamwaga, wanaweza wakakatisha katika yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Barabara ya Mogabiri - Nyamongo kilometa 25 imeenda mpaka Kemakorere. Tunaomba Mheshimiwa Waziri anayehusika aongeze kasi ifike Nyamongo, iende Mugumu - Serengeti ili tuunganishe Tarime na Wilaya ya Serengeti na watu wetu wapate huduma, ulinzi, usalama, utalii na uchumi utaongezeka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata fedha zaidi ya shilingi bilioni kadhaa katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Tumejenga jengo la utawala, *X-Ray Machine* ya kisasa ya

kidijiti, *mortuary,* uzio na ujenzi unaendelea. Ninapozungumza pale kuna shilingi milioni 900 na kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyamongo kumejengwa *VETA* kwa zaidi ya shilingi bilioni tatu. Wanaendelea na kazi ya kupaua na kupaka rangi ili vijana wetu wapate kazi ya ufundi na pia wapate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme umewaka katika vijiji vyote lakini vitongoji zaidi ya 200 havijapata umeme. Tunaomba katika eneo hili pia nguvu iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa ujumla wake tumepata shilingi 11,563,000,000. Pia, tumepata fedha ya *CSR* mwaka 2021 shilingi bilioni 5.7. Ninapozungumza, mwaka 2022/2023 miradi inaendelea ya zaidi ya shilingi bilioni tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeingia katika jimbo lile tangu mwaka 1995 mpaka 1996, vijiji vitano havikupata asilimia moja ya kutoka *Barrick North Mara*. Ninapozungumza, wamepata shilingi bilioni 6.8 ipo kwenye akaunti za vijiji na kazi inaendelea. Halmashauri yangu imepokea fedha kutoka Barrick kama kodi ya ushuru shilingi bilioni 21.7 lakini na wadau wengine ni shilingi bilioni 94. Ninawapongeza Barrick kwa uhusiano ambao wameutoa na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nilivyosema, nikizungumza habari ya miradi nahitaji masaa kadhaa kufanya kazi Tarime Vijijini. Sasa nataka nizungumze habari muhimu ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wa uchaguzi 2025 na ninataka vijana wanaodanganywa kule Mtwara na maeneo mengine na Waheshimiwa Wabunge, nataka niwape dawa ya wahuni. Dawa ya mhuni ni kuwa mhuni zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mtwara vijana wenu wamedanganywa sana, lakini vijana niwaambie, mimi nina uzoefu wa ndani ya Chama cha Mapinduzi, nina uzoefu wa hicho

chama kinachozurura mtaani. Kile siyo chama cha siasa, wale ni wanaharakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia muundo tu wa Chama cha Mapinduzi, hapa Mwenyekiti ni Mama Samia, amejaa kwenye kiti na chenchi inabaki, na kazi inasonga mbele. Amemchukua Makamu Mwenyekiti, mzee mwenye busara, hekima imetulia, Mzee Stephen Masatu Wasira, kijana wa Baba wa Taifa yuko pale ametulia. Maana yake ukiangalia Mheshimiwa Majaliwa ametulia pale, angalia Mheshimiwa Dkt. Dotto Biteko, angalia Waheshimiwa Mawaziri, angalia viongozi wa chama wa mikoa, wa-*NEC*, Makatibu na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ndiyo chama cha siasa. Ukitaka kujifunza uongozi, njoo Chama cha Mapinduzi; na ukitaka kufanya harakati, nenda vyama vingine, na utasubiri sana kuingia katika Ufalme wa Mungu, na kwa kweli utakuta mlango umefungwa. Kwa hiyo, vijana nawaambia, msidanganywe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia uchaguzi upo na utafanyika mwaka huu na hata sasa tunaye Mgombea mwenza Mheshimiwa Dkt. Nchimbi. Vijana wa Chama cha Mapinduzi wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Kwa mara ya kwanza Mwenyekiti wa Vijana Taifa kwa muda wa miaka 10 amepata fursa ya kuwa Makamu wa Rais wa Nchi hii. Mama Samia tunakuunga mkono sana, tunakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa zamani wa CCM na vijana wa sasa mjifunze, kwamba ukipata fursa ni kuchapa kazi ili upate fursa, tupate akina Nchimbi wengine na Mheshimiwa Nchimbi tutakuunga mkono kwa 200%. Kazi iendelee na Kazi na Utu, Tunasonga Mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama kimeshaleta mgombea mwenza, uchaguzi upo. Dkt. Nchimbi ametoa kauli ya kiongozi, "Uchaguzi upo." Tumetoa kauli mbiu, Kazi na Utu, tunasonga mbele na Mama Samia. Uchaguzi upo. Kama kuna mtu

anahangaika, wewe kama unataka kuwa Diwani changamkia CCM, vuta fomu, ratiba imetoka; kama unataka kuingia kwenye Bunge hili, rudi CCM, vuta fomu, uchaguzi ratiba imeshatoka, uchaguzi upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi tumeshafanya mabadiliko ya sheria hapa, lakini tumebadilisha daftari na mzunguko unaendelea. Maana yake uchaguzi upo. Vilevile, wale watu ambao wamefanya ziara kule kusini, Makamu Mwenyekiti, yule kijana, bwana mdogo ni muongo na mbinafsi. Nisikilizeni vizuri, muongo na mbinafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama akija kwenye Jimbo lako kiboko yake nipo. Yule nimemgonga 2008, nimemgonga 2015, nimemgonga 2020 na mwaka huu kichapo kiko pale pale. Mpango wa kumchapa unabaki pale pale. Huyu ni mtu ambaye alienda Sirari, na anajua kuna sheria ya kufanya biashara kwa mujibu wa sheria, anawaambia vijana, nendeni mfanye magendo. Walipokwenda wakakamatwa, wakanyang'anywa pikipiki, zikataifishwa. Hakuwasaidia, alisepa na alikula kona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ameenda kwenye Hifadhi ya Serengeti, anajua kuna sheria, anawaambia chukueni ng'ombe mkachunge hifadhini. Ng'ombe walikamatwa, watu wakaumia, alikula kona na hakuwasaidia. Huyu amekwenda *Barrick* pale *North* Mara, akawaambia vijana wa bodaboda tangulieni nakuja. Watu walikamatwa zikataifishwa pikipiki, watu wana kesi, alikula kona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni mbinafsi, nataka niwaambie, mliona juzi kuna nyumba inatembea inajengwa mpya. Huyu sio Mbunge, hafanyi biashara, ni mwana harakati, anamiliki maghorofa, anajenga nyumba mpya. Anachofanya pale Nyamongo, wale watu ambao wanakuwa na kesi, mgodi unafanya kazi nzuri, ukiona unataka kujitia hasara unafanya *bargaining* wazungumze, hapa wanaye mbia anaitwa Fatuma Karume, nina kesi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fatuma Karume ametengeneza *deal* na watu wa Nyamongo, wanajifanya kuwatetea watu wetu, wanakwenda Kanada kufungua kesi ya kuwatetea, wakikubaliana kuzungumza nje ya utaratibu kwenye meza, wanachukua 50% ya pesa, nao wanachukua 50%. Kwa hiyo, utaona wana magari mapya, watajenga nyumba, watafanya ziara, wanawaambia vijana kwamba wao ni viongozi. Hawa ni wanaharakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niwaambie, huyu ni mtu muongo, mbinafsi, ni matapeli wa kisiasa, msiwasikilize. Jambo la uongo likisemwa na mtu muongo, unalipuuza tu. Watanzania wajue, kazi imefanyika kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge hawa wa Chama cha Mapinduzi, miaka mitano iliyopita, kuna Wabunge walishtakiwa kwa wizi. Humu kuna mtu ameshtakiwa! Wabunge wote humu ndani ni safi kabisa, makada wa Chama cha Mapinduzi wanarudi kwenye Majimbo, ni watu wamefanya kazi kubwa, na katika uchaguzi ambao utakuwa ni mwepesi ndugu zangu, hawa watu wanakimbia mapambano. Wanajua ngoma hii tunaanua mapema. Hatuendi *halftime,* kwa sababu Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, mgombea wa Udiwani, ukienda kwenye eneo unafanya mkutano, unaomba kura kwa wananchi, huku wameegemea ukuta wa zahanati uliojengwa kupitia chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaenda kufanya mkutano, wamepanda kwenye treni ya *SGR*, imejengwa na Chama cha Mapinduzi; unakwenda kuomba watu kura, wako kwenye barabara ya lami, imejengwa na Chama cha Mapinduzi; unakwenda kuongea na wanafunzi, wapo kwenye jengo zuri, darasa, viti na meza ameleta Mama Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi ni mwepesi na mweupe kama karatasi. Kwa hiyo, ni lazima wakimbie. Tunasema Chama cha Mapinduzi ni kazi njema, ni chama, ni uongozi, chama cha kutoa ushuhuda kwa watu. Vijana ambao wanatafuta ajira, ajira inatengenezwa na Chama cha Mapinduzi, ajira haipo kwenye

harakati, njoo ujifunze uongozi, utafute fursa, tushirikiane kujenga nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya kutafuta uhuru kwa Tanganyia, alifanya Baba wa Taifa, kwa Zanzibar ni Abeid Amani Karume na akapoteza maisha, tumefunga mjadala. Kilichobaki hapa ni kujadiliana kwa heshima, hekima, kubadilisha baadhi ya mambo na tunasonga mbele. Taifa letu hili litasonga mbele, na huu ni mpango wa Mungu. Upinzani hapa ng'o, haupo! Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara. Nilimtaja Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Tarime Vijijini, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye bajeti ambayo tunakwenda kumalizia kuingia kwenye uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya nami nimeweza kusimama hapa kuchangia kwenye bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022 nchi yetu ilifanya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi. Nimekumbusha hili, nina jambo ambalo nataka nikumbushe kwa Serikali. Mkoa wa Tabora ni moja kati ya mikoa ambayo ina wakazi ama wananchi wengi. Ni Mkoa wa tatu kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema haya kwa sababu natambua kwamba, siku zote Serikali imekuwa ikifanya tathmini

na kuangalia maeneo yaliyo na watu wengi, ndipo palipokuwa panapelekwa pia rasilimali kulingana na watu waliopo kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwenye suala zima la afya. Mkoa wa Tabora tunayo Hospitali ya Mkoa inaitwa Hospitali ya Kitete. Hospitali hii kwa sasa haitufai wananchi wa Tabora kutokana na *population* iliyopo. Hospitali hii kwa mujibu wa wazee wetu, iko tangu kabla ya Vita ya Pili ya Dunia. Majengo mengi yaliyoko pale ni majengo ambayo yapo tangu wakati wa Vita ya Pili ya Dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo kwa *population* tuliyonayo katika Mkoa wetu wa Tabora, bado tuendelee kufanya Hospitali ile iendelee kuwa hospitali ya Mkoa. Kwanza, nyumba zimeshakuwa nyingi, majengo yameshazunguka, nafasi haitoshi hata ya kuweza kuongeza baadhi ya majengo ili hospitali ile iweze kufanana na hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali. Naiomba sana Serikali, kwa sababu Wilaya ya Tabora Mjini ina ujenzi wa hospitali ya Wilaya ambayo inaendelea, iko nje kidogo ya Mji wa Tabora, wananchi wanatamani hospitali ile ambayo ndiyo hospitali ya Mkoa ifanywe kuwa hospitali ya Wilaya ya Tabora na ile Hospitali ambayo inajenga kwa sasa ya Wilaya, waende wakaifanye iwe hospitali ya Mkoa ili wananchi wa Tabora waweze kunufaika na huduma za afya bora na siyo bora huduma.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa…

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu majengo yale mengi yamechakaa…

**MWENYEKITI:** Taarifa Dokta.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kumjulisha msemaji anayezungumza sasa hivi, ni kweli hali ya Hospitali ya Kitete ni mbaya. Ukienda kutembelea ile hospitali, iko kama kituo cha afya, majengo yale yamezeeka, hayafai. Kwa hiyo, hilo jambo analolizungumza Mheshimiwa Hawa naomba lizingatiwe sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa, unapokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara?

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili taarifa kutoka kwa *RAS* Mstaafu wa Tabora. Anaijua hospitali hii na ninachokizungumza anakielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kupitia Ofisi hii ya Waziri Mkuu kwa sababu ndiyo Serikali yenyewe, watubadilishie ile hospitali pale, wakaifanye iwe hospitali ya Wilaya sasa, na ile hospitali ya Wilaya ambayo inajengwa sasa iende ikawe hospitali ya Mkoa, iweze kuendana na wingi wa wananchi waliopo katika Mkoa wetu wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuweza kufanikisha kuongeza umeme kwa sasa kwa nchi yetu. Naipongeza sana Serikali kwa jambo hilo, nasi wananchi wa Tabora tunanufaika na umeme uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Tabora na hapa nazungumzia kwenye Halmashauri ambayo natokea, ambalo ni Jimbo la Tabora Mjini. Kukatika umeme katika Jimbo la Tabora Mjini na Mkoa mzima wa Tabora, imekuwa ni changamoto kubwa ya mara kwa mara. Huwezi ukaingia kwenye *group* la *TANESCO* Tabora kwa siku hujakuta malalamiko ya kukatika kwa umeme. Kama umeme umeshakuwa mwingi, wananchi wanahitaji kuona wanapata huduma hii kwa ufasaha na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, kwanza itubadilishie miundombinu kwa sababu hapa tatizo siyo upatikanaji wa umeme, tatizo ni miundombinu ya siku nyingi mibovu iliyopo katika Mkoa wetu. Hata hivyo, katika Jimbo la Tabora Mjini, wananchi wameshakuwa wengi, *transformer* moja iliyopo pale kwenye Halmashauri ya Tabora Mjini, haitoshi kutawanya umeme katika Manispaa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake kumekuwa na mgao wa kila mara kwa sababu hakuna umeme wa kutosha na hatuna *transformer* ambayo inaweza kubeba wananchi wote. Naiomba Serikali iende ikatuongezee *substation* nyingine pale na watuwekee *transformer* nyingine ili wananchi wa Tabora waweze kunufaika na umeme uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wa Tabora wamejiajiri kwenye mambo mengi ambayo yanahitaji huduma ya umeme. Kuna vijana ambao wanachomelea, lakini kuna akina mama wanauza samaki, akina baba wanauza dagaa, lakini kuna watu wanafanya biashara ndogo ndogo ambazo zinahitaji umeme, watu wana mikopo, watu wanahitaji kurejesha mikopo hii, kama umeme utakuwa haupo saa zote, hii ni changamoto na inasababisha wananchi wetu wa Tabora wasiweze kupata kipato kwa sababu ya kukatikakatika kwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba jambo hili katika bajeti ya hii watusaidie, watupelekee na watuongezee *transformer* nyingine pale ili wananchi wa Tabora waweze kunufaika na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala zima la mabonde yaliyopo nchini kwetu. Nchi yetu imebarikiwa mabonde mengi sana, hata hivyo mabonde haya hayatumiki ipasavyo kwa kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Tabora, ukianzia hapo Bahi – Singida – Tabora kuelekea Katavi – Kigoma kuja Shinyanga na Kahama yake, kuna mabonde mengi kweli kweli. Mabonde haya kama Serikali itaamua kuyaangalia na kuwekeza

kwenye mabonde haya, hususani kwenye kilimo cha mpunga, tutakuwa nchi ya kwanza kuilisha Afrika kwa mpunga utakaozalishwa hapa, kwa sababu haya mabonde yamekuwepo, hayana kazi yoyote, lakini ni vizuri kuwaelekeza wananchi na kuwaambia wahamie kwenye kilimo hiki cha mpunga na Serikali iweze kuwekeza, kutoa elimu kwa wananchi na iweze kuwasaidia kwenye masoko ili waweze kuuza nje mchele wetu ambao utazalishwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifanye utaratibu huu ili kuweza kusaidia vijana wengi waweze kujiajiri katika kilimo. Maeneo tunayo mengi, ni mazuri na yana maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora tumepata bahati ya kupata maji ya Ziwa Victoria, nampongeza sana Mheshimiwa Aweso, kwa kazi nzuri anayoifanya, na ndiye Waziri wa kwanza kuwepo kwenye Wizara hii, tangu ameingia kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni mwaka wa kumi sasa unakwenda, umekuwa Naibu Waziri na sasa amekuwa Waziri. Mheshimiwa Aweso, nikupongeze sana kwa kazi nzuri ambayo unafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora maji yamefika, lakini bado kuna baadhi ya maeneo ya Tabora Mjini hususan kwenye Kata za pembezoni, bado hawapati haya maji. Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri, angalia jambo hili, wananchi wetu waweze kupata maji na waweze kunufaika na mradi wa Ziwa Victoria kwa kupeleka miundombinu yakiwemo mabomba ili wananchi hawa waweze kunufaika na maji haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, mwezi Oktoba mwaka huu nchi yetu inakwenda kuingia kwenye Uchaguzi Mkuu. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, pamoja na Watanzania kwa ujumla, kila mmoja kwa dini yake na kwa imani yake, tumwombe Mwenyezi Mungu aweze kutujalia na kutusaidia tuingie kwenye uchaguzi tukiwa Watanzania wamoja, tumalize tukiwa Watanzania na tuweze kuwa pamoja mpaka wakati tunaendelea kuiendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kumwombea Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyezi Mungu amjalie afya njema, amjalie hekima wakati tunaelekea kwenye zoezi hili gumu, lakini tunaamini Mwenyezi Mungu atampa hekima na busara ya kuweza kutufikisha pale ambapo Watanzania wote tunapatarajia.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu mbariki Mheshimiwa Rais wetu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga. Nilimtaja Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mheshimiwa Janejelly James Ntate na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, wajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka wa tano tunakwenda kuingia kwenye uchaguzi mwingine. Tumekuwa tukiomba sana hapa Bungeni kila siku tukisimama na kwa kweli imefika wakati pia tutoe shukrani za dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu za kwanza, mimi kwanza nampelekea Mwenyezi Mungu. Namshukuru sana Mungu kwa ajili ya Taifa letu la Tanzania na kwa ajili ya ulinzi ambao anaufanya kwenye nchi yetu na namna ambavyo anatusaidia. Namshukuru sana Mungu kwa ajili ya viongozi wetu ambao ametupatia katika Taifa letu, tukianza na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote ambao tuko nao, pamoja na viongozi wote wa Serikali Kuu, Wakuu wa Mikoa, Ma-*DC* pamoja na wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu mambo yanayoendelea kwenye nchi yetu, yanatia moyo, yanatupatia faraja na yanaonesha kabisa nchi yetu itaendelea kuwepo. Yapo Mataifa mengine na nafikiri wale wanaochezacheza kwenye

mitandao wanaona. Wapo watu wanasema ni laana kuzaliwa katika nchi zao, lakini sisi Watanzania tuna kila sababu ya kumwambia Mungu tunakushukuru, na ni baraka kuzaliwa katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Serikali kwa uwekezaji mkubwa walioufanya kwenye miundombinu. Hii ndiyo inatupatia mwelekeo wa Taifa letu linaelekea wapi? Uwekezaji mkubwa uliofanyika kwenye miundombinu katika Taifa letu, tukianza kwenye miundombinu ya usafirishaji, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametusomea taarifa yake hapa, pia sisi wenyewe tumeona kwa macho, na tumetumia miundombinu hiyo. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuisimamia na kuhakikisha tunafika tulipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imeingia madarakani wakati tumetoka kwenye mtikisiko, bado wameweza kushika usukani na kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa imara, yale tuliyojipangia yameendelea mpaka tumefika leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia uwekezaji mkubwa, watu wote tulikuwa tunafikiria, hivi tunakwendaje? Wote hapa sisi ni watu wazima, fikiria tu nyumbani mpo watu wawili, akatokea mmoja akafariki, au baba akafariki, namna ambavyo unayumba kujikusanya kusanya ili uendelee kuiendesha familia; au mama amefariki, baba atakavyoyumbayumba kuiendesha familia. Hata hivyo, sisi tumeondokewa na Rais ambaye alikuwa ni dereva, na bado tumechukua nchi, tumetulia, miradi yote imekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu, na kuwashukuru viongozi wetu kwa moyo wao wa dhati wa kuipenda nchi yetu na kujitoa kuitumikia Tanzania. Tunawashukuru kwa ajili ya kukamilisha Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais anakabidhiwa nchi hii ya Tanzania au nchi zilizo nchi za Afrika zilizo nyingi. Unakabidhiwa watu, unakabidhiwa na bajeti na mipango, haukabidhiwi fedha

kwamba, fedha hii ndiyo ya kufanyia mambo hayo uliyopewa uyatekeleze. Wewe utajua mwenyewe kwamba unakwenda kutafuta wapi? Rais anaanza kuhangaika na ndiyo inapotokea *issue* inayoitwa *cash budget,* ukakusanye ndipo uendeshe nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni jambo ambalo linahitaji kiongozi mwenye moyo, kiongozi mwenye uzalendo na upendo mkubwa kwa watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru sana mmetumalizia Bwawa la Mwalimu Nyerere *(megawatt 2115)* kwa trilioni 6.6. Vilevile, mmetujengea *SGR* ambayo kwa *level* iliyofika ni zaidi ya trilioni 10 zimetumika. Bado tumekwenda kuboresha afya kwenye nchi hii. Kwa kiasi kikubwa sana hakuna jimbo hapa ambalo halijapewa vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya vituo 1,300 vimejengwa kwenye nchi yetu, lakini zahanati zimejengwa za kutosha. Umefanyika uboreshaji mkubwa kwenye hospitali za Halmashauri ikiwepo Hospitali yangu ya Iringa (*Frelimo)*. Kwa miaka 15 ilikuwa imepelekewa shilingi milioni 400 tu, lakini ndani ya miaka hii minne tumepewa zaidi ya shilingi 3,550,000,000. Hivi ni vitu vya kuvipongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tumeboresha huduma za elimu kuanzia awali. Tumeelezwa hapa ni kiasi gani, tumetumia zaidi ya shilingi trilioni 1.2 kwenye elimu ya msingi, kwenye sekondari kwa miradi ya *BOOST* na *SEQUIP* kwa ajili ya kujenga shule mpya kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iringa tu pale shule za sekondari nne, shule za msingi ambazo zimejengwa nne mpya kabisa. Vilevile, madarasa ya kutosha. Sasa hivi kila mahali kuna madarasa yanabaki. Watoto walikuwa wakienda darasani wanakaa wengi, wengine wanasubiri na wanaotakiwa kuanza Januari wanakuja mwezi Machi. Hata hivyo, hicho kitu sasa hivi kwenye nchi yetu imekuwa historia. Tunaishukuru sana Serikali yetu na viongozi wetu kwa kuyasimamia haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo yanasababisha sasa mnaendelea kuheshimisha Chama Cha Mapinduzi, na sisi makada tunajisikia vizuri sana kwa sababu ya utekelezaji ambao umefanyika kwenye usafirishaji. Hii inaonesha ni namna gani nchi yetu inatoka hatua moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ununuzi wa ndege sita za abiria pamoja na ndege moja ya mizigo, uwekezaji wa shilingi trilioni 1.49, kuliimarisha lile Shirika. Shirika lile lilikuwa linasafirisha abiria 850,000, mpaka sasa abiria milioni tatu wanasafiri kupitia ndege za Tanzania. Mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 250 mpaka shilingi trilioni 1.5. Unataka kutuambia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo uwekezaji uliofanyika kwenye shirika la ndege kwenye nchi yetu, lazima tumshukuru Mungu na tuwashukuru sana viongozi wetu. Sisi tunaendelea kuwaombea. Kwenye liturjia zetu Makanisani ndiyo maana tumeweka kipengele cha kuwaombea viongozi wa Taifa letu likianzia na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizi, yapo mengi ambayo tungesema. Mikopo ya wanafunzi wetu wa elimu ya juu, zamani walikuwa wanapewa fedha shilingi 7,000, wamepewa mpaka shilingi 10,000/= tumeongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe Iringa pale, wanafunzi wangu wa vyuo vikuu vinne; tuna *MUCE* pale, tuna Chuo cha *Roman Catholic (RUCO),* tuna Chuo cha Iringa, tuna vyuo vya kati, *CDTI* kiko pale Ruaha, tumeletewa fedha vimeboreshwa kiasi cha kutosha, watoto wamekopeshwa, bado watoto wanaendelea kusoma. Tuna kila sababu za kumshukuru Mungu.

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa kengele inagonga, niende moja kwa moja kwenye hoja. Tunakoelekea sasa, kwa kuwa, tumefanya mambo makubwa, naomba sana tuwalinde vijana wa Taifa letu. Hii ndiyo

nguvu kazi ya *future* ya Taifa letu. Tunaomba vijana wafanyiwe uwekezaji kama ambavyo taarifa inaeleza. Sasa wafundishwe mambo ya maadili, wafundishwe mambo ya kujitambua na vijana wetu wawekezwe kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana machinga wangu pale Iringa na wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wengi ni vijana. Wale waliahidiwa kupewa shilingi milioni 700 na Mama alipokuja mwaka 2022, najua muda bado haujaisha, mpaka mwezi wa Sita tunaendelea kutekeleza hii bajeti, hilo nalo liangaliwe, ili uwezeshaji kwa vijana uwe mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakoelekea jamani, kikitolewa, hata kama ni kama ifuatavyo, shilingi trilioni moja paap, kipelekwe kwa vijana, tukachakachue uchumi wa hawa, siyo tu kuwaanzishia, lakini hata wale wanaofanya, kama wako kwenye kilimo, kwenye ufugaji, kwenye ufundi, tupeleke. Tumwezeshe huyu kutoka kwenye ufundi, tumsaidie *skills* na pia tumsaidie *capital.* hawa ndiyo future ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana walindwe, wapewe elimu ya kutosha, vijana wetu ndiyo wanaoathirika kiasi kikubwa na maambukizi ya UKIMWI na mimi sijajua hapa ni watoto au vijana? Maana ukisema kuanzia miaka 15 mpaka 24, miaka 15 mimi najua bado ni watoto. Kisheria, kuanzia miaka 18 ndiyo kijana, lakini leo watoto wetu kuanzia miaka 15 – 25 wameathirika. Tumeambiwa hapa kwenye Taarifa ya Waziri Mkuu, kwa mwaka watu 60,000 wanaambukizwa maambukizi mapya ya *HIV*, lakini 34% ni vijana. Vijana wanalindwa vipi jamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuwaangalie, watoto wetu hawa ndio ambao wengi wanaathirika kwenye pombe, na hili naomba nilielezee. Pombe zipo, lakini zipo pombe zilizochafuliwa. Nchi hii watu wengi wanakunywa pombe zilizochafuliwa, pombe ambazo hazijapimwa kitaalamu, na jana aliongelea hapa Mheshimiwa Neema, hii yote ni kukosa chombo madhubuti ambacho kinasimamia usalama wa chakula kwenye nchi hii. Watu wanatengeneza pombe wanavyotaka wao, naomba hili tuliangalie ili tuwalinde vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niliomba hapa Baraza la Afya ya Akili. Ndugu zangu, viongozi wangu, naomba Baraza la Afya la Akili liundwe, watu wahudumiwe kwenye akili zao. Msione watu wanafanya vituko kwenye nchi hii, siyo kitu rahisi mtu kwenda kumpiga ngumi Mwenezi Taifa, mwanamke. Mambo haya kwenye akili tayari tumepinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu ambao walikataa isiandikwe Katiba Mpya, hao hao waliongoza mapambano ya kutoandika Katiba Mpya; hao hao leo ndio wanarudi wanaongoza mapambano ya kutuhumu, lazima tuandike Katiba Mpya, wakati wao ndio waliopinga. Tumeanzisha mchakato wa kuandika Katiba Mpya hapa, wakaanzisha kundi linaitwa UKAWA, wakapinga uendelezaji wa ile Katiba, mchakato ukaisha. Leo anatoka nje anapambana kama vile kuna mtu fulani alizuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awaambie Watanzania, yeye ndio aliyeanzisha ajenda ya kuzuia Katiba na yote yanayodaiwa mle kwenye Katiba yalikuwa yameingia kwenye Katiba inayopendekezwa. Jambo ambalo halikuwepo ni moja tu, la Serikali tatu, mengine yote yaliingia, kelele hizi huku nje za nini? Jamani baraza la afya ya akili lianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa hapa kuhusu uwekezaji wa bandari. Watu walitupinga, walitutukana, walifanya vitu vya ovyo, lakini tumeambiwa namna ambavyo bandari yetu imeongeza mapato, jinsi ambavyo makontena na siku za meli kukaa bandarini zimepungua. Saa za kuhudumia meli za mafuta zimepungua kiasi kwamba, watu hawalipi tozo kubwa. Kwa hiyo, ndiyo maana sasa hivi, tunaona kuna utulivu wa mfumuko wa bei kwenye bidhaa, lakini hawa ndiyo walioongoza mapambano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndio waliobeza miradi mikubwa ya kichumi ikiwepo umeme na *SGR*, lakini hawa ndio leo wanawageuka Watanzania wanawaambia vitu ambavyo havipo. Jamani tuanzishe baraza la afya ya akili nchini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Janejelly James Ntate.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata wasaa huu, lakini niendelee kumshukuru kwa kutulinda miaka yote hii mitano. Hakika haikuwa kwa akili zetu au kwa busara zetu, bali ni kwa mkono wa Bwana ulitufunika. Kuna tulioanza nao, leo hii hatukonao. Sisi ni nani? Kwa nini, tusimrudishie heshima na utukufu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi aliyofanya kwa watumishi wa Tanzania. Mimi nikiamka ni watumishi; watumishi na mimi, lakini nalipongeza Baraza la Mawaziri, wametekeleza maono ya Mheshimiwa Rais, hasa wale ambao walipita Wizara ya Utumishi na Wizara ya Kazi, maana hao ndio nimefanyanao kazi kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye uzalishaji wa ajira. Naishukuru sana Serikali, kuanzia mwaka 2020 – 2025 wamezalisha ajira 8,084,204, siyo kazi ndogo na ilikuwa ni ahadi, wameitekeleza. Niwashauri, hizi wamezalisha kutoka kwenye mikakati ya miradi ambayo wameiendeleza, lakini kuna sehemu ambayo tunaisahau. Tunaweza tukapata ajira za vijana za kudumu; kuna mifuko kadhaa ya vijana, hapa kuna 10% ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape mfano ndani ya Temeke. Manispaa ya Temeke tulichukua madaktari bingwa watano tukawapa mkopo wa 10%, shilingi milioni 250, wakaanzisha *polyclinic*. *Clinic* hiyo sasa hivi ina watumishi 20. Ina maana wameshaajiri vijana wenzao ambao ni wa fani ya uuguzi, na wameajiri na ambao sio wa fani ya uuguzi, na hapo ni kipindi cha

miaka mitatu. Hawa wakifika miaka kumi watakuwa tayari wameajiri vijana wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende tufanye hivyo na hii mifuko, tufanye hivyo na hii 10%, kwa kutafuta wale vijana waliomaliza vyuo, lakini hawana ajira. Waunde vikundi kwa pamoja, tunasema vikundi vitano ni vigumu, lakini tukiwaunda wenye *profession* moja, tukawapa hizi fedha, wataweza kufanya kwa sababu, ndege wenye kufanana, wenye bawa moja, huruka pamoja. Twende kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naipongeza Serikali kwa jinsi ilivyoboresha sehemu za utumishi, hasa Mji wa Mtumba, umekuwa ni kioo na kielelezo. Mtumishi ukishamweka kwenye nafasi ambayo ni nzuri, atafanya kazi vizuri, lakini hapo pamoja na kuboresha yote, pamoja na juhudi zote zinazofanywa na na Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mawaziri mnaohusika kutekeleza maono yake, niwaombe mshuke chini mwendelee kusimamia, bado watekelezaji wa chini wanawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya ziara zangu, nitawapa mfano. Kuna sehemu moja Kanda ya Ziwa, siyo vizuri kutaja majina, lakini kuna uhamisho, wanamhamisha mtumishi, wanachukua kanuni ya utumishi wa *transfer* ya ndani, lakini tuangalie jiografia zetu. Kuna wilaya nyingine kutoka kata moja kwenda nyingine ni kilomita 70 mpaka 80, mtumishi huyu aliyehamishwa anatembea kwenye ziwa saa nane kutoka kwenye kituo alichohamishwa kwenda kituo kingine. Barua inamwambia kabla ya siku nne uwe umeripoti, lakini kanuni inasema siku 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi huyo unamwambia ni uhamisho wa ndani, hatakiwi kulipwa. Sasa hiyo inasababisha watumishi wanaingia mikopo ambayo Mheshimiwa Njau amekuwa akiipigia kelele, akope ili aende kujikimu. Namwomba Waziri wa Utumishi na Waziri wa Kazi, hebu waliangalie hili, kwani huko chini kidogo hapajaenda vizuri, pamoja na juhudi kubwa sana ambazo zimefanyika hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishukuru Serikali, wameboresha Sheria ya Taasisi ya kazi ya mahusiano kazini, Sura Namba 300. Wameboresha Sheria ya Ajira za Wageni, Sura Namba 436.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sheria ni nzuri na wameboresha, lakini sasa mimi niseme, pale walipoboresha nawapongeza, hasa kwa sheria ya likizo. Wabunge tuliongea humu na mliniunga mkono, nawashukuru sana Wabunge, ili wanaozaa watoto njiti wapewe likizo ya kutosha. Nakumbuka siku hiyo baada ya kuongea, namshukuru sana Waziri wa Utumishi, alinipeleka kwa wataalamu wake nieleze ninachokiongea ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamenielewa na wameenda kubadilisha, lakini sasa hapo naomba waweke maboresho kidogo, hata huyu mwenza wake anayemhudumia, basi naye aongezewe likizo kidogo ya kumhudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine sasa, twende kwenye taasisi. Kwa Serikali mtafanya, lakini kwenye taasisi binafsi bado ni pagumu. Mtumishi akijifungua mtoto njiti, wakati mwingine anaambiwa uache kazi ama uje. Kwa hiyo, miezi ya kawaida inayosemekana ya siku 36 au uache kazi uende ukamhudumie huyo mtoto wako. Sasa, sheria ni msumeno, mmeitunga iende ikaangalie na taasisi binafsi, ili hawa watumishi sasa waweze kufaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mmerekebisha Sheria ya Ajira za Kigeni. Nawashukuru sana, lakini bado tuna la kuangalia. Mimi sielewi pale Kariakoo, Mchina anayetembea na *t-shirt*, anayetembea na viatu mkononi, ameingiaingiaje, nanyi mmebadilisha hii sheria! Kibali ametoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende tuangalie wataalamu wetu wanaotoa vibali. Tunaweza tukawa na sheria nzuri, lakini kule kwenye utekelezaji je, kuko salama? Kuko sawasawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeunda elektroniki ya kusuluhisha migogoro ya kazi, nawapongeza sana. Sasa hivi

mashauri yamepungua, mashauri hayachukui miaka, kwa hiyo, watumishi hawapati ile *frustration*, lakini mahusiano mliyojenga na vyama vya wafanyakazi mimi hapa nawapongeza sana, ingawa kuna mtu mmoja kama alivyosema, ianzishwe taasisi ya afya za akili, yuko sawa, anasema ninyi vyama vya wafanyakazi, kwa nini msigome? Hivi wagome kwa nini wakati kuna *4Rs*? Wanakaa na Serikali, mambo yanaenda. Wagome kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, anataka kushinikiza watumishi wagome. Watumishi wa Tanzania hawagomi, watakuwa wanajadiliana na Serikali kupitia vyama vyao na mahusiano haya yamekuwa makubwa sana. Tumekuwa tukiona kwenye Mei Mosi jinsi Serikali inavyoshirikiana na vyama vya wafanyakazi na kufanya shughuli zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie tu, mtumishi naye ni raia, anaingia nyumbani baada ya saa za kazi. Kulikuwa na zoezi la uandikishaji wa daftari, nilipita kwenye Ofisi za Serikali nikihamasisha, lakini rafiki zetu wale wakaanza kuniandika kwenye mitandao kwamba, napeleka siasa kwenye Ofisi za Serikali. Sasa mimi nikashangaa, Mtumishi wa Serikali Katiba ya nchi inampa haki ya kupiga na kupigiwa kura, lakini kwa sababu mtumishi wa Serikali hajaamua kuja upande huu, inampa haki ya kupiga kura na kumchagua kiongozi amtakaye ili aweke dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nasema rasmi ndani ya Bunge, ninapolindwa, wafanyakazi wanasema hivi, unayetafuta naye kuni ndiye unayeota naye moto. Wametafuta kuni na Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya mambo mengi kwa watumishi, kwa hiyo, kura zao ziko barabara kwa Dkt. Samia na hili hawapepesi macho, watafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *OSHA*. Jamani mtu akifanya vyema mpe maua yake, Mkurugenzi wa *OSHA*, Bi. Khadija, ni msikivu, ni mnyenyekevu. Nilivyochangia mara ya kwanza hapa 2020 nilimwambia ukaguzi wa kwenye migodi na viwanda, lakini leo hii amekuja, wamekagua kwenye migodi, wamekagua migodi 13,003 kwenye kukagua usalama wa kazi

pale. Kwa hiyo, Serikali mmefanya, mmeweza kuingia kwenye migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migodi ilikuwa haiingiliwi, viwanda vilikuwa havikaguliwi, lakini huyu mama katafuna mfupa uliomshinda fisi na mmetoa elimu kwa waajiri na waajiriwa. Hapa tu nawaomba, hii namba iliyofanyiwa kazi haitoshi, bado kunahitaji kufanywa elimu ya kutosha ili watumishi waelewe wanafanya nini, na mwajiri aelewe anafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imepima afya za watumishi. Kuna vifo vilikuwa vinatokea, ni kwa sababu ya kutofanyiwa upimaji wa afya. Sasa hii iendelee kwa sababu, hapa mlivyopima na kufanya ushauri mliona ambao wana matatizo na changamoto za kiafya ni 122,000, hii siyo namba ndogo. Mkiendelea kufanya na mkaanza kuwafundisha hawa namna ya kujihudumia tunaweza tukaendelea na nguvu kazi yetu bila kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Mfuko wa *NSSF*. Nawapongeza Wizara ya Kazi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, mfuko saa hizi umekuwa na uhai, mfuko sasa hivi umeweza kulipa kwa wakati, ila bado kuna ukwamishaji. Kama Waziri wa Utumishi alivyokuwa ananijibu swali juzi, hizi *data* zisomane. Haipendezi mtumishi kuombwa *documents* za kustaafu wakati ninyi ndio mliniajiri. Mziandae *documents* zangu, mnaponipa barua ya miezi sita kustaafu muwe mmepeleka *documents* zangu na cheo cha mwisho, muwe mmepeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanalipwa, lakini cheo cha mwisho hakiangaliwi wakati ndiyo kinachofanya ukokotozi. Ni kwa sababu, tunapopiga kelele hapa wanakimbia, wanampa cheo leo wakati wanajua Julai anastaafu. Hicho cheo kitakuwa chini ya miezi sita, hawezi kufanyiwa *calculations* kwa cheo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nawapongeza, niwatakie uchaguzi mwema. Tarehe moja tumeambiwa tukachukue fomu, niwaombee kwa Mungu ili atujalie wote turudi ndani ya Bunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Janejelly Ntate. Tunamalizia na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ya Waziri Mkuu, kwa ajili ya Bajeti ya Mwaka 2025/2026 ambayo kimsingi ni bajeti ya mwisho katika kipindi cha miaka mitano ya uchaguzi toka 2020 ambayo tunaenda kuimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyetujalia uzima kukutana leo katika Bunge lako Tukufu. Kama ambavyo tumekuwa tukisema siku zote, tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais ambaye kwa kweli, ameendelea kutuongoza vizuri katika uongozi wake wa miaka minne hii. Tumeona mapinduzi makubwa ya kimaendeleo na hali hiyo tumeiona katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ameeleza mambo makubwa yaliyofanyika katika mwaka wa fedha tunaoenda kuumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa, ameweka alama kubwa katika nchi yetu, nasi Wabunge ambao tunatoka kwenye majimbo ni mashahidi kwa sababu, tumeona namna ambavyo fedha nyingi zimekuja na kumekuwa na mabadiliko makubwa ya kihuduma na zaidi katika kuhakikisha kwamba, tunafanya shughuli za uzalishaji ambazo leo zinaleta maendeleo makubwa yakiwemo uchumi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, ambaye ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni. Kwa hakika kupitia hotuba yake na kazi ambazo amezifanya kwa muda wa miaka hii yote mitano, amefanya kazi kubwa ya kuisimamia Serikali. Kwa hakika sisi kama Wabunge, tunaona namna ambavyo amekuwa akitupa ushirikiano kupitia Mawaziri ambao amekuwa akiwasimamia. Kwa hili Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakupongeza sana na tunakutakia kila la heri kule Ruangwa, Mungu akujalie uweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia wasaidizi wake Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete kwa namna ambavyo wanamsaidia, pamoja na Manaibu na Makatibu wake Wakuu katika Wizara hii ambayo ni Wizara mhimili katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani na pongezi hizo, nichukue nafasi hii kuendelea kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki kwa namna ambavyo wamenipa ushirikiano kwa miaka hii mitano. Tumefanya kazi kwa pamoja ambayo leo inaleta matokeo makubwa na machache nitayaeleza wakati naendelea kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikiliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitagusa maeneo machache sana. La kwanza ambalo nitaweza kulirejea ni suala la bandari yetu ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam tumekuwa tukiisemea hapa Bungeni kwa sababu ni kitovu cha uchumi wa nchi yetu, na kwa hakika katika muda wa miaka hii miwili, *almost* tumeweza kufanya mapinduzi makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tulipoleta hoja za kuwekeza katika bandari yetu, kuna baadhi walitupinga, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema, ni kwa sababu, kulikuwa na upotoshaji mkubwa. Leo tunavyoongea, Bandari ya Dar es Salaam tuliboresha sana ile ghati namba sifuri mpaka saba ambayo kimsingi imeweza kuongeza uwezo wa kupakua makasha na kuyatoa pale bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka ule katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025 tulikuwa tuna uwezo wa kutoa yale makasha 670,000, lakini leo tunaweza kushusha makasha 685,000 kwa pamoja na kwa haraka. Ni jambo kubwa ambalo limefanyika katika bandari yetu na katika kipindi hicho pia, tumeweza katika hayo magati ambayo yameboreshwa tumeweza kushusha makasha 122,000, lakini sasa tunaweza kushusha makasha 160,000, kitu ambacho huko nyuma kilikuwa hakipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, sasa zile meli ambazo zinashusha makasha hazisubiri gatini, zinaenda moja kwa moja kushusha. Maana yake ni kwamba tumepunguza kabisa muda wa ushushaji wa makasha ambao ilikuwa ni kero katika Bandari yetu ya Dar es Salaam na ilikuwa inatupotezea wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyoongea, tumetoka siku 46 tumeenda mpaka siku saba na mapato yameongezeka kutoka shilingi trilioni 9.35, sasa ni shilingi trilioni 9.86. Ni mambo makubwa, na unaposikia mapato yameongezeka maana yake ni uwezo wa Serikali kuhudumia watu wake. Ndiyo maana leo tunaongelea habari ya baadhi ya miradi kwamba imefanyika vizuri kwa sababu, tumekuwa na uwezo mkubwa wa fedha kupitia mapato ya *TRA* na kupitia mapato mengine yanayokusanywa na watu wa *TPA*, ambao wanafanya kazi kubwa pale bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme, Watanzania tuendelee kuwapima wanasiasa. Mtu anapotoka anakosa hoja ya msingi, anazunguka kuwaambia nchi nzima kwamba, bandari zote nchi hii zimeuzwa, halafu wakati huo bandari tulizonazo zinaendelea kutuzalishia mapato na bado Sheria ya Mwaka 2007 ya kuanzishwa *TPA* inatambua *TPA* ndiyo inasimamia bandari zote za nchi yetu. Kwa hiyo, mtu akikosa hoja, asipotoshe Watanzania na kwa sababu, unaendelea kupotosha wanakujua wewe akili yako imekalia upande gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niwaombe sana Watanzania waendelee kutupima tunapoongelea suala la maendeleo ya nchi yetu, na hili Mheshimiwa Rais hakusikiliza kelele yoyote, aliamua ku-*focus* kwenye malengo ya nchi yetu na bahati nzuri tumefanikiwa. Leo ndiyo maana tunaona Bandari ya Dar es Salaam imekuwa kimbilio na wateja wetu wanakuja kushushia mizigo yao hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa inaendelea kufanywa *SGR* na kuhakikisha kwamba, tunakuwa na bandari kavu, itasaidia kuondoa msongamano wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, ndiyo kazi ambayo inafanywa. Naamini ipo kwenye Kamati ya

Miundombinu, tumeendelea kuishauri Serikali iendelee kufanya kazi hiyo nzuri ambayo inaendelea kutuongezea heshima kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la miundombinu na baadhi ya shughuli mbalimbali za uchumi, ninaamini kabisa Serikali itaendelea kufanyia kazi mawazo yetu ambayo tumeendelea kuyatoa, lakini kwenye eneo hili tuzungumzie suala eneo la huduma. Huduma zimeendelea kuboreshwa, ikiwemo huduma ya afya. Tumeona kazi kubwa imefanyika kuboresha eneo la huduma ya mama na mtoto, tumepunguza vifo vya mama na mtoto. Hii kazi imewezekana kwa sababu tumejenga vituo vya afya, tumejenga zahanati, tumejenga na hospitali zetu za wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, ukienda pale kwenye Wilaya yetu ya Ikungi, Jimbo la Singida Mashariki, tumejenga kituo cha afya, tumejenga zahanati na tumejenga hospitali ya wilaya ambayo leo inaweza kuhudumia wananchi wetu ambao huko nyuma walikuwa wanaenda mbali. Kama haitoshi, vifaatiba vimewekwa pale katika hospitali ile, lakini leo tunavyoongea kumekuwa na chumba maalum cha upasuaji, kina vifaa vyote ambavyo kimsingi vinaenda kuwasaidia wananchi wetu katika kutoa huduma mbalimbali ikiwemo huduma za afua na mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kuomba, Musuhaa tumeomba tupate kituo cha afya, tumeomba Mang'onyi pamoja na Isuna. Katibu Mkuu alikuja pale akaahidi, ninaomba sana Serikali itusaidie kujenga vituo vile vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni maji. Huko nyuma kulikuwa kuna changamoto, tulikuwa tunapata 47% ya utoaji wa maji. Leo tunavyoongea baada ya miradi mbalimbali, pamoja na uchimbaji wa visima, tumeweza kufanikiwa. Minyinga tumepata maji, Sakaa, Mbwanjiki, Mang'onyi pamoja na Mkunguwakiendo mambo yanabadilika. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kuendelea kutusaidia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie suala la mafao. Wananchi wetu, viongozi wetu waliostaafu, hasa wale wa Jeshi la Wananchi ambao wako kwenye jimbo langu wameendelea kuwa wanaomba sana walipwe mafao yao kupitia hiyo. Tunaye mzee wetu ambaye anaitwa Homboyi, alistaafu jeshi katika Kambi ya 501KJ, yeye na wenzake wanaomba waweze kulipwa mafao kwa sababu, wamefanya kazi kubwa ya uzalendo, waendelee kuweza kuilinda nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ili tuweze kwenda kutekeleza miradi ya maendeleo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi ya leo, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu. Waheshimiwa Wabunge nitawataja wachangiaji ambao wataanza kuchangia jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay. Tutaanza na hao, halafu tutaendelea na wengine.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niwatakie mchana mwema. Nasitisha Shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Bunge lilirejea Saa 11.00 Jioni)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Nilimtaja Mheshimiwa Jackson Kiswaga na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, atafuatia.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza jioni ya leo. Kwanza, nianze kwa kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu mpendwa kabisa anayefanya kazi za kipekee sana katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nawaambia ndugu zangu pale Iringa kwamba kuna Watanzania wawili ambao walipewa wosia wa umma wakati Mheshimiwa Dkt. Magufuli anaondoka. Wosia wa kwanza alipewa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan akaambiwa kwamba, naona kuna dalili kwamba malaika wananiita, lakini naomba kazi zote ambazo nilizianza, mwenzangu ukazimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wosia wa pili nilipewa mimi pale Iringa. Mheshimiwa Dkt. Magufuli alivyokuja akawaambia watu wa Kalenga kwamba, nileteeni Kiswaga akaswage maendeleo. Alizungumza jambo hili mara mbili. Kwa hiyo, tuanze na Rais, kwa kweli ametekeleza huu wosia vizuri sana. Tumeona kazi kubwa ambazo Mheshimiwa Dkt. Magufuli aliziacha zinakwenda vizuri. Tukianza na bwawa la umeme, amelimalizia, na reli sasa hivi tunapanda; na mambo mengi makubwa ya kimapinduzi ambayo yanafanyika katika Taifa hili la Tanzania. Tunampongeza sana kwa hizo kazi kubwa ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kalenga ni namna gani nimeswaga maendeleo baada ya kupokea ule wosia? Fedha nyingi zimepokelewa katika Jimbo la Kalenga. Tukianzia pale halmashauri, takribani shilingi bilioni 20 tumezipokea, hiyo ni halmashauri peke yake, ambapo tumezitumia kwa namna hii. Kwanza, tumejenga shule za sekondari mpya nne ambapo moja inaendelea kujengwa hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga jumla ya vyumba vya madarasa 155, hivi ni vya sekondari pamoja na shule ya msingi. Matundu ya vyoo tumejenga 902, tumejenga nyumba tano za walimu na pia tumekamilisha kujenga ofisi ya halmashauri; na mambo mengi yaliyofanyika hapa jumla ya takribani shilingi bilioni 20 zimetumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye masuala ya afya, nako tumejenga vituo vya afya vitatu. Tulikuwa na vituo vya afya vitatu na sasa tumeongeza vituo vingine vitatu kufanya 100% ya nyongeza ya vituo vya afya, na sasa Serikali italeta kituo kingine kimoja, hivyo tutakuwa na vituo vya afya vinne ambavyo vimejengwa katika Jimbo la Kalenga ambayo ni sawa na 125% ya vituo vilivyopo. Pia tumekamilisha ujenzi wa zahanati 14. Hiyo ndiyo namna ambavyo nimefanikiwa kuswaga maendeleo kama nilivyoachiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa maji, tumepokea takribani shilingi bilioni nane ambazo zinatekeleza miradi mbalimbali. Pia, tumepokea magari mawili ya wagonjwa na tunaendelea na mambo mengine. Kwa mfano, kwenye skimu za umwagiliaji, hivi karibuni tumesaini skimu ya umwagiliaji ya shilingi bilioni 13 ambayo inakwenda kutekeleza Skimu ya Mangalali, na tarehe 17 mkandarasi atakabidhiwa. Tumeweza pia kukarabati skimu nyingine kama ya Ipwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunakwenda kujenga mabwawa na tayari fedha tumeshapewa. Tutajenga Bwawa la Magubike na tunakwenda kusanifu Mabwawa ya Mgama, Makota na maeneo yote hayo tunakwenda kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, kazi nyingi zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye Barabara, upande wa *TARURA* tumefungua barabara mpya nyingi na za kutosha. Kwa hiyo, jimbo zima sasa linapitika. Ukiacha changamoto ndogondogo za mvua zilizojitokeza lakini barabara tumezifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye *TANROAD,* tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, barabara tatu zinajengwa katika Jimbo la Kalenga. Barabara ya kutoka Wenda kwenda Mgama shilingi bilioni 19 tunakwenda kuimalizia. Nina mazungumzo na Mheshimiwa Mchengerwa hapa, pengine tuiite Kiswaga halafu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia tutamwita kwenye zile kubwa kubwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nyingine ya kilometa 22 ambayo inajengwa kutoka Iringa kwenda Kilolo, na kuna nyingine ambayo mimi na kaka yangu Lukuvi tunashirikiana, barabara ambayo imesubiriwa tangu wakati wa Mwalimu Nyerere, barabara ya kutoka Iringa kwenda Msembe, kilometa 104; na tumepewa jumla ya shilingi bilioni 142. Sasa mkandarasi yuko *site* anajenga kambi upande wa nyumbani kwa ndugu yangu pale Mheshimiwa Lukuvi. Kambi imekamilika na sasa wanamalizia nyumba za wakandarasi. Hayo ni mapinduzi makubwa ambayo yamefanyika kwenye Jimbo la Kalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unavyosikia watu wanasema kwamba hawawezi kuingia kwenye uchaguzi, unashangaa. Yaani unashangaa ni nini hasa kimewakuta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua suala la kukosa amani siyo suala la mchezo. Nilipata Bahati wiki iliyopita nilialikwa na chama kimoja cha Kimataifa cha Kibunge kuhudhuria Mkutano wa Umoja wa Mabunge Duniani, na Spika wangu alinipa kibali niweze kuhudhuria. Mambo yaliyokuwa yanajadiliwa pale ni mengi, lakini makubwa yalikuwa yanahusu migogoro ya kivita pamoja na amani na namna ambavyo watu wameendelea kuteseka katika Mataifa hayo kwa sababu ya kukosa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Chama cha Mapinduzi kitaendelea kuilinda hii tunu yetu ya amani kwa nguvu

kubwa kwa namna yoyote ile. Hata atokee mtu yeyote awe ni wa ndani au wa nje ambaye atajaribu kuichezea hii amani, kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Rais wetu aliapa kuilinda na atailinda kwa nguvu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawashauri wenzangu, kule Iringa huwa tunakula sana kande; ukishakula kande na umeshiba mshukuru Mungu, nenda ukalale ukapumzike, kwa sababu amani ya nchi hii inalindwa wakati mwingine hata kwa gharama ya damu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu walioko huko mipakani wakati mwingine kinachowatokea hatuwezi kusema. Kwa hiyo, naomba Watanzania tuwe na utulivu na tuendelee kudumisha amani katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ushauri. Serikali imeongeza ajira nyingi. Hapa tumesomewa kiasi cha ajiri milioni nane kimeongezeka, lakini ipo nafasi ya kuongeza ajira kwenye sekta binafsi, watu wengi wanatamani sana kuja kuwekeza katika Taifa la Tanzania. Tunaopata nafasi ya kutembea tembea huko unakutana na watu wengi wanaomba kuja kuwekeza, lakini mara nyingi wanasema kwamba ninyi sera zenu kidogo haziwi rafiki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa tumejaribu kutengeneza mazingira ya uwekezaji kuwa mepesi, lakini bado inaonekana kuna kikwazo cha watu kuja kuwekeza, kwamba kwanza kujibiwa kwa wakati maombi yao hilo ni changamoto ambayo tunaipata. Kwa hiyo, kama tukiweza kurekebisha hayo, tutakwenda vizuri na tutaongeza ajira kupitia sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inakua. Wakati fulani nilihudhuria mkutano mmoja ambapo mwakilishi wa *UNDP* hapa nchini Bwana Shigeki Komatsubara alisema kwa maneno yake kwamba, *"If Tanzania will continue with this same growth trajectory within the next ten years, it will be the strongest economy in East Africa."* Kwamba, kama Tanzania itaendelea

kukua kwa mwendo huu huu kwa miaka 10, nchi hii itakuwa na uchumi mkubwa ndani ya Afrika, yaani itaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji huu unaendana na changamoto mbalimbali. Ni lazima sera zetu ziwe vizuri, namna tunavyowakaribisha wageni, tuwe wepesi ili tuendane na ukuaji ambao vyombo mbalimbali vya kifedha, *World Bank* na *IMF* vinazungumza. Maana tunazungumzia mazingira rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukuaji wa nchi yetu hauendani sana na mipango miji. Yaani ukuaji wa nchi kiuchumi hauendani sana na ukuaji wa mipango miji. Kwa hiyo, iko sababu ya kuhakikisha kwamba tunawekeza kwenye mipango miji ili ukuaji wa uchumi uende sambamba na ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kushauri kwenye upande wa Serikali, kuna dalili kwamba katika maeneo mbalimbali ya nchi mwaka huu kutakuwa na njaa. Moja ya tarafa yangu katika tarafa tatu nilizokuwanazo, Tarafa ya Kalenga na maeneo mbalimbali ya nchi yatakuwa na njaa. Kwa hiyo, Serikali ijipange ni namna gani itakwenda sasa kuwahudumia Watanzania mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu Serikali ina akiba ya chakula zaidi ya tani 700,000. Kwa hiyo, tuanze kuweka mipango mapema na kutambua maeneo ambayo yameathirika na tuone namna gani tutahakikisha kila Mtanzania anapata chakula na kwamba hakuna Mtanzania atakayekufa kwa njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika upande wa kilimo, kwa sababu mabadiliko ya tabianchi ni jambo halisi kwa hiyo, ujenzi wa mabwawa yanayotokana na mvua iwe ni kipaumbele cha Taifa. Namshukuru sana Waziri wangu Jumaa Aweso, ameanza kutekeleza kujenga mabwawa ya kuvuna maji, na tumeyatembelea tumeyaona. Kwa hiyo, iwe ni dira ya Taifa na uelekeo kwamba kila eneo ambalo tunaweza tukajenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua uwe ni mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwenye eneo hilo ni kuhusu elimu. Naishukuru Serikali, kwa sababu sasa tumeelekea upande wa elimu ya ufundi zaid. Elimu ya Ufundi ndiyo itakayokwenda kuliokoa Taifa hili. Wiki iliyopita nilikuwa nasikiliza *BBC,* Tim Cook huyu *CEO* wa *Apple* aliulizwa, kwa nini umepeleka viwanda vyako China? Akasema China unaweza ukapata mafundi mchundo wengi katika eneo moja. Siyo kwamba tunakwenda kwa sababu kuna vibarua rahisi, hapana. Kwa hiyo, eneo hili ni eneo ambalo tunatakiwa tulitilie mkazo na Watanzania walipokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naona kengele imelia. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga. Nilimtaja Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Jonas William Mbunda, ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii tena ambayo nimeipata ya kuchangia kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Vilevile, nampoingeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ametajwa mara nyingi katika hotuba hii kutokana na kazi kubwa ambayo imefanyika ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uratibu mzuri sana wa miradi mingi ambayo imeandikwa kwenye hotuba hii, mingine ikiwa kwenye asilimia tisa, mingine asilimia tano na mingine asilimia mia moja. Pia, nawapongeza sana Mawaziri walio chini ya Waziri Mkuu, Makatibu Wakuu na wataalamu wote ambao wamehusika katika usimamizi na uratibu makini chini ya Wizara za Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa wazi kwamba Mheshimiwa Rais tarehe 22 Aprili, 2021 alihutubia na akaweka vipaumbele gani ambavyo anakwenda kuvifanyia kazi. Aliahidi

kudumisha mazuri yote ya awamu zote zilizopita. Ndicho hiki ambacho tumekiona kinaendelea kufanyika. Vilevile, kuendeleza mema yaliyopo na kuibua mengine mapya. Haya mambo mawili aliyasema kwenye hotuba yake na tumeendelea kuyaona katika utekelezaji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwenye kumbukumbu zetu pamoja na yale yaliyoandikwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, kuna miradi mikubwa imetekelezwa. Mradi wa kwanza ni wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere. Nilipata nafasi ya kwenda kulitembelea kama Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Kazi iliyofanyika pale ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari sasa hivi tunavyozungumza mashine zote zimeshawashwa. Maana yake ni kwamba mradi ule sasa upo katika 100%. *Megawatts* kama 2,115 sasa zinaweza kutumika na Watanzania. Hii yote ni nafasi nzuri ya kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mkuu na timu yake nzima kwa uratibu makini iliyohakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninatoka Kanda ya Ziwa. Ni wiki moja tu nimepita pale Daraja la Busisi. Wapo kwenye hatua za mwisho kabisa na daraja hili sasa lipo kwenye 98%. Ninampongeza Mheshimiwa Rais na ninampongeza Waziri Mkuu na timu yake yote kwa uratibu makini. Daraja ambalo mwaka 2021 lilikuwa na kiwango kidogo kabisa cha asilimia, hivi sasa linakwenda 98%. Muda siyo mrefu watu wa Kanda ya Ziwa na wengine kwa ajili ya biashara wataanza kupita kwenye daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe wazi kwamba ipo meli ya MV Mwanza ambayo inatengenezwa. Ukiangalia vizuri kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, utagundua kwamba meli hii nayo sasa ipo 98%. Kwa hiyo, mambo mengi yaliyofanywa yanaonekana kabisa yameratibiwa vizuri na yameasisiwa na Mheshimiwa Rais na yameratibiwa vizuri na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *SGR* ambayo watu wengi wanaitaja, imetupunguzia matatizo makubwa ya kwenda Dar es

Salaam na kurudi hapa. Vipo vipande vingine vingi ambapo kila kimoja kipo katika hatua fulani. Kipo kipande cha kutoka hapa kwenda Makutupora, kutoka Makutupora kwenda Tabora, kutoka Tabora kwenda Isaka na kipo cha Isaka kwenda Mwanza, na vilevile kwenye reli inayoelekea Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni kazi kubwa ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya. Kwa hiyo, mtu yeyote akitokea akasema kwamba haoni chochote kilichofanyika, kimsingi anakuwa anajidanganya mwenyewe kwa sababu mambo haya yanaonekana kwa macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sehemu ya ajira zilizozalishwa kwenye ripoti hii, inaonekana wazi kwamba kuna ajira zimezalishwa katika sekta binafsi na sekta ya umma ambazo hazipungui milioni nane. Tutakumbuka vizuri kabisa kwamba hata kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi hili lilikuwa limetajwa. Kwa hiyo, kimsingi tumetekeleza, tume-*comply* kwa zaidi ya 100%. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hili. Tulichoahidi kimetekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote niliyoyasema ni ya Kitaifa. Yapo yale ambayo mimi ninayaona jimboni kwangu. Ni vizuri nikayasema, ni kwa nini tunampongeza Mheshimiwa Rais na kwa nini uratibu huu wa Waziri Mkuu tunaupongeza sana? Kwa mfano pale Busanda sekta ya elimu ya shule za msingi mwaka 2021 tulikuwa na shule za msingi 132, sasa hivi ziko 150. Kwa hiyo, unaweza ukaona kuna kazi kubwa imefanyika kwenye elimu ya shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu ya sekondari tulikuwa na shule 30 mwaka 2021 na sasa hivi tuna shule 50. Hatukuwa na *high school* hata moja, na sasa hivi tuna *high school* nne. Kwa hiyo, tuna shule za Kidato cha Tano na Sita nne ambazo zimekuwepo tu kuanzia mwaka 2021 hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipita kwenye sekta ya afya sisi Busanda tuna hospitali yenye hadhi ya hospitali ya wilaya. Mwaka 2021 ilikuwa haijakamilika, imepelekewa fedha takribani shilingi

bilioni tatu, na sasa imekamilika na inafanya kazi katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo la Busanda wanapata huduma. Pongezi sana Mheshimiwa Rais na uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ndugu zangu wa *TARURA*, itakumbukwa wazi kwenye kumbukumbu zetu inaonekana kabisa *TARURA* kama *TARURA* tulikuwa tunapata kama shilingi bilioni 1.9 mwaka 2021. Leo tunapozungumza tunapata shilingi bilioni tano za kutengeneza barabara jimboni Busanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba kile ambacho kinaonekana Jimboni Busanda. Jimbo la nne kwa ukubwa Tanzania limeongezewa fedha kama mara nne hivi kwa ajili ya kutengeneza barabara zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, ninaishauri Serikali kwamba kuna mahali fulani kwa sababu ya baraka ya mvua ambayo imenyesha nyingi barabara zile sasa nyingine ziko katika hali mbaya. Kwa hotuba au bajeti hii itusaidie kuhakikisha kwamba zile barabara zinatengenezwa wananchi waendelee kufanya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, naishauri tu Serikali kwamba kuna mahali fulani kwa sababu ya baraka ya mvua ambayo imenyesha nyingi, barabara zile sasa nyingine ziko katika hali mbaya. Bajeti hii itusaidie kuhakikisha kwamba, zile barabara zinatengenezwa ili wananchi waendelee kufanya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *TANROADS* zipo barabara ambazo ziliingizwa kwenye bajeti mwaka 2024, barabara ya kutoka Mpovu - Geita kuelekea Kakola takribani kilometa 60. Tunasubiri tu kutia saini mkataba ule ili kazi hii iendelee kufanyika. Kwa hiyo, na hili nalo tuhakikishe kwamba hii inasainiwa ili barabara hii iendelee kufanyiwa kazi, na vilevile, kwa barabara inayotoka Ushirombo kuja pale Katoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji, katika miaka hii takribani minne tumepata visima virefu 17, ni pongezi kubwa tunakupatia Mheshimiwa Rais vilevile uratibu mkubwa unaofanyika na Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninaamini kabisa kwamba, kwa mazingira haya, hata kumtua mama ndoo kichwani inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, uko mradi mkubwa wa kutoka Chankorongo kuja pale jimboni kwangu wa takribani bilioni 6.2 kwenda pale Katoro. Maji yameanza kutoka na sasa kazi kubwa iliyopo katika bajeti hii ni kuomba pesa iongezwe ili mtandao uongezwe na wananchi waendelee kuhudumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya umeme mwaka 2021 katika vijiji 84 vya Jimbo la Busanda, vijiji 26 ndivyo vilikuwa na umeme. Leo hii ninapozungumza, vijiji vyote vina umeme, pongezi sana Mheshimiwa Rais, lakini pongezi kwa umakini na uratibu mzuri wa Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya niliyoyataja, sasa tunashughulika na vizimba vya samaki hatukuwa na ufugaji wa samaki kwenye jimbo letu, lakini sasa hivi tunashughulika na vizimba vya samaki na watu kadhaa, vikundi kadhaa vimeanza kufuga samaki eneo lile. Ninaamini kwa haya mazuri ambayo yametendeka na hotuba hii imeonesha yako mambo mengi ambayo yanaenda kufanyika hapa. Wananchi wetu watatoka hatua moja kwenda hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu tu, bajeti hii ijikite sana kuhakikisha kwamba yale ambayo nimeyasema ya kufanyiwa kazi, yafanyiwe kazi. Vilevile, bajeti hii ihakikishe kwamba yale ambayo yanatokea ghafla kwa sababu ya mvua hii kama hizo barabara ambazo nimesema za *TARURA,* basi ziweze kusaidika ili wananchi wetu waweze kupita kutoka hatua moja kwenda nyingine kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa wazi sekta ya madini. Sasa hivi kwenye maeneo yetu ya madini sisi ni wachimbaji wadogo, umeme umeenda kwenye migodi yetu. Niwapongeze

sana kwa kuwa uratibu katika sekta ya madini ni mkubwa sasa biashara ile inafanyika kwa namna ambayo watu wengi wanaona iko huru na tunaweza kuendelea kufanya uzalishaji wetu bila matatizo. Tutengenezewe barabara migodi hii ifikike na nchi iendelee kupata fedha na michango yetu ya Taifa kwa maana ya maendeleo iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naomba kuunga mkono hoja, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa. Nilimtaja Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, ajiandae.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, amenipa uhai na nimepata muda leo wa kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Kabla sijaanza na lolote naomba kwanza niunge mkono hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuandaa taarifa nzuri na hotuba nzuri ambayo ina mchanganuo mkubwa sana kwa mambo mbalimbali na miradi mbalimbali ya maendeleo yaliyotekelezwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie nafasi hii nimpongeze Naibu Waziri Mkuu kwa kumsaidia Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake. Pia, nawapongeza Mawaziri wawili: Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete pamoja na Manaibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Nderiananga na Patrobass Katambi kwa kuendelea kumsaidia Waziri Mkuu kutekeleza majukumu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Dira ya Taifa ambayo tunafikia ukomo wake mwaka 2025/2026 pamoja na mkakati ule wa miaka mitano ambao unaishia sasa hivi, lengo kubwa ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, tunakuwa na uchumi shindani wa

viwanda na tuhakikishe kwamba tunapofikia ukomo wa dira hiyo pamoja na Mpangomkakati wa Taifa, tunakuwa tumeboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulitekeleza hilo, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha nyingi na kutekeleza miradi mingi katika nchi yetu ili kufikia lengo la kuhakikisha kwamba maisha ya wananchi yanaboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji wa miradi ya kimkakati kama Bwawa la Mwalimu Nyerere, Mradi wa *SGR,* na Mradi wa Daraja la Busisi pia, ametekeleza miradi mingi sana kwenye maeneo yetu ya majimbo ambako tunatokea. Miradi hiyo iliyotekelezwa, imelenga moja kwa moja kuhakikisha kwamba inatatua changamoto ya wananchi katika mazingira mbalimbali, pia inaboresha moja kwa moja maisha ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba changamoto za wananchi zinatatuliwa, tukianza na sekta ya elimu katika kipindi hiki cha miaka minne, kuna miradi mingi imetekelezwa pamoja na kujenga shule mpya. Katika Jimbo langu la Mbinga Mjini, kuna shule mbili za msingi mpya zimejengwa. Kuna Shule ya Matengo Matarawe na Shule ya Mwamko Mpepai; hizi ni shule mpya zimejengwa na Serikali hii ambayo ilikuwa ina lengo la kuhakikisha kwamba inaboresha maisha ya wananchi. Katika kuondoa ujinga, niliona kwamba, ni vizuri kupunguza msongamano ambao ulikuwepo kwenye shule zetu mbalimbali kwa kujenga shule mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa shule za sekondari, pamoja na kujenga madarasa mengi kupitia Mradi wa *SEQUIP*, pia Serikali kwenye Jimbo la Mbinga Mjini imejenga shule nne mpya, shule tatu za sekondari za kawaida, na shule moja ya ufundi ambayo inaitwa Amali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maisha yangu sijawahi kuona Serikali inajenga shule ndani ya miezi mitatu au minne inakamilika na watoto wanaanza kusoma. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba imefanya vizuri kwenye sekta ya elimu kujenga shule kupunguza msongamano kwenye shule mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo, kwenye upande wa elimu, Serikali ilitoa zaidi ya shilingi bilioni moja kukarabati chuo kikongwe cha maendeleo ambacho kimekaa muda mrefu na majengo yalikuwa yamechakaa, lakini naipongeza Serikali, majengo yake yamekarabatiwa na sasa hivi chuo hiki kinaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la afya, katika mpango ule ule wa kuhakikisha kwamba Serikali inaboresha maisha ya wananchi, naomba niipongeze Serikali kwa kufanya mambo yafuatayo: Kwanza, kuendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kununua dawa pamoja na vifaatiba. Pia, Serikali ilitoa msaada wa kujenga zahanati 13 katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyongeza ya hiyo, Serikali pia ilitoa fedha ya kujenga vituo vipya vya afya viwili. Halmashauri ya Mji wa Mbinga ilikuwa na changamoto kubwa sana ya uchakavu wa majengo ya hospitali ya wilaya. Mwaka 2023 Serikali ilitoa shilingi milioni 900 kuanza kufanya ukarabati katika majengo yale. Sasa hivi nataka niseme kwamba, majengo matatu ya *OPD,* jengo la maabara pamoja na jengo la wagonjwa mahututi yameshakamilika na wananchi wale wamefurahi sana kwa sababu mazingira ya hospitali yamebadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya maji, Mji wa Mbinga pamoja na maeneo mengine ya pembezoni yalikuwa na changamoto kubwa sana ya maji pamoja na kwamba sisi kule tuna vyanzo vingi vya maji kwa upande wa mteremko, lakini bado kulikuwa na changamoto ya upatikanaji wa maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali, ilitoa miradi mikubwa katika Kata ya Mbangamao, Kata ya Mpepai, Kijiji cha Ruvuma Chini, Kijiji cha Tanga, Kijiji cha Kitanda, Utiri, Miyangayanga. Maeneo haya yote yamepelekewa miradi mikubwa mikubwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa Mbinga Mjini tulikuwa na changamoto ya maji, Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaongeza upatikanaji wa maji. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali kwa hilo. Pia, tarehe 26 Machi, 2025 Serikali imesaini mkataba wenye thamani ya shilingi bilioni 4.6 kwa ajili ya kuongeza vyanzo vya maji na upatikanaji wa maji kwa mji wa Mbinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miundombinu naomba niishukuru Serikali, kwani imetoa shilingi bilioni 16.5 kwa ajili ya kujenga barabara inayotoka Mbinga Mjini kwenda Utiri Mahande kwa kilometa 14.4. Pia, pale mjini imejenga kilometa 3.6 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara zile za mjini pale zinakuwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, kuna maeneo ambayo yalikuwa na changamoto kwa upande wa Barabara za changarawe kutoka Mbinga kwenda Mpepai, Mbinga – Kikolo – Kihungu; Mbinga – Kitanda – Kihungu na Mbinga – Luwaita. Katika maeneo haya, barabara hizo zimetengenezwa kwa kiwango cha changarawe na sasa hivi zinapitika. Naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa umeme, Jimbo la Mbinga Mjini lina vijiji 78. Leo nikupe taaifa kwamba, vijiji vyote vimepatiwa umeme, na vitongoji 104 vimepatiwa umeme. Pia, kwenye upande wa mawasiliano, Mbinga kuna maeneo mengine watu walikuwa wanapanda kwenye miti kutafuta mawasiliano, lakini leo nataka nitoe taarifa kwamba, Serikali hii sikivu imeweza kupeleka minara ya simu katika Kata ya Mpepai, Kata ya Kitanda, Kata ya Utiri na Kijiji cha Ruvuma Chini. Wananchi wale wamefurahi sana na wanatoa shukrani sana kwa Serikali kwa kukamilisha hili suala la mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye upande wa kilimo, wananchi wa Mbinga ni wakulima wa mazao mbalimbali ya biashara, tunatoa shukrani kwa Serikali kwa kutoa pembejeo za ruzuku pamoja na mbegu. Pamoja na mambo yote yaliyotekelezwa kuhakikisha kwamba wananchi hawa wananeemeka na utendaji kazi wa Serikali, pia bado kuna mambo ambayo bado yanatakiwa yatekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kugawa umeme kwenye vijiji vyote, miundombinu iliyopo ile inazidiwa. Kwa hiyo, kuna uhitaji wa kuwepo na kituo kidogo cha kupooza umeme ili kuweza kuhakikisha kwamba, umeme haukatiki mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wananchi wale wanahitaji zile barabara zinazosafirisha mazao kuja mjini, kama barabara kutoka Mbinga kwenda Litembo, Mbinga – Pachanne – Longa wananchi hawa wanahitaji barabara hizi zitengenezwe ili waweze kupitisha mazao na kuweza kuneemeka katika eneo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya sasa na kwenye bajeti ya safari hii, tunaomba tuweze kupata shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuendelea kumalizia ukarabati wa Hospitali ya Mji wa Mbinga. Mji wa Mbinga upo katika miji 45 ambayo itatakiwa ineemeke na mradi wa *TACTIC*. Miji mingi imeshafanikiwa, sisi tulikuwa awamu ya tatu. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo ambayo tutakwenda kujenga barabara kilometa 12.6, mradi wa soko pamoja na stendi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imejenga madarasa mengi, imeongeza miundombinu ya shule za msingi pamoja na sekondari bado tuna changamoto ya wafanyakazi, walimu na wafanyakazi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ili kuendelea kuwapa moyo wale wakulima ambao wanalima mazao mbalimbali ya kahawa na chakula, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuhakikisha inaimarisha na kutafuta masoko mbalimbali ili wananchi wale waweze kupata masoko ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi na ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jonas William Mbunda. Nilimtaja Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nami nafasi niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba hii ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo tunasema hizi ni bajeti za majumuisho baada ya kazi kubwa ambayo imefanyika kwa miaka hii minne ya uhai wa Bunge hili. Sasa hii ni bajeti ya majumuisho ya mambo mema mengi mazuri ambayo Serikali yetu kupitia usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu imeyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, pamoja na Mawaziri walioko kwenye ofisi yake, Manaibu pamoja na watendaji kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nipo kwenye Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria kule tunasimamia pia ofisi ambazo ziko chini ya Waziri Mkuu. Tunapata ushirikiano mzuri kutoka kwao na tunaona mambo mengi yanakwenda ikiwemo lile la kukamilika kwa jengo la Msajili wa Vyama vya Siasa hapa Dodoma ambapo tunatarajia fomu ile ya Mheshimiwa Rais itatokea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo niseme kwamba nampongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye kwa kiwango kikubwa Watanzania wanaridhika na utendaji kazi wake, uaminifu wake, uadilifu wake na uchapakazi ambao ameuonesha kwa kipindi hiki akiwa madarakani, na ndiyo maana siku ile ya tarehe 18 - 19 Januari, 2025 wanachama wenzake wa CCM tukiwepo sisi tukasema kwa kauli moja kwamba mama yetu huyu, Rais wetu kipenzi, anastahili kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa kipindi kingine cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya hivyo siyo kwa kukurupuka, ni baada ya kuona kazi nzuri iliyofanyika. Kikao cha watu 3,000 kimefanya tathmini maeneo mbalimbali, kona mbalimbali za nchi yetu tukaridhika kwamba Rais wetu na Serikali yake inastahili kuungwa mkono na kupewa ridhaa tena kwenda kuongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuseme ukweli, Chama cha Mapinduzi ndicho kinachoongoza hii nchi. Tumeona uadilifu na msimamo mzuri wa Rais wetu kama Mwenyekiti wa CCM pamoja na Chama chake. Ndiyo maana hata aliposema Dkt. Nchimbi awe mgombea mwenza wa nafasi ya Makamu wa Rais, Watanzania na Wana-CCM walipongeza na waliridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani kubwa na Dkt. Nchimbi, tuna imani kubwa na Rais wetu, wafanye kazi kwa kujiamini wakiwa na *confidence* kwamba sisi Wabunge wa CCM, Wabunge wa Bunge hili tunawaunga mkono na tunaamini kwamba, yale wanayoyafanya yanawahudumia Watanzania na Watanzania wanaridhika na kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo langu la Singida Kaskazini, nasi tunazo sababu za msingi za kusema kwamba hii bajeti hii ya sasa ni majumuisho. Tumeona mambo mengi mema yaliyofanyika ya kuondoa kero na adha mbalimbali kwenye huduma za kijamii ambazo zilikuwa zinawatatiza sana wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalan, nikianza kwenye *issues* za eneo la umeme. Suala la umeme katika jimbo lenye vijiji 84, leo vijiji vyote 84 vimewasha umeme, shughuli za wananchi zinaendelea. Siyo tu kuwasha umeme, tumepata hata umeme kwenye maeneo yale ya madini, hata ya umwagiliaji. Ni maeneo ambayo yalikuwa yanafanya kazi kwa kusuasua, lakini katika Serikali hii tumeona mambo yakifanyika kwa uthabiti mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Mgodi wa Madini ya Mpambaa pale, Mpipiti pale, Mudida pamoja na eneo la

umwagiliaji pale Jangwa kwa Ma-*sister,* Leo wanafanya kazi zao vizuri kwa ufanisi kwa sababu wana vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili, niendelee tu kuomba sasa kwa kuwa tunasema tunakwenda kwenye ngazi ya vitongoji, kazi iendelee na kasi iongezeke ili wananchi wetu walioko kwenye vitongoji wanaohitaji umeme nao wafikiwe. Pia, tathmini iendelee kufanyika ya ile shilingi 320,000/= kwenye vijiji miji ambayo tulisema iwe shilingi 27,000/= baadaye ikawa shilingi 320,000/= bado ina malalamiko kidogo. Kwa hiyo, ni vyema nayo ifanyiwe tathmini ili wananchi wetu waweze kuunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la elimu, kwenye jimbo langu tumepata shule mpya zilizoota kama uyoga. Tumeona Shule ya Sekondari Mkimbii, Shule ya Sekondari Sekouture, Shule ya Sekondari Msange ambayo tunaenda kuizindua keshokutwa na Mkuu wa Mkoa, tarehe 12. Hakika tunayo sababu ya kujivunia utendaji mzuri wa hii Serikali yetu ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zinaota kama uyoga, inaanza na tofali mpaka na madawati, vyumba 16 vya madarasa. Hii haijawahi kutokea, tunayo kila sababu ya kuiunga mkono Serikali hii. Tumepata hizi shule tatu mpya, lakini na vyumba kemkem vya madarasa, mfano pale Ughandi tumepata vyumba 15 vya madarasa, na Kinyeto vyumba 15 vya madarasa. Hizi ni shule ambazo tungeweza kusema tukaanzishe shule nyingine, leo tungesema shule zimeongezeka 10 katika jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia njema ya kuboresha miundombinu ya elimu na kuhakikisha watoto wetu wanasoma katika mazingira mazuri ya shule za msingi na ile ya Minyaa pamoja na Sekoutoure. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kengele, nizungumzie kidogo kwenye eneo la kilimo. Namshukuru

sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumepata Mradi wa Umwagiliaji pale Msange shilingi 17,700,000 ambao unakwenda kukomboa maisha ya Wanasingida Kaskazini. Mnafahamu Mkoa wa Singida ni *semidesert* kama unavyoona Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pale tunakwenda kuhakikisha tunafanya kilimo hata wakati wa kiangazi, hii ni historia kubwa katika Jimbo letu la Singida Kaskazini. Nampongeza sana Waziri wa sekta husika Mheshimiwa Bashe pamoja na *Eng.* Raymond pamoja na yule *Eng.* Japhet Senyina wa Mkoa Singida, Meneja wa Umwagiliaji wa Mkoa Singida kwa usimamizi mzuri wa mradi ule ambao unaendelea na utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapozungumza, kazi inaendelea ya kutathimini ile *feasibility study* katika Bonde la Songa Mwandumwa pale Kata ya Mughamo, nao unakwenda kukamilika labda katika bajeti hii. Kwa hiyo, naishukuru na kuipongeza sana hii Serikali sikivu kwa wananchi wake wanyonge, na miradi mingine ile ya visima virefu katika Jimbo langu ninaomba pia iendelee kutekelezwa ili wananchi wetu wanyonge waachane na unyonge huo, wapate huduma ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la afya, katika historia, jimbo lile halijawahi kuwa na Hospitali ya Wilaya, lakini leo tuna hospitali nzuri ya wilaya ambayo mgonjwa kabla hajaanza kutibiwa, tayari ameshapata matumaini ya kupona kwa majengo mazuri, huduma nzuri kutoka kwa madaktari, na vifaatiba. Leo mama zangu, wadogo zangu, dada zangu wanakwenda pale wanajifungua kwa utaratibu mzuri na kwa huduma nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunakwenda hospitali za mikoa mingine ya jirani, lakini leo mikoa ya jirani na wilaya za jirani wanakuja Ilongero pale Singida Kaskazini kupata huduma za afya. Sasa mimi ni nani mpaka nisiseme ahsante Serikali yangu, ahsante Rais Dkt. Samia pamoja na Waziri Mkuu ambaye anasimamia kazi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata vituo vya afya, tumepata fedha hivi sasa Ujenzi wa Kituo cha Afya Ngimu unaendelea. Shilingi milioni 686, Kituo cha Afya Makuro kimeshakamilika wananchi wanapata huduma. Niendelee kushukuru hatua hizi, na niseme kwamba,

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umewasha maiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maboma ya zahanati, maboma ya madarasa ambayo bado hayajakamilika yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi, naiomba sana Serikali yetu itupe fedha tukamilishe maboma yale ili wananchi wetu waendelee kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, naomba fedha kwa ajili ya Ujenzi wa barabara ile ya lami ya Igauri – Ilongero inayokwenda Makao Makuu ya Wilaya. Hili ni hitaji la wananchi wa Singida Kaskazini, na ni ahadi ya bajeti ya 2023/2024 lakini hadi sasa bado hatujapata fedha na wananchi wanaililia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Flatei Gregory Massay na Mheshimiwa Venant Daud Protas ajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Kwanza nianze kumshukuru Mungu jioni ya leo kwa sababu ya nafasi hii kuwepo hapa. Pili, nitoe shukrani zangu za kwanza kabisa kwa Waziri Mkuu, maana nimeiona bajeti hii ambayo ametusomea hapa na tumeona kila sekta katika eneo hili la ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Mawaziri walio kwenye ofisi yake. Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Ridhiwani,

niwapongeze pia na Manaibu wawili ambao kwa kweli wapo kwenye Wizara hii wakisaidiana na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ametusaidia sana kwenye maeneo yetu, kazi yake ameifanya *effectively,* yaani kwa usahihi sana. Kwenye Jimbo langu ameshawahi kuja kuweka jiwe la msingi la halmashauri ambayo kwa kweli imetutoa aibu. Maana yake tulikuwa tunakwenda kilomita zaidi ya 50 kutafuta halmashauri. Leo hii nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye bajeti yake hii ambayo kwa kweli huwezi kuamini imegusa nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza pia Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua na kumweka hapa ambapo kweli bajeti hii ameileta leo na kuisoma. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, naridhika na bajeti hii na kuanza kuiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa sio mtu anayesifia sana, lakini leo naomba nisifu hii kwa sababu nimeiona na imetusaidia kwa kipindi hiki ambapo nimekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini. Ukiangalia maeneo mengi ambayo Mbulu Vijijini tulikuwa tunahitaji bajeti hii imegusa, lakini kabla ya hapo pia katika miaka hii minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeguswa Mbulu Vijijini kwa maeneo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia eneo ambalo lilikuwa na shida kubwa ilikuwa ni namna ya kumtua ndoo mama kichwani. Jimbo la Mbulu Vijijini lina kata 18, na hivi navyozungumza kila kata ina mradi ambao umeletwa na Serikali kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambako miradi hii inakwenda kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yako maeneo mengine hayajafikiwa, lakini juzi hapa tumesaini mkataba wa kujenga kituo kikubwa cha maji ambacho maarufu tunaita kwa jina la Dambia, inakwenda kufikia vijiji 21. Nina vijiji 76, lakini mradi huu unakwenda kumaliza kero kwenye vijiji 76 ukiwepo mji mkubwa

ambao tunaita wa Haydom, ambapo kuna hospitali kubwa ya rufaa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaposema ukimaliza kazi unavalishwa taji, kwa sisi tunaoabudu kwenye Biblia huwa ni kwamba mama huyu anayeitwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri kwa kweli anatakiwa kuvalishwa taji kutokana na jinsi ambavyo anakwenda kutusaidia kwenye eneo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Waziri wa Maji na amekuja jimboni kwangu amesaidia kuipeleka ile miradi ambayo kimsingi ilikuwa imekwama na sasa miradi ya maji inaendelea. Najua kuna visima vichache vitano ambavyo tunatakiwa kuvichimba, vinne vimeshachimbwa, bado kimoja na hii ilikuwa imaliziwe tu, na juzi bahati mbaya kulikuwa na mvua ambayo najua gari la kuchimba halikuweza kufika. Naamini baada ya muda, atamalizia kile kisima kimoja. Kwa jinsi hii, ndiyo maana leo nashukuru hapa kwa eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo mengi leo tunapaswa kushukuru sana Serikali. Unajua sisi Wakristo tunaposali sala ya Baba Yetu Uliye Mbinguni, tunamsifu Mungu halafu ukisema Jina lako litukuzwe, unamsifu Mungu; halafu ukisema mapenzi yako yatimizwe, unamsifu Mungu; lakini kuna mahali unasema utupe riziki za kila siku; hapo maana yake unaweka ombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Mimi Flatei leo ninasifu hapa ili baadaye niweke ombi, na kila mtu anataka sifa. Kwa nini nasema hivi? Kama Mwenyezi Mungu mwenyewe anataka sifa, amesema kwenye mistari yake ile ya kwanza na hii sala ameisema; ukisoma kwenye Yohana, anasema hii ni sala kuu aliyekufundisha yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naposema hii sala maana yake namsifu Mungu, lakini Dkt. Samia Suluhu Hassan namsifu kwa sababu naye pia ana roho, ni binadamu, naye anataka sifa. Kwa nini nasifu? Siyo nasifu tu kwa sababu, nasifu, Hapana. Nasifu kwa sababu tumepata jambo. Kwenye Jimbo la

Mbulu Vijijini, nilipokuja Bungeni hapa, tulikuwa na vijiji tisa vyenye umeme, leo vijiji 76 vina umeme Jimbo la Mbulu Vijijini na Kata zake 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa muungwana ni vitendo. Ukiangalia hapa Mheshimiwa Dkt. Samia ametusaidia kwenye shule mbalimbali. Kwenye Jimbo la Mbulu Vijijini kulikuwa na shule za sekondari 15, lakini sasa hivi tuna shule za sekondari 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko shule ambazo zimemea, huwezi kuamini. Kuna Shule ya Masieda imejengwa imekamilika, unatoka mwanzo mpaka mwisho inamalizika. Pia kuna Shule ya Haydom pale inaitwa Basonyagwe inajengwa mpaka mwisho inakamilika. Vile vile kuna Shule ya Eshkesh imejengwa na hata sasa hivi na wasiwasi wanafunzi wanaweza wasiijaze shule hiyo. Ziko shule zinazojengwa za amali pale Bashay, kwenye eneo la elimu tu, tumepata shilingi bilioni 11, ni jambo la kushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia eneo *TARURA*, *TARURA* tulikuwa tunapewa shilingi milioni 666, lakini sasa hivi tunapewa shilingi bilioni nne kwa mwaka. Nafikiri huu ndiyo wakati muafaka wa kusema ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule ni wakulima wa vitunguu, mahindi, mbaazi, maharage na wakulima wa dengu. Leo hii Bajeti ya Kilimo imeshakuja na shilingi bilioni 19, tunakwenda kukarabati majosho, mabwawa, tunakarabati skimu yenyewe ya Mongahay, tunaenda kujenga Skimu ya Mongahay, tunakarabati Skimu ya Mangisa na Dongobesh na pia tunajenga skimu mpya Dirim.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nayoyasema yameandikwa, na yapo, ndiyo maana naipongeza bajeti hii ambayo najua kwamba inaenda kusaidia kwenye eneo la uzalishaji kwa maeneo yetu. Haya ninayoyasema ni kwa sababu tu tumeshapata, lakini ukiangalia kwenye eneo la mitandao au minara ya simu leo hii kuna maeneo yetu ambayo yalisahaulika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika maeneo ya Yaedachini, Eshkesh, Endahagichan, Masieda na maeneo mengine ambayo

hata nikitaja ni vigumu hata wewe mwenyewe kukumbuka, lakini ukweli nimepata minara ya simu na watu wanasikilizana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa wale watu wanaojua kule kwetu tuna kabila linaloitwa Wahadzabe, walikuwa hawawezi kabisa kuwasiliana kwa simu. Leo wanakaa porini na wakiwa kule wanasikilizana na mambo yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu leo nimeongea naye na kuna jambo zuri ambalo tumeshaambiana pale na Waziri husika wa TAMISEMI ametupatia pesa, shilingi milioni 100 ya kukarabati barabara ya kutoka Maretadu kwenda Haydom ambayo tuliiomba sana, ilikuwa barabara ya halmashauri, hali yake ilikuwa mbaya. Kutokana na hali hii, amekubali kutusaidia hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naishukuru pia Serikali, nayo imekubali kujenga Barabara ya Haydom kuja Labay na hivi karibuni ilisimama kwa sababu ya kukosekana kwa pesa. Leo hii nakwambia nimepata ahadi ya kutosha kwamba mkandarasi ameambiwa arudi *site* ili barabara hii iendelee kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, kama, tangu uhuru barabara haikuwa imejengwa kabisa, leo hii Mheshimiwa Dkt. Samia amekubali, tumetia Saini, amerudi mkandarasi *site* anaendelea kuijenga, kwa hiyo, kwa muungwana ni vitendo, ni vizuri kusema ahsante. Unajua ukisema ahsante, basi maana yake unapewa nyingine. Naishukuru sana hii Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hapa tulipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuja Bungeni nikiwa na mchecheto kweli kweli, nawe ulikuwa hapo, siku moja uliona mambo yalivyokuwa, nilipojaribu kung’ang’ania bajeti ya Wizara ya Ujenzi, lakini mama akaona huyu kijana atavunjia kiuno, ngoja nimsaidie. Akatuwekea mambo, akawaambia wakasaini mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria, kuna wazazi wengine unaweza kuwa mtundu akakutolea nje, lakini mama huyu mimi baada ya kuwa mtundu Bungeni hapa, nawe unakumbuka Spika alikaa hapo naye akanivumilia. Hivyo, nashukuru sana kiti chako Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, kwa kweli umenivumilia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni wakati wa kuidai barabara kwa nguvu, ilikuwa ni wakati wa kuwawakilisha watu wa Mbulu Vijijini kwa nguvu, ilikuwa ni wakati wa kupaza sauti yao kwa nguvu, lakini kwa lugha ya picha hapa daktari alinivumilia. Huyo ni Spika wetu, nimpe ahsante sana, kwa kweli alinivumilia. Siyo yeye kunivumilia tu, mama naye akasema Hapana, hebu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu njoo, weka hela pale, rudi kule mambo yakaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nina furaha kusema barabara nayo imeanza kujengwa, naamini kwamba wataenda vizuri. Ni muda mzuri wa Flatei kusema ahsante mbele la Bunge hili. Maana ile ilienda maeneo mengi sana wakasema jamaa huyu vipi? Ile ilikuwa ni kuonesha lugha ya picha na kuonesha uchungu wa barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu naye ameniahidi leo kwamba fedha bwana usiwe na wasiwasi, kabla ya bajeti yake atapeleka pesa. Sasa kwa nini mimi nisikubali? Yule mwenye pesa, mwenye pochi kasema atafungua, Rais mwenyewe kashakubali, mimi ni mtumishi tu, nyoka wa Mbulu Vijijini nina shida gani hapa? Nami nakupongeza na kukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii na Bajeti ya Waziri Mkuu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Gregory Massay ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Venant Daud Protas, na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya ajiandae. Mheshimiwa Venant hayupo, karibu Mheshimiwa Khadija. *(Makofi)*

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima ambao amenijalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa pia ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais kwa kweli amefanya kazi nzuri sana. Sisi watu wenye ulemavu tuna mengi sana ya kumshukuru sana sana. Kwa hiyo, naomba nieleze umma mambo mangapi Mheshimiwa Rais ameyafanya kwa watu wenye ulemavu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye upande wa vyuo, leo watu wenye ulemavu wengi wanapata elimu, na baadhi ya vyuo ambavyo vimekarabatiwa katika kipindi cha Mheshimiwa Rais, ni Chuo cha Yombo – Dar es Salaam kimekarabatiwa, Chuo cha Sabasaba – Singida kimekarabatiwa, Chuo cha Ruwanzari – Tabora kimekarabatiwa, Chuo cha Mtapika – Masasi kimekarabatiwa, na Chuo cha Masiwani – Tanga kimekarabatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hakuishia hapo, ameidhinisha tena fedha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi katika mikoa hii hapa ninayoenda kuitaja; Mkoa wa Kigoma – Chuo cha Watu Wenye Ulemavu, Mkoa wa Songea – Chuo cha Watu Wenye Ulemavu, Mkoa wa Mwanza pamoja na Ruvuma – Chuo cha Watu Wenye Ulemavu. Tumpe nini Mheshimiwa Rais? Yaani hatuna cha kumlipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwa upande wa mafuta ya watu wenye u-*albino* eh Mungu wangu, mbariki huyu mama. Mwaka 2022/2023 Mheshimiwa Rais ameidhinisha shilingi milioni 60 kwa ajili ya maandalizi ya kutengeneza mafuta ya watu wenye u-*albino;* mwaka 2023/2024 Mheshimiwa Rais ameidhinisha tena shilingi milioni 60 nyingine jumla katika miaka hii ya bajeti ya fedha shilingi milioni 120 imeidhinishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizuri zaidi, mwaka 2024/2025 yametoka maelekezo katika kila halmashauri, waweke bajeti ya

kununua mafuta ya watu wenye u-*albino*. Maana yake ni nini? Maana yake mafuta haya yanaenda kutolewa bure. Bure, sijui mnanielewa! Mnanisikia! Mafuta ya kinga yanaenda kutolewa bure. Kwa nini tusimshukuru Mheshimiwa Rais? Kwa nini nisimshukuru? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiachana na hayo kwenye upande wa ajira, Mheshimiwa Rais ameweza kuajiri katika sekta mbalimbali watu wenye ulemavu, ameweza kuajiri katika sekta ya afya, sekta ya elimu, sekta ya ustawi wa jamii pamoja na lishe idadi ya watu 1,218. Mheshimiwa Rais tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Mheshimiwa Rais hakuishia hapo, ameenda kwenye upande wa elimu, Mheshimiwa Rais ameidhinisha shilingi bilioni nne. Hizi shilingi bilioni nne zimeenda kujenga mabweni 50 katika halmashauri 50, ambapo wanaenda kuchukua wanafunzi 4,000, hawa ni watu wenye ulemavu. Tumpe nini Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais huyo huyo ametujengea imani watu wenye ulemavu. Leo hii tuna Naibu Waziri ambaye ni mtu mwenye ulemavu, tuna Wakili Mkuu wa Serikali ni mtu mwenye u-*albino*, kuna Makatibu Wakuu, sasa tumpe nini huyu Mheshimiwa Rais? Eeh! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nawapongeza wasaidizi wake. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza sana, umefanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe pamoja na msaidizi wako Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko pamoja na Mawaziri wako wawili, Mheshimiwa Ridhiwani pamoja na Mheshimiwa Lukuvi na Manaibu Waziri wote, kwa kweli mmefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu pale ambapo alikuja katika kongamano ambalo liliandaliwa na *Keysha Empowering Development Foundation,* alitoa amri katika halmashauri zake zote waweke ofisi za watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi za SHIVYAWATA katika halmashauri zote zinaenda kujengwa, zinakuwepo pale. Maana yake ni nini? Watu wenye ulemavu wanaenda kufikika, na changamoto zao zinaenda kusikika. Hadi sasa ni 70% ya halmashauri ambazo zimeweza kutengeneza ofisi za watu wenye ulemavu. Tumpe nini huyu mama? Tumpe nini huyu mama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu, Waheshimiwa kwa wenzangu wale wanasema, "Baba wa Mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, utupe leo mkate wa kila siku." Sisi Waislam tunasema, *"Alhamdulillahi Rabbil Alamin, A-rahman Rahim."* Mwingi wa Rehma na mwenye kurehemu, Mfalme wa siku ya malipo na tukasema, utuongoze katika njia iliyonyooka. Maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, tunasifia halafu tunaomba. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika bajeti ya mwaka 2024/2025 mlitenga kiasi cha fedha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kusaidia Vyama vya Watu Wenye Ulemavu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hii fedha bado haijaingia. Ombi letu, fedha hii iingie. Tunakuomba sana, ili fedha hii iende kufanya vile vyama viweze kufanya kazi nzuri ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Serikali imeweza kutengeneza mkakati mzuri wa kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata mafunzo katika vyuo. Hivi vyuo wakimaliza, wanaenda kupewa tena mikopo ya asilimia mbili. Tumpe nini Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kama mikopo itatolewa, basi tuanze hata kwa kutoa vifaa. Kama mtu amejifunza kutengeneza keki, basi anunuliwe hata mashine ya kilo moja ya keki ili aweze kuanza kuuza hata *cupcakes,* aweze kujipatia kipato kiasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaomba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, la mwisho, naomba niseme ambalo nimeshalisema sana humu ndani. Naomba sana kwa jicho la Mheshimiwa huyu mama ambaye leo hii ana kauli mbiu ya kusema, "Kazi na Utu, Tunasonga Mbele." Kwa kweli utu wake ameudhihirisha na aendelee kuudhihirisha kwa kusaidia wamama wenye watoto wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wenye watoto wenye ulemavu wanateseka sana. Utakuta kuna mwingine ni mfanyakazi wa Serikali kajifungua mtoto mwenye ulemavu, hawezi kumwachia mtu. Siku hizi hatuna ndugu wa kutusaidia, hatuna chochote, sasa hawa watoto wanalelewa vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni ombi langu la mwisho katika ile kaulimbiu ya kazi na utu, Mheshimiwa Rais Mungu akikujaalia unarudi tena katika Tanzania hii kutuongoza. Tunaenda kukupatia kura nyingi za "Ndiyo", lakini ombi letu kubwa ni kusaidia hawa akina mama wenye watoto wenye ulemavu, ili waweze kulea watoto wao vizuri na kufanya kazi zao vizuri. Ni namna gani ya kusaidia? Tutakaa sisi kama Kamati, tutakaa kama Serikali basi tuweze kuona ni namna gani mnaweza mkasaidia hili suala likaenda kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo machache, nawashukuru sana, naomba nishukuru sana leo hii kwa sababu hii ni Wizara yangu ambayo mimi ni Mjumbe wa Kamati. Niliamua niseme hayo machache na ni mengi ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya. Tunaendelea na Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo ajiandae.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi nami kuwa mmoja wa wachangiaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nami niungane na Wabunge wote kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ambayo

kimsingi kwa mujibu wa Katiba mwaka huu itakwenda kwenye uchaguzi na baadaye tunaamini tutakwenda kushinda kwa kishindo, kwa sababu leo tangu Mheshimiwa Waziri Mkuu amewasilisha bajeti yake ya Serikali, kila Mbunge hapa anayezungumza na anayesimama hapa, hakuna Mbunge ambaye amesimama anaeleza changamoto kubwa ambazo zimeshindikana kufanyika na Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wote hapa tunaungana kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uthubutu wake. Tunafahamu aliipokea Serikali katika kipindi cha mpito, lakini amesimama kwa uimara wake na kuisaidia nchi na wananchi kutokuona mabadiliko yoyote, zaidi ameongeza *morale* kwa wananchi na leo kila mahali maendeleo yamepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi za kumpongeza Mheshimiwa Rais, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kiukweli Mheshimiwa Waziri Mkuu licha ya kuwa na shughuli nyingine kuwa ni msimamizi wa Shughuli za Serikali Bungeni, lakini amekuwa kiunganishi muhimu baina ya Serikali na Bunge letu hili kwa Mbunge mmoja mmoja, pia Bunge na Serikali vyote vinakwenda katika kutatua changamoto za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wawakilishi wa wananchi tumekuwa na ukaribu zaidi na msimamizi wa Serikali na kusaidiana na wasaidizi wake Mawaziri hao ili kuweza kuleta maendeleo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hapa wamesema mengi. Leo tukisema kila Mbunge aseme nini amefanyiwa na Serikali yake, tutasema kila mambo ya kila namna. Kwenye Jimbo la Igalula, tumeingia, tumeona angalau Serikali zilizopita zimefanya kazi kwa kipindi chake, lakini Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya zaidi na zaidi kuliko Serikali zote ambazo zilikuwa zimetangulia na watangulizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Sekta ya Elimu tumeweza kujenga shule mpya. Zamani ilikuwa fedha zinaletwa kujaziliza kwenye shule za zamani, lakini kwa kutambua umuhimu wa wananchi wanahitaji huduma, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kujenga shule mpya za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika kipindi cha miaka mitano kwenye Jimbo moja tu la Igalula tumeweza kujenga shule zaidi ya tano ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta zaidi ya shilingi bilioni 3.8 ambazo zimekwenda kusaidia wananchi. Pia, tumeweza kupata shule moja ambayo tumesaidiwa na Shirika la Reli *(TRC),* na hapa napenda kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli, Ndugu Masanja Kadogosa na wasaidizi wake, *Eng.* Machibya. Hawa wameweza kutusaidia shule ya kisasa ambayo Mheshimiwa Rais alikuja kuahidi katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hiyo nitoe kauli hapa kwamba imeshakamilika na sasa ipo katika hatua ya usajili ili iweze kupokea wanafunzi. Nawapongeza sana Shirika la Reli pamoja na Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kuwaahidi wananchi na kutoa maelekezo kwamba Shirika la Reli lijenge shule, na shule imejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika Sekta ya Nishati, Jimbo la Igalula wakati tunaingia tulikuwa na vijiji 12 ambavyo vimepata nishati kati ya 58. Leo tunamaliza miaka mitano chini ya Serikali ya Awamu ya Sita tumeweza kufikisha vijiji vyote 46 ambavyo vilivyokuwa vimebaki katika Jimbo la Igalula na vyote vimekwenda kuwa na nishati ya umeme, hata wananchi ambao walikuwa hawafikirii kupata nishati ya umeme, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amewafikishia wote. Hilo ni jambo la kumpongeza Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwenye Sekta ya Maji, maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi 2020 tulipewa maelekezo angalau kwenye vijiji kuwe kuna zaidi ya 80%, lakini Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso tumeshirikiana naye vizuri kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Rais alinunua mitambo ya kujenga mabwawa katika kila Mkoa. Katika Mkoa wa Tabora alipendekeza Jimbo langu liwe la mfano kutumia mitambo hiyo na tumeweza kujenga bwawa la kisasa ambalo Mheshimiwa Waziri na Kamati yake ilifika pale na wakalisifia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme lile bwawa lipo na ninaamini maelekezo ya Mheshimiwa Waziri ya kuleta zile kumalizia, ninaomba tumalizie mapema ili sasa wananchi waanze kupata maji kama tulivyokuwa tumetarajia; na Mheshimiwa Rais azma yake ni kwenda kuwatua akina mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji mimi ninafahamu tulipigana hapa mwanzoni lakini kwa nia njema ya kuwasaidia wananchi. Mradi wa Ziwa Victoria ambao ulikuwa unatakiwa kwenda kuhudumia kata za Kigwa, Goweko, Igalula na Nsololo, mradi ule unasemekana upo 85%, nami nawapongeza kwa kazi kubwa. Wakati naingia hapa, ulikuwa 0% lakini sasa hivi upo 85%. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusaidia fedha na kukamilisha kufika 85%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ilikuwa ni kuwafikia wananchi wa kata nne za Goweko, Igalula, Nsololo na Kigwa. Mradi ule wameshaweka maji katika kata moja tu. Sasa wasije wakamwandikia taarifa kule wameukamilisha. Kata tatu za Igalula, Goweko na Nsololo bado hawajafikisha, lakini mtandao wa kusambaza maji *DP* zimeshajengwa. Kilichobaki ni kuunganisha tenki moja kwenda lingine kilometa zaidi ya tisa, lakini sasa hivi wameshalaza bomba kilometa zaidi ya nne, bado kilometa tano wanavutana vutana na mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso akisema tu neno siku anafanya *wind-up* ya Waziri Mkuu, lile bomba linakamilika. Mwezi huu matarajio yetu mwezi wa Tano bomba liwe limeshafika katika kata zile tulizokuwa tumetarajia. Tunapokwenda kuzitafuta kura za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tusiwe na maswali mengi, ni kufungua bomba maji

yanatoka wananchi wanamimina kura badala ya kumimina maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya kilimo, tunaishukuru Wizara ya Kilimo imefanya kazi kubwa sana. Kwanza, ninyi mnafahamu tuliingia kwenye changamoto ya upatikanaji wa mbolea katika maeneo yetu, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema, mzigo wote tukiwatwisha wananchi kwenye maeneo yetu, hawawezi kupata chochote. Mheshimiwa Rais akaingiza ruzuku. Leo wananchi wanafurahia ruzuku ambazo Mama Samia aliwapatia. Leo mwananchi alikuwa anatakiwa kununua mfuko kwa shilingi 160,000/= mpaka shilingi 170,000/= lakini mwananchi anakwenda na shilingi 80,000/= au shilingi 72,000/= anapata mfuko anakwenda kulima, fedha nyingine zinalipwa na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo tunataka kwenda kuyasema na wale ambao wanataka kukimbia uchaguzi kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amemfikia mpaka mwananchi ambaye hakuwahi kusikia kama kuna Serikali inafanya kazi. Leo ukienda kila kitongoji kuna mwananchi amepata matunda ya Serikali ambayo anaiongoza. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali ambayo inaongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika Sekta hiyo ya Kilimo, katika mabwawa 120 ambayo yanajengwa nchi nzima, tumeweza kupata Bwawa la Goweko la Kilimo ambalo linaenda kujengwa na litalima zaidi ya ekari 1,000 ambayo wananchi watapata ajira, uzalishaji utakuwa mkubwa na watu watafanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, bwawa hili licha ya kuwa na changamoto, jana tumeongea na Mheshimiwa Waziri, tumekubaliana na ameniambia mkandarasi amepatikana wa *phase two* ya kwenda kutengeneza mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile bwawa lilikuwa lina zaidi ya shilingi bilioni mbili, lakini bwawa kukamilika lote linatakiwa

ligharamikie zaidi ya shilingi bilioni 32 na Mheshimiwa Waziri amesema mkandarasi ameshapatikana na anatafuta *advance payment* ya kumlipa ili sasa aingie kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata za Goweko niwaombe wawe watulivu, Mheshimiwa Rais amesikia kilio chao, bwawa kutoka shilingi bilioni mbili mpaka shilingi bilioni 32 siyo mchezo. Kwa hiyo, niwahakikishie, Mama Samia anafanya kazi na Waziri wa Kilimo anafanya kazi kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono Bajeti ya Waziri Mkuu, na sisi kama Wanaigalula tutaipitisha kwa kishindo na Bajeti Kuu ili waendelee kupata maendeleo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Venant Daud Protas. Kabla sijamruhusu mchangiaji anayefuata, naomba niwatangaze wageni waliopo Bungeni muda huu.

Tuna Wageni wa Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula ambaye ni Mbunge. Wageni hao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaosomea Sayansi ya Siasa *(Political Science)*. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunaendelea na mchangiaji wetu anayefuata ambaye ni Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Athuman Almas Maige, ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia hotuba iliyopo Mezani ya Makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niungane na Wabunge wote waliochangia kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kipindi cha miaka minne. Kwa kweli tukianza kuorodhesha hapa, nadhani hata Mheshimiwa Spika,

hataruhusu Bunge lifungwe kwa sababu kazi ni kubwa na ni nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naweza kusema yale ambayo yanatugusa sisi wanawake pamoja na mambo mengi ambayo yamesemwa, nina takribani sekta nne. Kwanza, ni sekta ya umeme ambapo tumeona mbali na kuunganisha umeme vijiji vyote 12,318 ambapo wanufaika wa kwanza ni wanawake, Mheshimiwa Rais pia ameibeba ajenda ya nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hapo kuna ajenda ya kumtua mama kuni kichwani na wewe unafahamu ambavyo wanawake walikuwa wanahangaika kutafuta kuni kwa ajili ya kupikia. Pia, kuna habari ya kumtua mama ndoo kichwani ambapo alipoanza kuibeba alipokuwa Makamu na mpaka sasa. Pia, Ilani ya Chama changu cha Mapinduzi, kwa kweli kwa mara hii imetekelezwa kwa kishindo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya tatu ni kilimo. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi, wanawake ndio tupo wengi 51%. Kwenye sekta ya uzalishaji hasa mashambani, wanawake ndio tunapofanya kazi huko. Mheshimiwa Rais kwa kutoa ruzuku ya mbolea na kule kwetu viuatilifu, ametupunguzia adha ya kutumia muda mrefu kukaa mashambani. Tunalima kidogo, tunapata mazao mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya nne ni ya afya. Unafahamu kila mahali kuna zahanati, vituo vya afya, Hospitali za Mkoa, Hospitali za Kanda za Rufaa. Naomba niende mahususi katika Mkoa wangu wa Mtwara. Sisi kule wananchi wa Mkoa wa Mtwara ni mashuhuda wa kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, lakini nitumie fursa hii pia kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa kwa namna anavyoratibu na kusimamia vyema shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mtwara kuna miradi mikubwa imetekelezwa. Hospitali ya Mitengwe ilitengewa shilingi bilioni 23.2

kwa ujenzi shilingi bilioni 15 na vifaatiba shilingi bilioni saba na hospitali ile sasa inatoa huduma. Kwa bandari tulipokea shilingi bilioni 56 na ujenzi umekamilika kuwezesha korosho zetu kusafirishwa kwa bandari. Uwanja wa Ndege awamu ya kwanza shilingi bilioni 51 umekamilika. Sasa hivi hata usiku ukitaka, peleka ndege yako yoyote Mtwara itatua. Awamu ya pili, shilingi bilioni 76 na kwa mara ya kwanza uwanja ule umetengewa fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maji, mimi huku ndiyo ninakofahamika kama mama wa maji ya kuokota. Pia, kwa kaka yangu Mheshimiwa Mhata pale kulikuwa kuna shida ya maji. Nikisema kwa kikwetu, inaitwa kiu. Kule kwake Nandete nimekwenda wanachota maji bombani, Likokona nimekwenda na kule wanasema hawana cha kumlipa kingine isipokuwa wanasubiri tarehe 25 ya mwezi wa Kumi tumpe malipo yake na maua yake kwa vitendo, daktari bingwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni baadhi tu. Ukisema shule, madarsa na vitu vinavyofanana na hivyo, kila kijiji ukienda utakuta alama iliyowekwa katika Serikali hii ya Awamu ya Sita na kazi nzuri iliyotekelezwa na Ilani ya Chama changu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi hiyo, sasa naomba nitumie fursa hii kujielekeza kwenye eneo moja tu ambalo nitatoa ushauri kwa Serikali yangu hasa kwenye kipande cha usafiri na usafirishaji ambapo hivi majuzi tumeona wananchi wanaotoka Mikoa ya Mtwara na Lindi walisota hapo tukisubiri Serikali yetu sikivu ifanye utaratibu wa kukwamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli natambua kazi nzuri iliyofanywa na Serikali yangu ya kuhakikisha mawasiliano au kule kukatika kwa barabara pale kunaondoka na usafiri uendelee. Pia, kwa kuwa sasa ni miaka miwili pale kumekuwa na tatizo, naomba nitumie fursa hii kushauri kwamba, pengine katika ule ukanda wetu kwanza itambulike kwamba ni ukanda wa pwani wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, barabara zake ni tofauti na kanda nyingine ambapo huko kunakuwa na ardhi kavu. Kwa hiyo, naomba nishauri, nimeona kwenye ule ukurasa wa 50 kifungu cha 133 kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, bahati nzuri yeye kwenye hiyo barabara sio mgeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vile vipande ambavyo vinasumbua tukubaliane mambo mawili. Jambo la kwanza, usanifu wake usilinganishwe na usanifu unaofanywa kwenye barabara nyingine, kwa sababu udongo wa pale kwetu na kwa kuwa upo ukanda wa chini na pia ni pwani, kwa hiyo, udongo wake hauwezi kuhimili mizigo mizito sana. Kwa hiyo, usanifu wake ungetofautishwa. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninaloishauri Serikali yangu Sikivu, ni gharama za matengenezo ya barabara kwa kuwa usanifu wake utakuwa ni tofauti. Barabara ile ya Kibiti – Lindi – Mtwara, Serikali ikubali kwamba itakuwa tofauti na maeneo mengine, kwa nini? Kwa sababu, usanifu huo sasa ukifanywa utawezesha barabara ile kwenye yale maeneo yaliyo chini kuinuliwa tuta ili maji yaweze kupita chini na hivyo itawezesha ile barabara kuwa ya kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Waziri wa Ujenzi anayehusika akisema kwenye sehemu 'X' anasanifu na kutumia kilometa moja kwa shilingi bilioni moja, pengine kwa lile eneo hata kama sijasoma hiyo *engineering* aliyosoma Mheshimiwa *Eng*. Kasekenya, lakini ninaamini ile adha tunayoipata pale ni ya muda mrefu. Niliwahi kukesha pale kwa siku mbili nilivyokuwa Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, na hatujawahi kuikomboa pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani gharama yake pale lazima tukubali kwamba barabara iinuliwe na maji yapite chini. Hii kukimbizana ya kupeleka mawe kwa hatua za dharura kama ilivyosemwa kwenye kitabu cha hotuba, nadhani tutakuwa tumepumzika kwa muda mrefu. Kwa hiyo, tukifanya hivyo, naamini kabisa tutakuwa tumeiondoa ile adha. Kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Waswahili wanasema, mito yote inapeleka maji baharini, na kwenye ule ukanda ndiko kunakopita mito mingi. Kule Somanga Mto Matandu, sijui Mto Mbwemkuru, sijui mto nini, ile mito yote inahitaji usanifu wa tofauti na maeneo mengine ili kuwezesha barabara ile kuwa ya kudumu na ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninashauri kwenye usafiri na usafiri na usafirishaji ni ujenzi wa barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi. Natambua kuna eneo ambalo pia mkataba wa zile kilometa 82 umesainiwa, kuna eneo ambalo bado tunasubiri. Ni rai yangu, ninaisihi sana Serikali yangu sikivu, basi huo utaratibu ukamilike kwa haraka kwa sababu kwa sasa pia barabara hiyo ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo lingine ni barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale. Baada ya ule utaratibu wa *EPC + F*, kwenye swali hapa niliuliza na Mheshimiwa Waziri alijibu kwamba kuna utaratibu mwingine utakaotumika wa kusanifu na kujenga. Naiomba Serikali yangu kwamba, kwa kuwa huko nako ndiko mito hiyo inakotokea, ndiko inakoanzia, inaenda kutua huko baharini, kwa hiyo, barabara imekuwa na usumbufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, huo ushauri wangu, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana sana sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sina namna nzuri ya kusema. Kwa barabara yetu ya Mnivata – Tandahimba – Newala wakandarasi wako *site* na kazi inaendelea. Ndiyo kusema, kazi na utu tunaendelea kusonga mbele kwa maendeleo. Hiyo kwa kweli kwetu sisi ni namna ambavyo tunaona Serikali hii imefanya mambo makubwa, lakini kimsingi yote ni kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi aungana na wale Wabunge waliosema kwamba hizo kelele nyingine zitasemwa tu, lakini mwezi wa 10 uchaguzi utafanyika na sisi tutaweka kura za kishindo kwa ajili ya kumchagua Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri iliyofanywa, pamoja na Wabunge wote wa Chama cha

Mapinduzi, na utaratibu ule wa mafiga matatu wa Madiwani wote wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Agnes.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo. Nilimtaja Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao ajiadae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu mimi nichangie hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayohusu mwelekeo wa bajeti, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka huu 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wale wawili, Makatibu Wakuu, na Watendaji wote wa Wizara hizi mbili ambazo Kamati yangu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii inasimamia. Wamefanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi hii ya kuandaa hotuba ambayo imekusanya mambo yote kwa ujumla, anastahili pongezi kubwa yeye na watendaji wake wote. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameisoma karibu kwa saa mbili, lakini sisi Wabunge tunachangia tu kwa muda mfupi, dakika 10 mpaka 15. Nimechagua mambo machache ambayo nitayachangia, ambayo nafikiri kwamba yalikuwa muhimu katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; pili, ni programu ya kukuza ujuzi; na la tatu, miradi iliyoko Jimboni kwangu, pia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo inatunza na kulipa pensheni za wafanyakazi waliostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, kila mwaka Serikali inapanga bajeti ya shilingi bilioni moja kwa muda wa miaka mitano, lakini fedha hizo hazitoki, kwa muda wote wa miaka mitano imetoka shilingi bilioni moja tu. Matokeo yake ni nini? Serikali ilipanga kusomesha vijana 42,000 kwa mwaka, lakini nafasi zimepungua, sasa wamefikia vijana 10,000 na bado inapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linatuletea tatizo kwa sababu Serikali ina wazo zuri, sera nzuri ya kuwafundisha vijana ujuzi ili waweze kujitegemea, lakini bahati mbaya sana fedha hizi hazitoki, na tunaishauri Serikali sasa izitoe hizo fedha. Nina hakika Mama Samia Suluhu Hassan, Daktari huyu mwenye upendo, utu na mlezi, anatusikia. Kwa kweli tuna imani kwamba fedha zitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nilitaka kuongelea ni kuhusu programu ya ujuzi kwa vijana wapya wanaotoka shuleni, ujuzi kwa wafanyakazi walioko kazini na *source* au chanzo cha fedha hii ni makato ya tozo ya asilimia 3.5 wanaolipa waajiri kwa wafanyakazi wao wote wanaomaliza, wanaosoma, wanaofuzu katika kazi zao wanataka wakasome, vilevile wanapeleka hizi fedha Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, fedha hizi zikifika Hazina hazitoki. Pia, nina mifano mizuri miwili hapa, mwaka 2022 na 2023 Serikali ilikusanya, maana yake Mfuko mzima huu wa tozo tulikubaliana na Serikali kwamba Serikali itatoa theluthi moja iende kwa ajili ya mafunzo ya mafunzo haya ya ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka 2022/2023 Serikali ilikusanya ile theluthi moja sawa na shilingi bilioni 124.7, lakini walipeleka shilingi bilioni tisa tu kwa ajili ya mafunzo haya. Mwaka 2023/2024 Serikali ilikusanya tozo hiyo theluthi moja yake, shilingi bilioni 119.6 lakini walipeleka kwa mfuko huu huu wa mafunzo ya ujuzi, shilingi bilioni tisa, matokeo yake imekuwa hayo niliyoyasema, kwamba, badala ya kusomesha wanafunzi 47,000 tumesomesha wanafunzi 8,000 tu kwa mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utendaji wa kazi kwa Serikali, ya Mama Samia Suluhu Hassan, hakuna mtu anayeuliza kwamba Mama amefanya kazi kubwa na anastahili pongezi. Tungejuaje kama tatizo la umeme lingeisha nchini bila kumalizia Bwawa la Mwalimu Nyerere? Tungejuaje kwamba madaraja yangejengwa? Tungejuaje kwamba angeweza kujenga shule, angeweza kujenga *SGR* na kadhalika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ninatoka Jimbo la Tabora Kaskazini ni bora nikatoa mfano mzuri wa Jimbo la Tabora Kaskazini tena kwa kisekta. Nianze na sekta ya afya. Tulikuwa hatuna hospitali ya Wilaya, tumejengewa hospitali ya Wilaya. Tulikuwa hatuna vituo vya afya, tumejengewa vitatu, tulikuwa hatuna zahanati katika baadhi ya Kata, tumejengewa zahanati nane mpya. Katika sekta ya maji, visima na mitandao ya maji vijijini, tunapata maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vijiji vyangu 98, sasa vijiji 60 vinapata maji ya Ziwa Victoria, tunafungua maji ya Ziwa Victoria chini ya miti, ni huyu Mama Samia Suluhu Hassan peke yake. Hakuna mtu ambaye angefanya mambo makubwa namna hiyo tukaona. Tunasema alama hizi katika Jimbo langu haziwezi kufutika, tutamkumbuka. Nasema kila siku, tunamwona Mama Samia kwa kuona vitu alivyotuwekea, au alama alizoziweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu tumejengewa shule za sekondari tatu, tumejengewa shule za Kidato cha Tano na cha Sita shule tatu. Pia, tumejengewa madarasa mengi sana, tumejengewa chuo cha *VETA*, na hiki chuo cha *VETA* ni muhimu sana. Zamani ilikuwa, Jimbo langu ni la vijijini, ukiharibikiwa gari kijijini upige simu mjini aje fundi umlipe na aondoke na hela, na umaskini unabaki vijijini. *(Makofi)i*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujenga chuo cha *VETA*, wametokea mafundi wa umeme, mafundi wa magari, mafundi wa kujenga, kwa hiyo, sasa hivi hela inazunguka. Hili ni wazo kubwa la Mama Samia, lazima tumpongeze sana. Ule uchumi unazunguka kule vijijini sasa, hata ukinunua televisheni siyo lazima

aje akufungie mtu kutoka mjini, anakufungia mtu kutoka kijijini na anapata fedha za kuposa pale pale kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya nishati, vijiji vyangu 98 vyote vina umeme na vitongoji 15 tumepata na sasa hivi tumepata vitongoji 86 vitakavyowekwa umeme. Hili siyo jambo dogo la kupuuzia kupongeza na asiyeshukuru kwa dogo hata kubwa hashukuru. Tunamshukusu sana Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utawala bora, tumeingia madarakani Wilaya ya Uyui haina majengo yake, tumepata kwenye majengo ya *DC* kama madarasa. Leo tumejengewa majengo mazuri na ukumbi mzuri wa kisasa, unafungua milango kama ya Bunge. Ukisogea mlango unafunguka na Wanyamwezi tulizubaa kwanza tukashangaa, lakini sasa hivi hatushangai tena, kama Bungeni hapa, ukisogea mlango unafunguka. Kijijini na Makao Makuu ya Wilaya na Halmashauri yangu iko Isikizya pale kijijini kabisa. Pia, tumejengewa Mahakama kama utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo, sisi Tabora tunalima tumbaku. Tabora ilikuwa na hali mbali haijapata kutokea. Mimi waliniita Mzee wa Tumbaku hapa kama mnakumbuka. Nilikuwa naidai Serikali inunue tumbaku iliyobakia kule, hawataki kununua. Leo tumbaku inagombaniwa. Serikali imetafuta wanunuzi wa tumbaku na masoko ya tumbaku na leo tumbaku inanunuliwa na mpaka inayobakia wanunuzi wanagombania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo changamoto mbili tatu katika Jimbo langu na ambazo bahati nzuri sana maelezo yake ninayo. Kwa mfano, kumalizia Kituo cha Benjamin Mkapa katika Kijiji cha Migungumalo, Kata ya Usagale. Hizi zilikuwa ahadi za Marehemu Mheshimiwa Benjamin Mkapa, lakini pia ilikuwa ahadi ya Marehemu Mheshimiwa Dkt. Magufuli na ilikuwa ipo ahadi ya Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimeongea na Wizara husika ya TAMISEMI, wamesema kwamba fedha zipo na Wizara ya Fedha

imetuthibitishia. Kituo hiki kikijengwa, basi wananchi wangu wa Kata ya Usagali na kata za karibu pale watapata kituo cha afya ambacho kilikuwa ni ahadi ya viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nina jambo dogo la gari la wagonjwa. Jimbo la Tabora Kaskazini au Wilaya ya Uyui ina majimbo mawili. Jimbo la Igalula na Jimbo la Tabora Kaskazini. Hapa tulipewa *ambulance* kila Mbunge, apeleke *ambulance* hiyo anakotaka. Hiyo *ambulance* nilikuwa nimepanga kuipeleka katika Kituo cha Afya cha Upuge, lakini busara, hospitali ya Wilaya ambayo imejengwa Jimboni kwangu haina *ambulance*, kwa hiyo, nikapeleka ile *ambulance* ya Upuge, nikaipeleka Wilayani. Upuge wanatembea kwa miguu, wanawabeba wanawake wenye mimba kwenye machela, hawawezi kukaa kwenye bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa na Waziri wa Afya na ninaomba nijivunie hapa, ameniahidi kwamba, zile *ambulance* ambazo zitatoka bandarini, moja itaenda Upuge. Namshukuru sana Mama Mhagama, nakushukuru sana, Mheshimiwa Waziri wa Afya. Pia, Mheshimiwa Dkt. Dugange nakumbuka nilikuomba hii, basi tuishie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mwongozo wake kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *NSSF, PSSSF* na *WCF*. Pia, Mfuko wa Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi. *(Makofi)*

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, nipe dakika moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko hii imefanya kazi kubwa sana. Sheria ya juzi tuliyopitisha hapa tumewapa Wakurugenzi madaraka au mamlaka ya kuwalipa watu wanaodai pensheni malipo badala ya kungojea kwanza waajiri wapeleke fedha. Hili limekuwa ukombozi mkubwa kwa wana-*pensionable* wote,

hawatakuwa wanalala tena barabarani, kwenye *corridor* za mashirika kuomba fedha kwa sababu waajiri hawakupeleka fedha kwenye mifuko, sasa hili suala limeisha na hizi ni kura za Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Athuman Almas Maige. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Bajeti hii ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naungana na Wabunge wengine kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa bajeti yake nzuri na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya hasa Jimboni kwangu Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli miaka hii mitano ambayo nimekuwa hapa Bungeni, Serikali imeweza kunisikiliza kwa kiasi kikubwa, na nimepata fedha nyingi ambazo wananchi wa Ludewa wamezishangaa. Nawashukuru sana wananchi wa Ludewa kwa kuniamini, kuendelea kuniunga mkono na kunipa moyo ili kazi yangu ya kuwatafutia maendeleo iweze kuwa nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nikianza na sekta ya elimu, miaka hii mitano Ludewa tumepata shule mpya za sekondari zipatazo tano. Vilevile tumepata shule mpya za msingi mbili. Shule moja ya msingi wananchi wakaona iitwe jina la Joseph Kamonga. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa heshima hiyo waliyonipa na mimi Ludewa siyo Mbunge wa kwanza, ni Mbunge wa kumi, ni Mbunge ambaye nimeingia nikiwa mtoto mdogo kuliko Wabunge wote, lakini wananchi wameweza kutambua

mchango wangu na kuweka kumbukumbu ya kuita ile shule jina la Jospeh Kamonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawahakikishia wananchi wa Ludewa kwamba niko imara, nina nguvu, bado nina uwezo wa kuendeleza pale ambapo tumeachia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la elimu kuna shule ambayo wananchi wa Ludewa, wakati huo Mkuu wa Wilaya alikuwa anaitwa Andrea Sere, (nisipomtaja huyu *DC* nitakuwa sijamtendea haki), alichangisha shilingi mia tano mia tano, shilingi elfu moja, shilingi elfu tano, shilingi elfu kumi, wananchi wakaweza kujenga shule kwa ajili ya watoto wenye ufaulu wa juu pale Ludewa. Madiwani tulipoingia tukaimalizia, tulikuta madarasa mawili pale, wakaipa jina Ludewa Kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hii inakuwa ya kwanza kwa shule za Serikali kwa Mkoa wa Njombe, lakini ilijengwa na wananchi wote wa Wilaya ya Ludewa. Shule hii kwa maendeleo iliyonayo na inavyosaidia watoto wenye ufaulu wa juu, wananchi wamenituma niiombe Serikalini iweze kuiongezea hata madarasa matatu, ambayo ni shilingi milioni 75 tu. Najua hii kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni jambo dogo sana, akitoka hapa ninaamini ataenda kutafakari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumepata Shule ya Sekondari Lubonde, tumepata Shule ya Mafunzo kwa Vitendo, Shule ya Amali pale Mlangali ya shilingi bilioni 1.6 imekamilika, imesajiliwa na mwezi wa tano tunatarajia watoto wataanza kupata mafunzo kwa vitendo. Tunashukuru pia tumepokea walimu kwa ajili ya shule hii. Haya ni mafanikio makubwa sana kupatikana kwa Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, pale Masasi napo tumeshamaliza Shule ya Sekondari *Chief Dustan Masasi*, nayo inatarajiwa kuanza mwezi huu, imeshasajiliwa tayari kwa kupokea wanafunzi. Pale Lugarawa tumejengewa miundombinu, karibia madarasa 19 na mabweni mawili, tayari imeshasajili Kidato cha Tano na cha Sita, tunatarajia mwezi wa saba wataanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari Mchuchuma mwaka 2024 Kidato cha Tano walianza pale ambapo mwaka huu wataingia Kidato cha Sita. Kwa hiyo, kwenye elimu sekondari kwa kweli tumepata mambo mengi yakiwemo mabweni tisa mapya, na nyumba nane za walimu, pamoja na maabara 12. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri na kubwa ambayo imefanyika Jimboni kwangu Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye sekta ya afya, hospitali ya Wilaya ya Ludewa ilikuwa imechakaa sana, Serikali imeweza kutuwekea pale zaidi ya shilingi bilioni mbili, miundombinu mingi imebadilishwa imerekebishwa na kuwa ya kisasa kabisa. Vilevile, tumejengewa zahanati mpya karibia 27, kati ya hizo, zahanati 21 tayari zimeshaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, tumewapunguzia wananchi mwendo wa kutembea kilometa nyingi kwenda kufuata huduma ndogo ndogo za afya. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa hili na tunaomba watumalizie ile Zahanati ya Chanjale ambayo wananchi bado wanatembea kilometa 17. Zimebaki fedha kidogo tu na kupata wahudumu wa afya kwa sababu, Mkurugenzi amejitahidi sana, alipeleka pale shilingi milioni 20, bado fedha chache tu ili wananchi wa Chanjale waanze kupata huduma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sekta ya Afya vilevile tumeweza kupewa shilingi milioni 400 na boti, kwa ajili ya kusaidia dharura za Ziwa Nyasa. Waheshimiwa Madiwani na wataalamu walienda kulikagua, ni boti zuri sana, baada ya siku 14 litakuwa limekamilika na tutaweza kulipeleka Jimboni Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba, hapa pia, kuna Kituo cha afya kimoja kinaitwa Mavanga. Ni kituo cha *mission,* kinatoa huduma hasa kwa akina mama wa masuala ya uzazi, ila tu wana changamoto ya *ambulance*. Pale Wizara ya Afya kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama kama kuna gari *Landcruiser* ambalo linaweza likafaa kuwa *ambulance,* wapo tayari kwenda kulirekebisha ili waendelee kuhudumia akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunashukuru sana pale Mundindi tumeweza kupata fedha zaidi ya shilingi milioni 700. Tumemalizia kituo kile cha afya na sasa kinahudumia wananchi, ila tu wanaomba wataalamu kidogo, watumishi waongezwe ili waweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, wanashukuru pale Kituo cha Afya Mundindi, baada ya kukamilika, Serikali ilipeleka *ambulance* mpya kabisa tena nilipewa mwenyewe nikaenda kuikabidhi pale. Nishukuru sana kwa heshima ile ambayo nilipewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija eneo la miundombinu ya Barabara, Serikali pia imefanya kazi kubwa sana, tumejengewa kilometa 50 za barabara za zege kuanzia pale Lusitu mpaka Mawengi, barabara ambayo imegharimu kiasi cha shilingi bilioni 179. Ni fedha nyingi, barabara ile ni bora na tunaambiwa ina uwezo wa kudumu kwa miaka isiyopungua 60. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutujali Ludewa, sambamba na lile Daraja la Mto Ruhuhu ambapo, alivyokuja kuomba kura alivuka kwenye pantoni, alivyoondoka nami nilivyosemeasemea hapa Bungeni, tuliweza kupata fedha nyingi karibu shilingi bilioni nane tukamaliza lile daraja na leo linasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye barabara za vijijini, kuna vijiji ambavyo wananchi walikuwa wanazaliwa mpaka wanafariki miaka 90, 100, hawajawahi kuona gari, lakini awamu hii tumeweza kufikisha gari Lumbila na tumeweza kufikisha gari Makonde. Siku ya kwanza gari linafika pale Makonde watoto wote walikimbia kwenda kufichama, wanaogopa gari, yaani wanadhani labda kuna vita. Kwa hiyo, miaka hii mitano yaliyofanyika kule yalikuwa ni kama muujiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu ile barabara ya kwenda Lumbila, kutokana na maporomoko ya vifusi kidogo maeneo machache yalizibaziba, lakini tunashukuru Serikali iliweza kutuingiza kwenye Mradi wa Benki ya Dunia ili tuweze kupata zaidi ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuboresha na kujenga *concrete strips* kuwasaidia wananchi wale kule kandokando ya Ziwa Nyasa,

ambao mtu anazaliwa, anakufa miaka 100, kuwapelekea barabara hiyo ni zaidi ya ibada. Kwa hiyo, wananchi wale waangaliwe zaidi, barabara ziweze kujengewa zile *concrete strips* na mitaro kwa sababu, zipo kwenye miteremko ya Milima ya *Livingstone,* ili zisije zikageuka kuwa mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna ile Barabara ya Mbwila kwenda Lifuma. Nashukuru sana watu wa *TARURA* walituidhinishia kiasi cha shilingi bilioni moja ili tuweze kukamilisha barabara ya kwenda Nkwimbili, huku nako wananchi wanapata karaha kubwa sana. Nkwimbili – Kilambo – Ntalawanda mpaka Nsisi hii ni barabara muhimu, inaweza kuunganisha wananchi wa kata karibia tatu na Makao Makuu ya Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Jimbo la Ludewa vilevile tunaishukuru sana Serikali kwa kutoa fedha. Tumeweza kutengeneza barabara nyingi na kuzifungua, ila tunaomba awamu nyingine bajeti iweze kuongezwa zaidi ili kujengwe mitaro kwa sababu, maji ndio yanayoharibu sana barabara na Wilaya ya Ludewa ni eneo ambalo lina wakulima wengi sana. Kwa hiyo, barabara, kama kule Ibumi nilikwenda wiki iliyopita, Barabara ya Ludewa kwenda Ibumi na ile ya Amani kwenda Ibumi. Barabara hizi ni ukanda wa uzalishaji mkubwa sana, mwananchi mmoja anavuna magunia mpaka 8,000 ya mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru watu wa *TARURA* nazo waliziingiza kwenye Mpango wa Fedha za Benki ya Dunia. Kwa hiyo, fedha hizi zikitoka, barabara ikaboreshwa, itaenda kusaidia na ule mradi ambao Mheshimiwa Rais ameuleta, wa Kilimo cha umwagiliaji. Kuna mradi mkubwa kule, lakini vilevile kuna lile daraja ambalo linajengwa linalounganisha Wilaya ya Mbinga na Wilaya ya Ludewa, ambapo Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 2.9. Tulipata bahati mbaya, wakandarasi walikuwa wanatelekeza kazi, lakini tumekubaliana na watu wa *TARURA* waweze kusimamia sheria vizuri, ili barabara hii na nyingine ziweze kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa yote, naomba sana, ile barabara inayoanzia Itoni – Ludewa mpaka Manda na Mkiu –

Liganga mpaka Madaba ziweze kukamilishwa kwa sababu, Serikali ilishalipa fidia kiasi cha shilingi bilioni 15. Muda siyo mrefu uwekezaji wa Liganga na Mchuchuma unaanza, uwekezaji huu unakwenda sambamba na miundombinu bora ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi zikiboreshwa itakuwa ni rahisi sana kwa wawekezaji wanaokwenda Liganga na Mchuchuma kuweza kufanya shughuli zao vizuri, lakini pia, wananchi wa Ludewa wanaweza kuepukana na usumbufu ambao wamekuwa wakiupata kwa muda mrefu. Zipo jitihada za Serikali, natambua walishalipa shilingi bilioni 4.7, lakini mkandarasi aliomba aongezewe shilingi bilioni tano ili aweze kurudi *site* na nguvu yote kwa sababu, mitambo anayo na ile ni kampuni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali kwa sababu, ule mradi ni wa fedha nyingi zaidi ya shilingi bilioni 114, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, hajawahi kutuangusha, akimwongezea fedha hizo naamini mkandarasi anaweza akarudi kazini na tunapokuja kuzungumzia masuala ya uchaguzi mambo yatakuwa safi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulisemea ni Kilimo. Wananchi wa Ludewa ni wakulima, wanategemea kilimo na ombi lao kubwa kwa Serikali ni soko la mazao ya mahindi ambayo wanalima kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashukuru mwaka 2023 walinunua tani 709, lakini mwaka 2024 watu wa kilimo wameweza kuongeza ununuzi mpaka kufikia tani 5,200. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa sana, wakulima wengi wamepata fedha na mwaka huu pia 2025, Ludewa tuna mahindi mengi sana. Kwa hiyo, wanaomba waweze kuandaliwa soko na ikiwezekana kwa Wizara ya Kilimo, tukapata *godown* kwa sababu, mwaka 2024 wangeweza kununua mahindi mengi zaidi, ila maeneo ya kuhifadhi yalikuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashukuru kwa ruzuku ya mbolea, wakulima wameweza kupata zaidi ya tani 15,000 za

mbolea ya ruzuku. Jambo hili limeongeza tija kwenye Kilimo, wananchi wamepata fedha, wameweza kusomesha watoto na leo sasa ndiyo maana wananituma niweze kuiomba Serikali iwaajiri watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naishukuru sana Serikali na nitamke kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga. Tunaendelea na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii nami niweze kuchangia hoja iliyopo Mezani. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyoonesha namna ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imetekeleza ilani yake vizuri pamoja na Mawaziri wake waliopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jimbo la Tunduru Kusini ni moja ya majimbo yaliyopo pembezoni mwa nchi yetu likipakana na Msumbiji kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa Wilaya hii ya Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwani kuna miradi minne ambayo imekwenda vizuri, hasa miradi ya afya. Tuna vituo vya afya viwili vilivyoboreshwa mpaka sasa vinafanya kazi ya upasuaji na vituo vingine viwili vipya vinaendelea kukamilishwa, ili viweze kutoa huduma ya upasuaji. Kwa kweli, kwa sisi watu wa Tunduru Kusini, kwetu sisi ni faraja kubwa sana kwa sababu, tulikuwa tunatembea mwendo mrefu kufuata hospitali ya wilaya, kwa ajili ya changamoto za akinamama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika hilo la afya, tumejengewa zahanati tisa ambazo zimekamilika, saba zinatoa huduma, mbili zinaweza kutuo huduma hivi karibuni. Tunashukuru

sana kwa sababu, katika vijiji 65, vijiji 22 vilikuwa na zahanati, sasa tumeongeza zahanati tisa na kufanya kwenye Jimbo la Tunduru Kusini kuwa na zahanati 31. Tunaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nashukuru sana kwenye Sekta ya Elimu, kwani tunazo shule za sekondari nne mpya. Kati ya kata 15 nilikuwa na shule za sekondari nane, lakini kipindi hiki kifupi cha Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumepata sekondari nne mpya. Mbili zimeanza kutoa huduma, mbili bado zinaendelea kujengwa pamoja na sekondari moja ya amali. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, tumeboresha sekondari mbili; Sekondari ya Mchoteka ambayo imeboreshwa kuwa ya Kidato cha Tano na Sita na Sekondari ya Tuwemacho, nayo imeboreshwa. Kwa kweli, Jimbo la Tunduru Kusini kielimu tulikuwa hatuna Kidato cha Tano na cha Sita, ni historia ya kwanza kupata Kidato cha Tano na Sita katika shule hizo mbili, tunashukuru sana, hasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, Jimbo la Tunduru Kusini 99% ni wakulima ambao wanategemea kuendesha maisha yao kwa Kilimo, hasa Kilimo cha Korosho. Kwanza tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo msimu uliopita wakulima wamepata fedha nyingi sana kutokana na bei iliyotokana na uuzaji wa Mfumo wa *TMX,* tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Bashe kwa kusimamia vizuri *TMX.* Kwa kweli, wananchi wa Tunduru Kusini wanaandaa zawadi ya kumpa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na fedha nyingi zilizotokana na hali iliyokuwa biashara nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, kuna changamoto kubwa sana ya ugawaji wa pembejeo. Tunashukuru Bodi ya Korosho kusimamia vizuri na kuweka Maafisa Ugani kusimamia zao la Korosho kila kata. Tunashukuru sana kwa

sababu wanafanya kazi zao kuwa karibu na wananchi na mwananchi akiwa na changamoto anawaona ili waweze kusaidiana, lakini kwenye jambo hili mfumo wa kugawa pembejeo mwaka uliopita ulikuwa na dosari kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hawa Maafisa Ugani waliokuja, wengi baada ya kuandikisha mashamba hawakupata pembejeo, uwazi wa kugawa pembejeo ulikuwa ni mdogo. Sasa hivi wameanza kuandikisha upya na kusajili mashamba ya wakulima, usajili unaenda vizuri, lakini kumeanza kujitokeza changamoto. Mtu alikuwa na shamba la eka 40, akienda pale anaambiwa wewe shamba lako ni eka 30 au eka 18; badala ya kwenda kuhakiki shamba wanaanza kuvutana na kumwandikia eka 38, kitu ambacho hakuwanacho tangu awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili litasababisha baadhi ya wakulima kupata pembejeo kidogo kuweza kuhudumia mashamba yao, hili jambo halijakaa vizuri. Kwa kweli, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa kuruhusu *Export Levy* 100% isaidie kuhudumia zao la korosho na pembejeo zinagaiwa bure, lakini kuna wajanja ambao wanatumia fursa hiyo kufanya wakulima wasipate haki yao ya msingi ya pembejeo ambayo inatokana na *Export Levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili naomba nishauri jambo lifuatalo. Kwanza usajili ukikamilika, kwa vile usajili ule unaonesha mkulima ana mikorosho mingapi, ana eka ngapi na hesabu zinaeleweka, basi ni vizuri kila mkulima, kila chama cha msingi au kijiji waweke mabango kwenye vijiji vyao ili waoneshe kila mkulima atapata *sulphur* kiasi gani? Dawa za maji kiasi gani? Hapo atakapokwenda na *token* yake inakuwa ni rahisi, kwamba anajua yeye ana mifuko 30 badala ya kuambiwa na wale wenzetu, wataalamu kwamba, wewe una vifuko 18 kumbe kwenye *system* ipo mifuko 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uwazi huu ukienda, kwa kweli, wakulima watakuwa wameenda vizuri sana na kuweza kuhudumia mikorosho yao vizuri na hii imesababisha ukulima wetu wa korosho na uzalishaji kupanda. Sisi mara ya mwisho tulizalisha

tani 18,000, lakini mwaka 2024 tulipata tani 30,000. Ni historia ambayo haijawahi kutokea tangu tumeanza kulima korosho katika Wilaya yetu ya Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto ya ugawaji wa pembejeo, sisi kama wakulima, tunaishukuru sana Serikali. Kupewa ruzuku kwenye mbolea ni jambo ambalo limemfanya kila mkulima alime kulingana na uwezo wake, lakini changamoto bado tumeijadili, inaonekana inashindikana kutumia vyama vya msingi katika kugawa pembejeo, hasa mbolea kwenye vijiji vyetu. Wakulima bado wanatembea mwendo mrefu kufuata mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijijini mbolea ya ruzuku haipatikani. Tulikubaliana wapitie vyama vya msingi, lakini vyama vya msingi vimeshindwa kuweza kuwahudumia wakulima wao kwenye hii mbolea ya ruzuku. Kwa hiyo, tunaomba jambo tulilokubaliana kwenye vikao mbalimbali, Bodi ya Mbolea ijitahidi kusambaza mbolea mpaka maeneo ya wakulima ili wapate kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye Sekta ya Kilimo, kwenye masuala ya maghala, vyama vingi vya msingi havina maghala. Maghala ya vijiji mengi yamechoka, uhifadhi wa mazao umekuwa ni mdogo, ufanisi na faida ya mazao umekuwa ni mdogo sana. Naiomba Serikali, kupitia Wizara ya Kilimo, ione namna ya kuongeza kasi ya kujenga maghala kwenye vijiji vyetu, ili wakulima waweze kuhifadhi mazao yao kwenye maghala yaliyo bora ambayo yatasaidia ubora kuwa ule ule badala ya kutumia maghala ambayo ni hafifu na mara nyingi vyama vya msingi vinatumia kupanga nyumba za watu, ili kuhifadhi mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nilipenda sana nilichangie ni kwenye suala la miundombinu ya barabara. Wenzangu wa Kusini wamezungumza nyuma, juu ya ubovu wa Barabara ya Lindi. Sisi watu wa Tunduru kupitia Songea, ni parefu. Njia yetu sahihi ni kupita Lindi. Ukitoka Tunduru mpaka Dar es Salaam ni kilometa 800. Tukipita Songea ni kilometa 1,300. Kwa hiyo, njia yetu kubwa ya kwenda Dar es Salaam ni kupita

Barabara ya Lindi. Ukweli ni kwamba barabara ile ni mbaya, ina mashimo na bahati mbaya au nzuri, kuna malori mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024 nilizungumza juu ya Serikali kuona umuhimu wa kutengeneza meli ya Serikali ambayo itafanya biashara kati ya Mtwara – Dar es Salaam – Komoro na Zanzibar, kama wanavyojenga kwenye maziwa makuu. Hii itasaidia mizigo mikubwa ya makaa ya mawe na *cement,* ambayo ni zaidi ya magari 300 kwa siku yanapita Tunduru kwenda Mtwara na kwenda Dar es Salaam, ili kupeleka makaa ya mawe pamoja na *cement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kwenye jambo hili waone namna ya kuunda meli ambayo itatoa huduma kwenye Bahari yetu ya Hindi kutoka Lindi, Mtwara, Komoro, Dar es Salaam na Tanga. Hili jambo litatusaidia, lakini sambamba na hilo, mkakati wetu wa kujenga reli ya Kusini bado ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mheshimiwa Kamonga, Ludewa, makaa ya mawe ya kwake yatakuwa na faida, kama reli ile itajengwa kutoka Mtwara – *Mbamba Bay* na mapacha yake kwenda Ludewa kwa ajili ya kusafirisha makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la reli litasaidia barabara zetu za Songea – Makambako Kupona. Barabara zetu za Mbinga kwenda Songea – Tunduru mpaka Dar es Salaam na Mtwara Kupona kwa sababu, mizigo ile inayosafirishwa ni mikubwa sana kiasi kwamba, inafanya barabara yetu ishindwe kuhimili vishindo vya mizigo ambayo itasafirishwa katika reli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, napenda nizungumzie Barabara ya Tunduru kwenda Nalasi, Mtwara Pachanne. Barabara hii ni ya kimkakati na bahati nzuri tumepata mwekezaji wa *copper,* ambaye anajenga kiwanda cha kuchenjuwa *copper* katika Kijiji cha Mbesa, ambacho kina uwezo wa kuchenjuwa *copper* tani 500 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili, ujenzi huu, utasimama kwa sababu ya kutokuwa na barabara nzuri, madaraja yaliyokuwepo kutoka Tunduru mpaka Mbesa kupitia Lusewa mpaka kufika Mtwara Pachanne hayana uwezo wa kusafirisha zaidi ya tani 15. Kwa hiyo, tunaomba mkakati wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara Pachanne – Lusewa – Nalasi mpaka Tunduru Mjini uwe wa kudumu ili ile biashara ya *copper* pale iweze kufanyika ipasavyo kwa sababu, ina uchumi mkubwa, kwa ajili ya nchi yetu na Wilaya ya Tunduru kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa nawakosea watu wa Tunduru bila kusema suala la tembo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tumepata ndege nyuki wawili wanaendelea na kufukuza tembo, lakini bado ghasia imekuwa ni kubwa. Naiomba Wizara, ahadi yake ya kujenga vituo kwa ajili ya kufukuzia tembo, vitatu Kusini, vitatu Tunduru Kaskazini itekelezeke ili kuondoa adha kwa wananchi wetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa mkubwa wa wakulima wetu wa Tunduru ni kukosa mazao yao ambayo yanaliwa na ndovu kwa maana ya tembo. Ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate. Tunamalizia na Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi ya mwisho. Nilikuwa kwenye shughuli za Kamati. Kwa hiyo, nilichelewa kidogo na hivyo nikakaa huku nyuma. Kwa hiyo, usishangae sasa kwamba nipo huku mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri sana ambayo anawafanyia Watanzania. Ametuletea hotuba nzuri sana ambayo inaakisi utendaji wake wa kazi. Hotuba hii pamoja na mambo mengine imebeba mafanikio makubwa ambayo nchi yetu imepata ndani ya kipindi cha miaka minne cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi yaliyosemwa kwenye hotuba yake ambayo ni mazuri sana, lakini nitazungumza machache ambayo ninadhani yanabeba yale yote ambayo yapo kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na Bwawa la Nyerere, la kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya maji la Julius Nyerere, lipo 99% sasa hivi, ambalo sasa linakaribia kumalizika linakuja kubadilisha maisha ya Watanzania, linaboresha maisha ya Watanzania, na kufanya maisha ya Watanzania kuwa ya furaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa *(SGR)*. Reli hii *section* ya Dar es Salaam – Morogoro mpaka Dodoma imekamilika kwa ajili ya abiria. Sasa hivi sensa ya uchumi ya wananchi wa Morogoro, Dodoma hata Mwanza imebadilika. Kuna watu wanatoka Mwanza na magari wanakuja wana-*park* Dodoma wanaingia kwenye *SGR* wanakwenda Dar es Salaam. Wananunua mizigo yao wanapanda treni wanarudi hapa, wanasubiri mizigo yao wanaisafirisha kwenda Mwanza na Rwanda. Kwa hiyo, imebadilisha maisha ya Watanzania wengi kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)*. Tulianza na ndege moja wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano sasa zipo ndege 16. Tumerudisha *identity* yetu kwenye anga, tulikuwa tumepotea. Kwa kweli tunapongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita. Hii imewekwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ameiweka vizuri, ameweka bayana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ukamilishaji, kuna usambazaji wa umeme wa *REA*, sasa hivi tuna vitongoji 15 ambavyo kazi inaendelea kwenye Majimbo yetu. Kwenye Jimbo langu kwa mfano baada ya hivyo vitongoji 15 nitakuwa nimebakiza vitongoji kama 68. Naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ilikuwa ndefu, ameisoma kwa saa mbili. Mimi nimesema nimetaka hayo machache ambayo yanachukua nafasi ya yale mengine mengi ambayo yapo kwenye hotuba hii. Niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuletea hotuba nzuri ambayo inaakisi utendaji kazi wake mzuri. Nampongeza sana yeye, Mawaziri walioko chini yake, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara yake kwa kazi nzuri ambayo wanawafanyia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona mwanaume ametoka vizuri ujue nyuma yake kuna mwanamke *smart*. Sasa mimi ninasema kiongozi akiwa *smart* nyuma yake kuna kiongozi mkubwa wake ambaye yupo *smart*. Niseme kwamba kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ina-*reflect* kazi nzuri ambayo anatufanyia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kipekee kabisa kumshukuru kwa jinsi ambayo ametutendea haki na wema, na kwa kazi nzuri iliyofanyika na jimbo langu nalo limenufaika kwa kiwango kikubwa. Sitaweza kuzungumza yote, lakini nizungumzie sekta chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na elimu; ndani ya miaka minne nimepata shule za sekondari tisa mpya. Ipo Sekondari ya Amsha Kata ya Ambureni, ipo Sekondari ya Madiira Kata ya Seela Sing'isi, ipo Sekondari ya Seela, Kata ya Seela Sing'isi, ipo Sekondari ya Samaria Kata Maroroni, ipo Sekondari ya Shambarai Burka Kata ya Shambarai Burka, ipo Sekondari ya Uwiro Kata ya Uwiro, ipo Sekondari mpya ya Karangai Kata ya Kikwe, zipo Sekondari mbili King'ori, Meru na ya Umoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata shule nyingi. Tumepata pia shule mpya ya mfano ya *primary* Kata ya Katiti, Kijiji cha Nasholi. Juu ya yote tumepata shule mpya ya Amali ambayo inajengwa Kata ya Makiba Kijiji cha Valeska. Ujenzi unaendelea vizuri na wakati wowote wanafunzi wataanza kuingia madarasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na shule tuna Chuo cha *VETA* kinajengwa Kata ya Uwiro kazi, inaendelea vizuri, tunaamini mwaka huu wanafunzi wataanza kuwa *enrolled*. Tutapata vijana watakaofundishwa ufundi wa umeme, ufundi wa magari, ufundi wa ujenzi wa nyumba, ufundi wa *welding* na mambo mengi ambayo yatawawezesha vijana kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana, nilisema umeme wa *REA* unaendelea kusambazwa vizuri jimboni kwangu. Tunaamini kwamba huu mradi ambao unakuja wa vitongoji 9,000 utakuja kutumalizia sisi tatizo la umeme jimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, bado tumepata miradi mingi ya maji. Kata ya Akheri na Kwa Rusamu tulipata mradi wa maji wa shilingi 3,200,000,000. Mradi umemalizika na sasa hivi wapo kwenye hatua ya kusambaza maji kwenye nyumba za watu. Kata za Imbaseni, Maji ya Chai, Kikatiti hadi Samaria, Kata ya Maroroni tumepata mradi wa shilingi 6,100,000,000. Mkandarasi yupo kazini, na tunaamini kabla hatujaenda kwenye uchaguzi, na ndivyo tunavyoomba, wananchi watakuwa wanakunywa maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Uwiro kuna mradi wa maji wenye thamani ya shilingi 4,000,000,000. Tunaamini wakati wowote mkandarasi ataanza kazi kwa sababu shughuli za manunuzi zilikuwa zimeshamalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za King'ori, Leguruki, Maruvango, Malula na Ngarenanyuki zinapata maji kutoka kwenye msitu wa Mlima Meru. Maji haya yana *fluoride* kwa wingi. Kuna mdau wa maendeleo, Taasisi ya *KOICA* waliamua kutusaidia kutuletea mitambo ya kusafisha na kuondoa *fluoride* kwenye maji yale. Mitambo hiyo imeshaanza kufanya kazi lakini

kwa kiwango kidogo kwa sababu inatumia *solar* kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge hili kwamba Serikali ipeleke umeme wa gridi kwenye ile mitambo ili ifanye kazi kwa kiwango ambacho kimekuwa *installed,* kwa maana ya lita 2,000,000 kwa siku ili wananchi wale waendelee kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo niliuliza kwamba, umeme utapelekwa lini? Mheshimiwa Waziri hakuweza kunijibu kwa sababu hakukumbuka kwamba lile eneo ni wapi? Nimkumbushe kwamba ni Leguruki, Kijiji cha Nkoasenga eneo la Bwawani. Ile mitambo imeshafungwa, inasafisha maji, na sasa hivi inasafisha maji lita 200,000 kwa siku, lakini uwezo wake ni lita 2,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi ya kusema. Nashauri kwamba ahadi za Viongozi Wakuu huwa zinatolewa mbele ya wananchi wengi sana. Kwa hiyo, wanasikia wengi wajanja na ambao sio wajanja na wanachukua kama ilivyosema. Kuna ahadi nyingi sana zimetolewa. Kule kwangu kuna ahadi ya ujenzi wa Barabara ya King'ori kuanzia Malula hadi Ngarenanyuki kwa kiwango cha lami, ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ni kwamba, nimesikia kwamba miradi yote ambayo ni ahadi ya Viongozi Wakuu inawekwa kwenye mpango mwaka huu. Nategemea basi kwamba hiyo Barabara ya King'ori na kilomita tano pale *Usa River* na nyingine zitawekwa kwenye mpango ili hatimaye mambo yetu yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi ya kusema, kwa leo naona niishie hapa, ujumbe wangu umefika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, ambaye ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru na kuwapongeza wote ambao mmechangia kuanzia asubuhi ya leo. Pia nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe chini ya usimamizi wake kwa kuvumilia na kuwepo muda huu na kusikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge. Mwenyezi Mungu awabariki sana na awajalie kazi njema.

Baada ya kusema hayo, nawatakia mapumziko mema ya siku ya Jumamosi na Jumapili na hivyo ninaahirisha shughuli za Bunge hadi tarehe 14 mwezi wa Nne, 2025 siku ya Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.10 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 14 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*